# Nipashe

Ijumaa Agosti 16, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579998

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



ST.JOSEPH UNIVERSITY In Tanzania

"WHERE YOUR DREAMS ARE NURTURED"

Calling all Old Students of SJCET, SJCIT, SJCMC, SJCHS and SJUIT-ARUSHA

SJUIT invites its Alumnus for the Alumni meet from 4:00PM-9:00PM on **24th August, 2019,** "Entrance is free". For details **www.alumni.sjuit.ac.tz**

For more information contact: +255 676 504 147 +255 745 281 505

215359802




## Spika Ndugai aomba muda kujibu hoja za Tundu Lissu

UKURASA 4

# Kardinali Pengo ang'atuka rasmi



• **Papa** aridhia kustaafu kwake, Askofu Ruwa'ichi akabidhiwa mikoba ...*Endelea ukurasa 4*

## YALIYOMO


UKURASA WA 5

**MAJERUHI WENGINE 7 AJALI LORI LA MAFUTA WAFARIKI**

MAJERUHI wengine saba katika ya 46 waliopokelewa katika Hospitali ya Taifa...

UKURASA WA 5

**MALINZI AJITETEA ANAIDAI TFF DENI LA MIL. 152.6/-**

RAIS wa zamani wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Jamal Malinzi, amedai...


UKURASA WA 7

**MUDA KUOMBA MIKOPO VYUO VIKUU WAONGEZWA**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imetangaza kuongeza...


## RAS atengua uamuzi wa DC

UKURASA 4



Rais Dk. John Pombe Magufuli, akipongezana na mgeni wake, Rais wa Jamhuri ya Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, baada ya kubadilishana zawadi, Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# JPM, Ramaphosa watangaza neema

• **Waahidi** manufaa makubwa kiuchumi Tanzania na Sauzi, Mkapa atoa neno ajira kwa vijana...*Uk.2& 3*


**MICHEZO** **AZAM FC YAIFURAHIA SIMBA JUMAMOSI** UK.31 **MAONI, KATUNI** UK.6




# Hasunga: Tutaimarisha biashara ya mazao SADC

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKARI imesema kuwa imejipanga kuimarisha biashara ya mazao ya kilimo na mengineyo kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), ili kuwanufaisha wakulima katika nchi hizo.

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi 16 wanachama wa SADC.

Alisema kuwa zaidi ya Watanzania milioni 50 wanategemea chakula, hivyo lazima kubadili mbinu za uzalishaji katika mazao ya kilimo kwa kuongeza tija kupitia teknolojia mpya ili kuwa na uzalishaji mkubwa na wenye tija.

Waziri Hasunga alisema kuwa malighafi zinazohitajika zaidi ya asilimia 66 zinatokana na mazao ya kilimo, hivyo ukamilisho wa serikali ya viwanda unaungwanishwa kwa ukaribu na sekta ya kilimo.

Kwa mujibu wa Hasunga, Mkutano wa SADC ni fursa kwa wakulima wa Tanzania kwa kuwa wageni wote waliowasili na watakaoendelea kuwasili watahitaji kula vizuri, hivyo mkutano huo ni sehemu ya kuimarisha na kutangaza masoko ya mazao mbalimbali hususani vyakula vya asili.

Aidha, utoshelevu wa chakula nchini ni asilimia 119 ukilinganisha na mwaka jana ambapo ulikuwa asilimia 124, hivyo serikali imefungua mipaka ya kuuza mazao nje ya nchi, lakini pia ni lazima kuwa na kumbukumbu muhimu za taarifa zote za usafirishaji wa mazao.

Waziri Hasunga alisema ni wakati mwafaka kwa nchi za Afrika Mashariki na nchi zote za SADC kuanza kutumia masoko ya ndani ya nchi katika mazao ya kilimo na mengineyo kuliko kutegemea kuagiza katika nchi zingine nje ya Afrika.

Alisema kuwa kufanya hivyo kutaimarisha masoko ya mazao mbalimbali nchini, hivyo kuwaimarisha wakulima katika kilimo chao, na kuwa na kipato kikubwa kinachokidhi mahitaji ya kila mkulima pamoja na uimara wa uchumi wa nchi.

# JPM, Ramaphosa waahidi neema

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS John Magufuli amemwomba Rais wa Afrika Kusini, Matamela Ramaphosa, kuwahamasisha zaidi wafanyabiashara wa Afrika Kusini kuja kuwekeza nchini kwa kuwa Tanzania inayo dhamira ya dhati ya kuongeza ushirikiano wake na nchi hiyo katika nyanja mbalimbali za kiuchumi.

Rais Magufuli aliyasema hayo jana Ikulu Jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na wananchi kupitia vyombo vya habari muda mfupi baada ya kufanya mazungumzo na Rais Ramaphosa ambaye aliwasili nchini juzi jioni kwa ziara ya siku 3 na baadaye kuhudhuria Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) utakaofanyika jijini kesho na keshokutwa.

Katika mazungumzo hayo yaliyotanguliwa na mapokezi rasmi yaliyofanyika katika Viwanja vya Ikulu, Rais Magufuli alisema katika kutekeleza mipango yake ya maendeleo na dira ya kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025, Tanzania inawakaribisha wawekezaji mbalimbali.

Alisema kwa kuwa Afrika Kusini imepiga hatua kubwa katika viwanda, anawaalika wafanyabiashara wa nchi hiyo kuja kujenga viwanda vya kuzalisha bidhaa mbalimbali zikiwamo dawa na vifaa tiba, kuchakata madini na kwamba Serikali itatoa ushirikiano utakaohitajika.

Rais Magufuli pia alimwomba Rais Ramaphosa kuongeza ushirikiano na Tanzania katika utalii, hasa ikizingatiwa nchi hiyo inapokea watalii zaidi ya milioni 10 kwa mwaka ikilinganishwa na watalii milioni 1.5 wanaoingia nchini.

Katika kufakikisha suala hilo, Rais Magufuli alitoa wito kwa Afrika Kusini kuongeza safari za treni ya watalii na kwa wawekezaji wake kuja kuwekeza katika hoteli na fukwe za Tanzania.


Kuhusu biashara, Rais Magufuli alisema Afrika Kusini ni nchi inayoongoza kwa kufanya biashara na Tanzania ikilinganishwa na nchi nyingine za SADC, akibainisha kuwa asilimia 70 ya bidhaa za Tanzania zinazokwenda SADC huenda Afrika Kusini.

Alisema biashara kati ya Tanzania na Afrika Kusini imeendelea kukua, akibainisha kuwa mwaka jana, ilikuwa na thamani ya Sh. trilioni 2.687 ikilinganishwa na mwaka 2017 ilipokuwa na thamani ya Sh. trilioni 2.528.

Rais Magufuli pia alimpongeza Rais Ramaphosa kwa kuja na wafanyabiashara ambao wanajadiliana na wafanyabiashara wa Tanzania juu ya kushirikiana kibiashara na akamhakikishia kuwa Tanzania itadumisha ushirikiano huo.

"Sisi Tanzania tumeamua kuwa tunanunua bidhaa zetu Afrika Kusini badala ya kununua bidhaa hizo huko mbali, na kwa kuanzia pikipiki za kuongozea misafara ya viongozi tutakazotumia wakati huu wa Mkutano wa 39 wa SADC

INAENDELEA UK.8




Rais mstaafu wa Awamu ya Tatu, Benjamini William Mkapa, akihutubia katika mhadhara uliokuwa ukizungumzia historia ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), uliofanyika katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam jana. **PICHA: CATHBERT KAJUNA**

# Mkapa atoa angalizo vijana kukosa ajira

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS mstaafu wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa, amewataka viongozi wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) kuwekeza zaidi katika kuwajengea uwezo vijana ili wajiajiri.

Amesema viongozi wa SADC wanapaswa kuwajengea mazingira mazuri ya kupata ajira vijana ambao ndiyo idadi kubwa ili waziendeleze rasilimali zilizoko katika nchi zao.

Mkapa alitoa rai hiyo jana katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) wakati akiongoza mjadala wa kikanda wa mtangamano wa SADC.

"Idadi kubwa ya wananchi wa SADC ni vijana, tunapaswa kuwaandaa vyema, elimu yetu inapaswa kuwaandaa katika kujiendeleza wenyewe, wanapaswa kujengwa katika ujuzi na uchumi wa kidijitali," Mkapa alishauri.

"Ili kufanikisha hayo, ni lazima kuwapo kwa ushirikiano wa pamoja baina ya sekta binafsi na serikali katika kusaidia utekelezaji wa sera ya kutokomeza umaskini miongoni mwa nchi wanachama pamoja na mabadiliko ya teknolojia."

Mkapa pia alisema kuna haja kutolewa elimu ya kutosha kuhusu umuhimu wa ushirikiano wa SADC na kuendeleza mikakati kama vile kuchochea ushirikiano baina ya viongozi, akieleza kuwa ndiyo njia pekee ya kufikia uchumi huru.

Alisema miongoni mwa mambo ambayo SADC imefanikiwa kwa kiasi kikubwa ni kuimarisha amani na usalama miongoni mwa nchi wanachama.

"Hata hivyo, bado kuna changamoto ambazo nimeziona zinaikabili jumuiya hii kama vile umaskini miongoni mwa jumuiya, uzalishaji mdogo wa bidhaa na ubovu wa miundombinu," Mkapa alisema.

Alisema umoja na mshikamano kati ya viongozi wa jumuiya hiyo ndiyo utasaidia kuondoa vikwazo hivyo, akibainisha kuwa changamoto zilizopo sasa ni tofauti na za miaka iliyopita.

Mkapa pia aliwataka viongozi wa SADC kutafuta wawekezaji wazuri watakaowekeza kwenye viwanda na teknolojia.

Katika mjadala huo, Makamu Mkuu wa UDSM, Prof. William Anangisye, alisema: "Sisi, UDSM tunafurahi kusikia kuwa mojawapo ya lugha ya mawasiliano itakayotumika katika vikao vya SADC ni Kiswahili, hata sisi hapa chuoni tumeanza jitihada za kukitangaza Kiswahili kwani tuna idara inayofundisha lugha hiyo."






Mke wa Rais Mama Janeth Magufuli akikabidhi zawadi ya picha kwa mke wa Rais wa Afrika Kusini, Dk. Tshepo Motsepe-Ramaphosa, baada ya kuwasili Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Elimu kuifanya SADC ukanda wa viwanda

**Na Gaudensia Mngumi**

JUMUIYA ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), itafanikiwa kwenye uchumi wa viwanda iwapo mataifa hayo yatawekeza zaidi na kuongeza bajeti ya elimu.

"Bila elimu bora ni sawa na kupiga risasi hewani kusiko na shabaha. Hakuna maendeleo ya viwanda wala uchumi kama raia hawana elimu bora."

Ni ushauri wa Matildah Mwamba, kutoka Zambia alioutoa wakati wa mkutano wa asasi za kiraia (NGOs) za SADC zilizokutana kutoa maoni na mapendekezo kuhusu elimu kabla ya mkutano wa wakuu wa SADC unaoanza kesho jijini Dar es Salaam.

Mwamba, ambaye ni Meneja Miradi wa Mtandao wa Kampeni ya Elimu kwa Wote Afrika, (Ancef), alisema hakuna maendeleo na viwanda bila raia kuwa na elimu bora, na kuzitaka serikali kukusanya na kutumia kodi kuboresha elimu.

Julie Juma, Meneja wa International Education Program wa shirika la kimataifa la Action Aid linalohamasisha masuala mengi ya maendeleo Afrika, aliwakumbusha viongozi wa SADC kuwa hakuna sababu ya kutegemea wengine kugharamia elimu ya raia wake.

Aliwataka viongozi hao kuzingatia Kanuni ya Afrika kuhusu elimu , iliyokubaliwa nchini Ivory Coast na kupewa jina la Abidjan Principles.

Julie alisema kanuni hiyo inaziagiza serikali kutenga zaidi ya asilimia 20 ya bajeti zake kugharamia elimu bora kwa raia wote, wakiwamo wenye mahitaji maalumu na wa kipato kidogo.

Aidha, kanuni zinaagiza elimu bora ya msingi na yenye viwango kupatikana kwa raia wote na serikali ikigharamia jukumu hilo. "Aidha, serikali zihakikishe kuwa muda wote kunakuwa na fedha za kutosha kugharamia mafunzo ya walimu, vifaa vya kazi na taaluma pamoja na kuifanya elimu kuwa endelevu. Yote haya yanawezekana kupitia kodi," alisema Julie.

Meneja huyo alizitaka asasi za kirai kutumia Kanuni za Abidjan kubana Serikali kwenye elimu.

Fillipe Sambo kutoka Msumbiji, akisisitiza kuhusu fedha za kugharamia elimu bure, alitaka Serikali zisimamie, kukusanya na kuhakikisha matumizi bora ya kodi.

"Afrika na SADC hupoteza fedha kupitia misamaha ya kifisadi ya kodi, utoroshaji fedha nje usiodhibitiwa, rushwa na ufisadi," alisema. "Msumbiji inapoteza dola milioni 31 kila mwaka misamaha ya kifisadi ya kodi, lakini milioni 69.4 hupotea kutokana na utoroshaji haramu wa fedha. Hii ni mifano tu, shida hii ipo sehemu nyingi Afrika."

Alizitaka NGO na umma kudai na kufuatilia haki zao kwa kuwa serikali zimesaini mikataba na makubaliano ya kuwaletea maendeleo.

# TADB yaasa taasisi za fedha SADC

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), imesema fedha ya uhakika ya kujenga miundombinu ya maendeleo katika nchi za SADC itatoka ndani na hasa itapatikana kwa kujenga ubia wa kimkakati baina ya taasisi za fedha zilizomo katika jumuiya hiyo.

Pia imeshauri kukazania kuongeza thamani mazao ya kilimo. Akiwasilisha mada jijini Dar es Salaam katika mkutano wa nne wa mwaka wa maendeleo ya viwanda katika nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, alisema historia inathibitisha kwamba nchi za Afrika hazitofanikiwa katika shabaha yake ya kujenga miundombinu ya maendeleo iwapo zitategemea fedha kutoka nje ya bara hili. "Tutaongeza minyororo ya thamani ya mazao ya kilimo katika nchi za jumuiya yetu iwapo tutaenzi kila aina ya ubia wa kimkakati baina yetu. Sisi TADB milango yetu iko wazi. Tuko tayari kuzungumza na taasisi ya fedha ya aina yoyote katika kanda yetu juu ya njia bora kujenga ubia wa kimkakati na wenye tija," Justine amezihakikishia nchi wanachama wa SADC.

Aliwaambia wajumbe hao kwamba umuhimu wa kuwapo kwa fedha ya kujenga miundombinu ya maendeleo katika Afrika unajulikana, lakini aliongeza kwamba kwa bahati mbaya kuna pengo kubwa kati ya mahitaji na fedha iliyopo ili kujenga miundombinu hiyo.

Alisema makadirio ya pengo ni dola za Marekani bilioni 130 kwa mwaka, lakini yawezekana makadirio halisi ni dola 170 bilioni kwa mwaka. Justine alisema uwezo uliopo kuzipa pengo hilo ni kidogo, sana sana ni uwezo wa kuziba nusu ya pengo hilo au usifikiwe. Misaada rasmi (ODA) nayo imekuwa ikiporomoka toka 2013 na mitaji ya uwekezaji (FDI) kuingia Afrika nayo imekuwa ikiporomoka toka mwaka huo, alieleza.

Alishauri zifanywe jitihada za kutafuta vyanzo mbadala na mifano ya kugeuzwa katika kupata fedha ya kujenga miundombinu ya maendeleo na viwanda.

Kwa mujibu wa Justine, fursa zilizopo kwa sasa ni kujitahidi kupata fedha kutoka mifuko ya jamii, mifuko inayojitegemea, kampuni za bima na hata watu binafsi wenye uwezo. Amewakumbusha wajumbe umuhimu wa kilimo katika kuiendeleza Afrika, na SADC na kusema kwa bahati mbaya kilimo kimekuwa kikipewa fedha kidogo sana na wakulima wadogo wamekuwa hawapewi msukumo wa kutosha kuzalisha mazao kwa tija.

"Afrika ina uwezo wa kuilisha dunia kwani nusu ya ardhi murua kwa kilimo ya dunia na ambayo haitumiki iko Afrika. Afrika ina maji mengi. Lakini Afrika inatumia dola bilioni 35 za Marekani kununua chakula kutoka nje kila mwaka. Afrika inaweza kuilisha dunia ikiwa itawajali wakulima wadogo ili kilimo kiwe na tija na endelevu," alisema.

## Wawekezaji Afrika Kusini wakaribishwa

**Na Beatrice Moses**

RAIS John Magufuli amewakaribisha wawekezaji kutoka Afrika Kusini kuwekeza viwanda vya nguo, viwanda vya dawa na vya magari, na maeneo mengine yatakayowavutia.

Akizungumza jana wakati wa mkutano wa Baraza la Wafanyabiashara wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) uliowakutanisha wafanyabiashara wa Tanzania na Afrika Kusini, alisema mahitaji ya kutengeneza nguo kwa pamba inayozalishwa nchini, pamoja na mazao ya nyama, wanaweza pia kuzalisha viatu na bidhaa zingine zitokanazo na ngozi.

Alisema lengo ni kupunguza bidhaa ghafi zinazokwenda nje ambazo zikitumika katika nchi husika, zitaweza kuzalisha ajira nyingi kwa vijana.

"Milango ipo wazi kwa ajili ya wawekezaji, tuna samaki katika bahari na maziwa, tunataka kufikia mahali ambapo tunaweza kuzalisha bidhaa zetu hapahapa ndani ya nchini," Rais Magufuli alisema.

Alielezea jinsi serikali yake ilivyojipanga katika kukuza sekta ya viwanda na uwekezaji, imeandaliwa mifumo wezeshi kuwezesha Tanzania kufanikiwa kuwa ya viwanda.

Alitaja baadhi ya miradi ambayo imewekwa kwenye mfumo wezeshi wa viwanda ni kuboresha upatikanaji wa nishati katika bonde la Rufiji, ujenzi wa miundombinu ukiwamo ujenzi wa viwanja vikubwa vya ndege, barabara na reli

Rais Magufuli alieleza jinsi serikali anayoiongoza ilivyoweza kufufua Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) na kuwezesha kununuliwa kwa ndege kadhaa, hivyo kuwa na usafiri wa anga unaoanzia nchini.

"Zipo ndege zinazokwenda Afrika Kusini mara nne kwa wiki, hii itasaidia kuwezesha biashara na uwekezaji, lakini pia kukuza utalii wa ndani kati ya nchi zetu mbili, bandari nazo zinatanuliwa na kujengwa," alisema.

# Kardinali Pengo ang'atuka, Ruwa'ichi awa mrithi rasmi

**Na Romana Mallya**

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki duniani, Papa Mtakatifu Francisko, ameridhia ombi la kustaafu, Polycarp Kardinali Pengo, Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam.

Wakati huo huo, Papa Francisko amemteua Askofu Mkuu Mwandamizi wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Yuda Ruwa'ichi, kuanzia sasa kuwa Askofu Mkuu wa Jimbo hilo.

Taarifa iliyotolewa jana na Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Padri Dk. Charles Kitima, ilieleza kuwa Balozi wa Baba Mtakatifu nchini, anataarifu kuwa kuanzia jana Baba Mtakatifu Fransis amekubali ombi la Kardinali Polycarp Pengo la kustaafu katika majukumu ya kuongoza Jimbo Kuu la Dar es Salaam.

"Askofu Mkuu Ruwa'ichi ambaye mpaka sasa ni Askofu Mwandamizi, anachukua rasmi majukumu ya kuliongoza Jimbo Kuu la Dar es Salaam," taarifa hiyo ilieleza.

Akizungumza na Nipashe, Padri Kitima alisema kwa utaratibu wanapostaafu, Kardinari Pengo hafungwi kwenda popote anakotaka, ingawa lazima akae kwenye jimbo.

"Kama ataamua kubaki Dar es Salaam hafungwi, akiamua kwenda jimbo alikobatizwa anaruhusiwa, popote atakapoamua yeye kwenda hakatazwi, ila hawezi kurudi nyumbani kwao bali atakaa kwenye jimbo lolote atakalolichagua ili akaishi huko," alisema.

Alisema tangu kuanzishwa kwa Jimbo Kuu la Dar es Salaam mwaka 1953, aliyeanza kuliongoza ni Askofu Mkuu, hayati Edgar Marantha na baada ya mwaka 1969 Hayati Laurian Kardinali Rugambwa. Kardinali Pengo alisimikwa kuwa Askofu Mkuu wa Jimbo hilo Julai 22, mwaka 1992 baada ya kustaafu kwa mtangulizi wake, hayati Laurean Kardinali Rugambwa.

**ALICHOSEMA PENGO KABLA YA KUSTAAFU**

Agosti 5, mwaka huu, Kardinali Pengo akiwa katika maadhimisho ya kumbukumbu ya miaka 75 tangu kuzaliwa kwake, aliwaambia watu wa Mungu Jimbo Kuu la Dar es Salaam kwamba, anasubiria wakati wowote kumtii Baba Mtakatifu Francisko atakapomwambia kupumzika katika utume wa kiaskofu.

"Nasubiria kumtii Mwenyezi Mungu wakati wowote atakaponiita na kuniambia pumzika kwa daima.

"Kuna kaburi langu pale Pugu, naomba liheshimiwe. Nawahisi viongozi wote wa kanisa, waumini na wengine wote, nikifa nizikwe kwenye kaburi langu la Pugu.

INENDELEA UK. 26



Askari Polisi akimzuia mwendesha pikipiki asiendelee na safari katika eneo la Daraja la Selander, jijini Dar es Salaam jana, kufuatia agizo lililotolewa na jeshi hilo la kupiga marufuku vyombo hivyo kuingia katikati ya Jiji, hasa kwa kipindi hiki cha Mkutano wa SADC unaoendelea. **PICHA: JOHN BADI**

## RAS atengua uamuzi wa DC

**Na Happy Severine,** BARIADI

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Simiyu, Jumanne Sagini, ametengua uamuzi uliotolewa jana na Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Festo Kiswaga wa kuwataka watumishi 137 wa Hospitali ya Halmashauri ya mji wa Bariadi (Somanda) kuchanga fedha na kulipia mashine ya ultra sound iliyoibwa.

Sagini alitengua uamuzi huo wakati akiongea na watumishi wa hospitali hiyo na kueleza kuwa jambo hilo haliwezi kuwa la kila mtumishi kwa kuwa sio wote walioshiriki katika tukio hilo.

Alisema ni vema na lazima wakatafutwa wahusika na wizi huo ili waweze kurejesha mashine hiyo na si kuwaadhibu watumishi wote.

Sagini alisema, mkoa umeangalia na kubaini kuwa sio watumishi wote 137 wa hospitali hiyo walioshiriki katika wizi huo kwa kuwa wengine walikuwa mapumziko, likizo hivyo si haki kuhukumu wote.

"Awali DC wangu aliwauliza watumishi kama wanatambua mhusika wa wizi sambamba na kuwapigisha kura za siri, lakini hakuna aliyekubali kubaini wapi ilipo ultrasound au kumtambua mhusika na ndipo DC akaamua kuchukua hatua ambazo ni sahihi, lakini kama mkoa tunasikitishwa na kitendo hiki cha wizi wa mashine hiyo, ukizingatia tumewakabidhi hospitali hata mwezi haujaisha kimeibiwa...pia tutambue kuwa sisi tuna vyombo vya dola ambavyo vina watu wanalipwa kwa shughuli hii, hivyo nawaomba wahusika warejeshe kifaa hicho," alisema Sagini.

Katibu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali, Catherine Dickson, alisema uamuzi wa Mkuu wa Wilaya ya Bariadi wa kuwataka watumishi wote kulipa kifaa hicho kimsingi ni kinyume na utaratibu kisheria na kwamba wanaushukuru uongozi wa mkoa kwa kutambua sheria, kanuni na taratibu kwa kusitisha uamuzi huo na kuviachia vyombo vya sheria vifanye kazi yake.

Naye mmoja wa watumishi wa hospitali hiyo, Flora Katoyo, ambaye anahudumu kitengo cha dawa, alisema ameshukuru tamko hilo lililotolewa na uongozi wa mkoa kwa kuwa limekuwa faraja kwao.

# Ndugai aomba muda zaidi kumjibu Tundu Lissu

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imesema Ijumaa ya wiki ijayo itasikiliza ombi la muda la kuzuia kuapishwa kwa Mbunge Mteule wa Jimbo la Singida Mashariki, Miraji Mtaturu (CCM), itakaposikiliza maombi ya kupinga kuvuliwa ubunge wa jimbo hilo, yaliyofunguliwa na Tundu Lissu aliyekuwa mbunge wake.

Vilevile, upande wa walalamikiwa katika kesi hiyo umeomba mahakama iwape muda wa kuandaa majibu ya kiapo kinzani ili kupata busara za Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mahakama hiyo imepanga kusikiliza maombi ya msingi ya Lissu dhidi ya Spika wa Bunge, Job Ndugai, na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Agosti 23, mwaka huu, mbele ya Jaji Sirilius Matupa.

Jaji huyo alisema ombi hilo la kuzuia kuapishwa kwa mbunge mteule limo ndani ya maombi ya msingi na lina hoja nyingi za kikatiba na kisheria na kwamba mahakama yake haina taarifa kuhusu Bunge kuanza vikao ndani ya siku 14 zijazo vitakavyowezesha mbunge huyo kuapishwa.

Alisema mahakama yake itasikiliza maombi yote na uamuzi utatolewa.

Upande wa mlalamikaji uliongozwa na mawakili; Peter Kibatala, Jeremiah Mtobesya na Omary Msemo.

Awali, Kibatala aliomba mwongozo wa mahakama hiyo kama itaweza kusikiliza ombi hilo na kutoa amri ya muda ya kuzuia uapishwaji wa Mtaturu.

Alidai lengo la ombi hilo ni kulinda maana ya maombi ya msingi ambayo wajibu maombi wataenda kuyajibu.

Hata hivyo, upande wa walalamikiwa ulioongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Vicent Tangoh, uliomba ombi dogo na ombi la msingi yasikilizwe kwa pamoja.

Upande huo wa walalamikiwa pia uliomba mahakama iwape muda wa kuandaa majibu ya kiapo kinzani ili upate busara za Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

"Mtukufu Jaji, maombi haya yanagusa mhimili mwingine wa serikali, hivyo tunaomba muda tupate ushauri wao ili tuandae majibu ya kiapo hicho kinzani," Tangoh alidai.

Wakili huyo wa walalamikiwa alidai atawasilisha majibu ya kiapo kinzani Agosti 21 na wakili wa mlalamikaji atawasilisha hoja za nyongeza Agosti 22 na mahakama itasikiliza maombi hayo Agosti 23, mwaka huu.

Kwa mujibu wa maombi hayo namba 18 ya mwaka huu, Lissu anaiomba mahakama hiyo impe kibali cha kufungua kesi ili mahakama hiyo itoe amri ya kumtaka Spika Ndugai ampe (Lissu) taarifa yake ya kumvua ubunge.

Pia, mtaalamu huyo wa sheria anaiomba mahakama hiyo impe kibali cha kufungua kesi ili mahakama hiyo iite taarifa ya uamuzi wa Spika wa kumvua ubunge na kisha itengue na kutupilia mbali uamuzi huo wa Spika Ndugai kumvua ubunge.

Mwombaji huyo pia anaomba mahakama impe kibali afungue shauri ili mahakama itoe amri ya kusimamisha kuapishwa kwa Mbunge Mteule wa Jimbo la Singida Mashariki, Mtaturu.

Katika hati ya dharura, Lissu anaiomba mahakama hiyo isikilize na kutoa uamuzi wa maombi yake haraka vinginevyo, Mtaturu ambaye Julai 19, mwaka huu alitangazwa mshindi na msimamizi wa uchaguzi wa jimbo hilo, ataapishwa kushika wadhifa huo.

Lissu anadai atakuwa ameathirika kwa kuwa atapoteza haki zake zote, kinga na maslahi yake yote yanayoambatana na wadhifa wake huo wa ubunge.

Uamuzi wa kumvua ubunge Lissu ulitangazwa na Spika Ndugai Juni 28, mwaka huu, wakati akiahirisha mkutano wa 15 wa Bunge, akitaja sababu mbili.

Spika Ndugai alizitaja sababu hizo kuwa ni kushindwa kuhudhuria vikao vya Bunge kwa muda mrefu bila kumjulisha Spika kwa maandishi mahali aliko na sababu ya pili ikiwa ni kutokujaza taarifa za mali na madeni kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

## HABARI KITAIFA

# Malinzi ajitetea anaidai TFF milioni 152.6/-

**Na Hellen Mwango**

RAIS wa zamani wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Jamal Malinzi, amedai mahakamani kwamba wakati wa uongozi wake mpaka alivyokamatwa na kushtakiwa bado analidai shirikisho hilo zaidi ya Sh. milioni 152.6.

Malinzi anayekabiliwa na mashtaka ya kughushi na kutakatisha fedha aliwasilisha jana taarifa ya benki ya mwaka 2014 na risiti 13 zilizoonyesha TFF kumlipa Malinzi fedha za mkopo alizokuwa anawadai.

Ushahidi wa utetezi wa kigogo huyo ulisikilizwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Maira Kasonde.

Mbali na Malinzi washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni aliyekuwa Katibu Mkuu wa TFF, Selestine Mwesigwa, Mhasibu wa TFF, Nsiande Mwanga na Karani Flora Rauya.

Akiongozwa na Wakili Richard Rweyongeza, Malinzi alidai katika taarifa ya benki ya kuanzia Januari, 2014 hadi Agosti 19, 2014 alikuwa anaidai Sh. 152,613,004.83 na kwamba kuna Dola za Marekani 5,000 ambazo alizitoa nchini Msumbiji hazikuingizwa kwenye mfumo huo badala yake waliingiza kwa mkono. Alidai fedha hizo zilipobadilishwa kuwa Shilingi, jumla ilikuwa Sh. milioni 8.3 na kwenye taarifa hiyo waliandika kuwa "kiasi unachotudai kwa mujibu wa kumbukumbu zetu ni Sh. 152,613,004.83."

Malinzi alidai uingizaji wa fedha hizo ulikuwa kwa njia mbalimbali ni kuweka kwenye akaunti za TFF na kutoa fedha taslimu kwa Shilingi au Dola.

Alidai alipokuwa anapewa fedha walikuwa wakimpa risiti kwa majina yake na kwamba aliendelea kutoa fedha hadi alipokamatwa mwaka 2017.

"Kati ya risiti hizo, nilizo nazo zilisainiwa na Hellen Adam ambaye alikuwa shahidi wa 10 wa upande wa mashtaka na Kaimu Mkurugenzi wa Fedha, Daniel Msangi, ambaye alikuwa shahidi wa sita. Risiti nyingine haikuwa na saini, lakini kwenye taarifa ya benki ilionyesha imeingizwa kama mkopo," alidai.

Pia alidai kuwa risiti zote zinatunzwa na idara ya uhasibu ya TFF na kwamba amekuwa akilipwa kwa mafungu mafungu kutokana na hali ya shirikisho hilo kuwa mbaya kiuchumi.

Aliendelea kudai kuwa idara ya fedha ilikuwa ikikaa na kuangalia namna ya kumlipa kutokana na kile wanachokipata.

"Mheshimiwa hakimu nilikuwa nalipwa madeni yangu pale tu TFF ilipopata fedha za ruzuku kutoka Shirikisho la Mpira wa Miguu Duniani (FIFA) au Shirikisho la Mpira Afrika (CAF) au kutoka kwa wafadhili kama ilivyokuwa kwa Kampuni ya Bia ya Serengeti na Kampuni ya Bia Tanzania (TBL)," alidai Malinzi.

Malinzi alidai mwaka 2015 hali ya TFF ilikuwa haijabadilika kwa hiyo alikuwa akitoa fedha zake mfukoni na kuwaomba wadau mbalimbali kuendelea kuchangia na mwishoni mwa mwaka 2014 alijenga ofisi ya rais na nyaraka alizokuwa anatunza nyumbani alianza kuzitunza ofisini.

# Majeruhi wengine 7 ajali ya lori la mafuta wafariki

**Na Waandishi Wetu**

MAJERUHI wengine saba katika ya 46 waliopokelewa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) baada ya kujeruhiwa katika ajali ya lori la mafuta eneo la Msamvu mkoani Morogoro, wamefariki dunia, hivyo kuifanya idadi ya waliopoteza maisha kutokana na ajali hiyo kufika 89.

Pia idadi ya majeruhi wa ajali hiyo, waliofariki dunia wakipata matibabu MNH sasa imefika 21. Majeruhi hao walifikishwa kwenye hospitali hiyo Jumamosi. Imeelezwa kuwa majeruhi wengine 16 kati ya 25 wanaoendelea kupata matibabu katika hospitali hiyo kubwa zaidi nchini, hali zao ni mbaya.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Huduma kwa Wateja wa MNH, Aminiel Aligaesha, alisema wagonjwa hao 16 wako katika chumba cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum (ICU).

"Kati ya majeruhi 46 waliofikishwa Muhimbili, tunasikitika kuwaeleza kuwa waliofariki dunia hadi leo (jana) alfajiri wamefika 21, waliobaki sasa ni 25, tunaomba tuendelee kuwaombea madaktari ambao wanaendelea kuwapatia matibabu wagonjwa waliobaki," Aligaesha alisema.

Aliongeza kuwa wagonjwa waliosalia wanaendelea kupatiwa matibabu ili kuokoa maisha yao. Aligaesha aliwataja waliopoteza maisha juzi kuwa ni Ramadhani Mdoe (50), mkazi wa Mwembesongo, Shabani Maringanya (40), mkazi wa Ifakara, Shabani Ayoub (34), mkazi wa Morogoro, Khalifa Iddy (26), mkazi wa Msamvu, Omary Omary (26), mkazi wa Morogoro, Omary Abdallah (24), mkazi wa Msamvu na Aloyce Mponzi (36), mkazi wa Kihonda.

Alisema miili yote imehifadhiwa katika chumba cha kuhifadhia maiti cha hospitali hiyo kwa ajili ya maandalizi ya kusafirishwa kwenda mkoani Morogoro kwa maziko.

"Miili yote ipo chumba chetu cha kuhifadhi maiti na leo jioni (jana) itasafirishwa kuelekea mkoani Morogoro kwa ajili ya maziko," Aligaesha alisema.

Ofisa huyo wa MNH alisema miili ya watu sita waliopoteza maisha juzi, ilisafirishwa jana kuelekea Morogoro kwa ajili ya maziko yatakayofanyika kwenye eneo maalum lililotengwa na serikali.

Aligaesha alisema serikali imeandaa utaratibu wa kuisafirisha miili hiyo hadi mkoani Morogoro katika eneo hilo maalum la maziko lililoandaliwa.

Alisema serikali pia inagharamia jeneza na sanda kwa ajili ya miili yote ya watu waliopoteza maisha kutokana na tukio hilo.

"Kwa ndugu ambao wanataka kuchukua miili ya wapendwa wao kwenda kuzika mikoa mingine mbali na eneo ambalo serikali imetenga mkoani Morogoro, watajigharamia usafiri na wataendesha taratibu nyingine wenyewe," Aligaesha alisema.

### CHUPA 400 ZA DAMU

Aligaesha pia alisema idadi ya wananchi waliojitokeza kwa ajili ya kuchangia damu inazidi kuongezeka na kwa siku nne hadi juzi, walikuwa wamekunywa takribani chupa 400.

Aliwataka watu wenye mapenzi mema kuendelea kujitokeza kuchangia damu ili kuokoa maisha ya majeruhi wengi ambao wanahitaji damu kwa wingi.

Ofisa Mhamasishaji Damu wa MNH, John Bigambalaye, alisema kwa siku kiwango cha damu kinachohitajika kwa wagonjwa wao na Mloganzila ni chupa 150. Alisema MNH pekee wanatumia chupa 120 kwa siku za kawaida na inapotokea majanga kama ya ajali ya moto, wanatumia chupa hadi 200 za damu kwa siku.

Alisema kwa siku hizo nne ambazo makundi ya watu mbalimbali yanajitokeza kuchangia damu, wamekusanya hadi chupa 120 tofauti na awali walipokuwa wakikusanya chupa 80 kwa siku.

Bigambalaye alisema majeruhi hao wa moto wanahitaji zaidi maji yanayotoka kwenye damu na chembechembe za damu.

***Imeandikwa na Mary Geofrey na Mariam Magili**



Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kinondoni, Benjamini Sitta, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mradi wa uendelezaji wa fukwe ya Oysterbay 'Coco Beach'. Kulia ni Ofisa Uhusiano wa manispaa hiyo, Sebastian Mhowera. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Mbivu mbichi ushahidi video kesi Mbowe, wenzake Jumatatu

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, imepanga kutoa uamuzi wa kukubali au kukataa ombi la Jamhuri la kuonyesha tukio kwa njia ya runinga Agosti 19, mwaka huu, katika kesi ya uchochezi inayowakabili vigogo tisa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) akiwamo Mwenyekiti wa Taifa, Freeman Mbowe.

Uamuzi huo ulipangwa kutolewa jana lakini mawakili wa utetezi walikuwa na kesi nyingine Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Dar es Salaam.

Hata hivyo, Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba, alisema mahakama yake itatoa uamuzi na itaendelea kusikilizwa Agosti 19.

Awali, upande wa Jamhuri ukiongozwa na Mawakili wa Serikali Wakuu, Faraja Nchimbi, Dk. Zainabu Mango na Wakili wa Serikali Jacqueline Nyantori, ulidai kuwa uko tayari kuendelea lakini mawakili wa utetezi wana kesi nyingine Mahakama Kuu. Hakimu alisema washtakiwa wote wataendelea kuwa nje kwa dhamana na kesi hiyo itaendelea kusikilizwa Jumatatu ijayo.

INAENDELEA UK. 8


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
Tarehe 15/08/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMAMOSI** tarehe **17/08/2019** kampuni ya **SINO-SHINE OVERSEARS CONSTRUCTION & INVESTMENT (EA) LTD** itasafirisha na mizigo yake kutoka **SUMBAWANGA** kuelekea **KAMBANGA** kupitia **MPANDA** Magari yenye namba za usajili:
   **1.T349 BNT/T 646 BCJ.**
   **2.T550 BES/T474BCJ**
   **3.T389 BES/668 BCJ**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   Urefu-mita 20.0
   Upana –mita 3.0
   Kimo – mita 4.8
3. Njia itakayotumika **SUMBAWANGA hadi KAMBANGA kupitia MPANDA gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

115373202

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Elimu ufunguo mafanikio SADC

**TUNAIPONGEZA** Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), kwa jitihada nyingi zinazofanyika kuhakikisha kuwa ukanda huu wa kusini mwa Afrika unaimarika kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Hongera viongozi wa SADC pamoja na Mwenyekiti wake mpya Rais John Magufuli, ambaye wiki hii anaianza na jukumu jipya la kuongoza nchi zetu 16 wanachama.

Tunamwamini Rais Magufuli ni kiongozi ambaye pamoja na nia ya kuiletea Tanzania maendeleo, atapenda pia kuiachia SADC alama zisizofutikana zilizobakizwa na uongozi wake. Kwa hiyo itakuwa SADC bora zaidi chini ya Magufuli.

Tunapenda kuunga mkono juhudi za pamoja kuwa na Bunge la SADC, kufikiria kuwa na mtangamano mkubwa zaidi kiuchumi hasa viwanda, lakini tunaomba kwanza elimu iwe kipaumbele.

Tunashauri jumuiya hii kuanzia sasa iweke mkazo kwenye utoaji wa elimu bora kwa kila raia kwani bila kuwa na raia wasomi, mataifa haya yatachelewa kufikia maendeleo endelevu na viwanda

Mathalani, Tanzania inatumia karibu Sh. bilioni 300 kugharamia elimu bure kila mwezi kwa wanafunzi wote wakiwamo wenye mahitaji maalumu.

Juhudi zimefanywa kuwasaidia watu wa familia maskini kujikimu ili kuwezesha watoto wasome na kupata elimu hasa wakati huu ambao serikali inagharamia elimu.

Pamoja na pongezi hizi kwa Tanzania kuwa mfano tunashauri usimamizi wa karibu ufanyike SADC kwenye sekta ya mapato, ili kupata fedha zaidi kugharamia elimu ili pia kufikia malengo endelevu (SDGs).

Sambamba na mkutano mkuu wa SADC, wadau wa asasi za kiraia (NGOs) wa jumuiya hiyo wanatoa angalizo kuwa ni elimu pekee ndiyo itakayokamilisha ushirikiano wa kweli.

Hivyo kila taifa linahimizwa kuwa na juhudi za kweli za kuwekeza kwenye elimu kwa kuongeza bajeti kwa kukusanya kodi zaidi ili kugharamia elimu.

NGO za SADC zinaona kuwa mataifa kama Msumbiji, Tanzania na Nepal yanapoteza mamilioni ya dola kutokana na misamaha ya kodi isiyo na tija.

Aidha, SADC inatajwa kuwa eneo lenye utoroshaji fedha kiholela nje ya mipaka, kuna ubadhirifu yote hayo yakinyong'onyeza bajeti za nchi na kuumiza elimu ambao ndiyo ufunguo wa maisha.

Ni dhahiri kuwa bila elimu bora watu hawatafahamu faida za mtangamano, kutabakia kuwa na ushirikiano kwenye makaratasi na makabrasha ndani ya ofisi lakini raia hawataufahamu.

Viwanda na ujenzi wa uchumi imara havitatengemaa kama wananchi washirika wakuu hawana elimu ya kutosha.

Hivyo ni wakati wa kushirikiana kwanza kuimarisha elimu ili makundi yote kuanzia wasichana, walemavu na watu maskini wawe na elimu kwa ajili ya maendeleo ya nchi zao.

Nguvu kazi iliyoelimika itatumika kikamilifu kwenye viwanda, kilimo, mifugo, madini, siasa, tiba na kwenye sekta zote za uchumi na kijamii.

Ni vyema kusimamia kikamilifu matumizi ya fedha za miradi ya elimu ili kuwa na SADC iliyoelimika inayoweza kujisimamia na kujitegemea kwa nyanja zote.


Hilo litawezekana tu iwapo kodi na mapato mengine yatasimamiwa kikamilifu kuelimisha raia wetu na kuwapa elimu bora.

Raia wakisoma watafanya maamuzi sahihi kwa wakati, wataepuka magonjwa, watatumia rasilimali kwa uangalifu, wataheshimu haki za binadamu, watawajibika kila mmoja kwa nafasi yake, watatunza miundombinu na mazingira, watashiriki siasa kikamilifu na huo ndiyo mwanzo wa mafanikio SADC inayoyatarajia inapoelekea kwenye mtangamano.

Hongera SADC, kila la heri kwa Mwenyekiti Magufuli. Aluta kantinyua. Mapambao yaendelee kuwa na elimu bora kwenye ukanda huu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Wauza mafuta, daladala msisahau angalizo mlilopewa kwenye sheria

**MOJA** ya mambo yasiyotakiwa, ambayo yanafanywa na baadhi ya madereva wa magari ya abiria ni kujaza mafuta 'sheli' huku yakiwa na abiria bila ya kujali ni kosa na hatari kwa usalama wa abiria.

Hata hivyo, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (Latra), ilishanuia kushughulika na madereva wote wenye tabia hiyo, ili kulinda usalama wa abiria ambao wamekuwa kwenye hatari inayotokana na mtindo huo ewa maisha.

Uamuzi wa Latra unatokana na ukweli kwamba, nchi zote duniani huongozwa na sheria na taratibu ilizojiwekea, lakini wanapotokea baadhi ya watu wanazikiuka, ni muhimu wawajibishwe.

Zipo tahadhari nyingi za kuzingatiwa na madereva wawapo katika vituo vya mafuta; kutokuwa na abiria ndani ya gari, kutovuta sigara, kuzima injini ya gari, na baadhi yao hawazingatii hayo.

Inaelezwa, kuna madhara makubwa yanayoweza kutokea hata kuhatarisha maisha ya abiria iwapo madereva hawataacha mtindo huo wa kwenda vituo vya mafuta wakiwa na abiria.

Kwa mfano, ukitokea mlipuko wa mafuta, abiria watajinusuru vipi? Ni kweli kwamba, ajali haina kinga, lakini ni vyema pia kutambua ajali haitokei tu, bali huwa inasababishwa. Sasa epuka kuwa kisababishi.

Hebu fikiria, jinsi daladala zimekuwa zikijaza abiria kupita kiasi, halafu zinakwenda kwenye vituo vya mafuta wakiwamo halafu ukatokea mlipuko, maana yake ni kwamba ni maafa.

Hivyo madereva na wauza mafuta, wanatakiwa kujiongeza, badala ya kuangalia biashara tu, waangalie pia usalama wao na wateja kwanza, kuliko kuangukia kufaya shughuli zao kienyeji tu.

Suala hili lisisubiri hadi tatizo litokee, bali ni kuzingatia sheria, taratibu na kanuni tulizojiwekea kwa ajili ya usalama wetu wenyewe kuliko kuruhusu watu wafanyabiashara wachache kuweka rehani maisha ya Watanzania.

> **Hivyo madereva na wauza mafuta, wanatakiwa kujiongeza, badala ya kuangalia biashara tu, waangalie pia usalama wao na wateja kwanza, kuliko kuangukia kufaya shughuli zao kienyeji tu.**

Mwaka jana, Wakili Yohanes Konda, alikaririwa na kituo cha East Africa Televisheni akisema, kwa sheria za usalama barabarani, ni makosa gari la abiria kujaza mafuta huku ikiwa na abiria.

Endapo muuzaji akishitakiwa, adhabu yake inaangukia pabaya katika sura ya kifungo na faini.

Pamoja na hayo, bado imekuwa jambo la kawaida madereva wakiwamo wa daladala kujaza mafuta huku wakiwa na abiria, jambo ambalo sasa linapaswa kukemewa kwa nguvu zote.

Hili liende sambamba na kuzuia ujenzi wa vituo vya mafuta kwenye makazi ya watu, hali ambayo nayo inaweza kusababisha maafa kwa wanaoishia jirani na vituo hivyo.

Nakumbuka, mwaka 2009, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Amina Said, alivifungia vituo 18 kati ya 31 vya mafuta wilayani Kibaha, baada ya kubainika vilikiuka taratibu za uendeshaji, ikiwamo kujengwa karibu na makazi ya watu na kukosa vyeti vya usalama wa moto na vifaa vya tahadhari.

Kilichofanywa na mkuu huyo wa mkoa, ni kutambua umuhimu wa vituo vya mafuta vinajengwa mbali na makazi ya watu, kuna uwezekano mkubwa wa kutosababisha madhara makubwa.

Kwa hiyo mjadala huu unajikita zaidi kwa mambo mawili ambayo ni gari la abiria kutokwenda sheli kujaza mafuta likiwa na abiria na pia kutojenga sheli karibu na makazi ya watu.

Mjadala huu unashauri biashara hii izingatie usalama wa watu kwanza, mambo mengine baadaye ili isije kusababisha maafa yasiyo ya lazima.

# Muda kuomba mikopo vyuo vikuu waongezwa

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imetangaza kuongeza muda wa kuomba mkopo kwa njia ya mtandao kwa siku tano hadi Ijumaa, Agosti 23, 2019, ili kuwapa fursa waombaji ambao hawajakamilisha maombi yao kutumia muda ulioongezwa kufanya hivyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru, alitangaza uamuzi huo jijini Dar es salaam jana kuwa HESLB ilianza kupokea maombi ya mkopo kwa mwaka wa masomo 2019/2020 Julai Mosi mwaka huu na tarehe ya mwisho ilipaswa kuwa jana.

Kwa mujibu wa Badru, HESLB imepokea maombi kutoka kwa baadhi ya waombaji mikopo ambao hawajakamilisha maombi yao kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kukosa nyaraka muhimu.

"Ingawa hadi leo (jana) asubuhi, tumeshapokea maombi zaidi ya 74,821 yaliyokamilika kwa njia ya mtandao, tumepokea pia maombi kutoka kwa wateja wetu wakitaka kuongezewa muda ili wakamilishe nyaraka muhimu kama nakala za vyeti vya vifo vya wazazi wao, barua kutoka kwa wadhamini wao na nyaraka nyinginezo ... tumewasikiliza na kuongeza muda," alisema Badru.

Mkurugenzi Mtendaji huyo aliwataka waombaji mkopo ambao hawajakamilisha maombi yao kutumia muda ulioongezwa kukamilisha maombi yao kwa kuwa HESLB haitaongeza muda zaidi baada ya Agosti 23, mwaka huu.

"Tunasihi waombaji wetu watumie muda huu ulioongezwa kukamilisha maombi yao kwa kuwa hatutaongeza tena. Baada ya Agosti 23, tutaanza kufanya uchambuzi wa maombi tuliyopokea ili tuwapangie mikopo wenye sifa kwa wakati na tupeleke fedha za mikopo vyuoni kabla vyuo havijafunguliwa," alisema Badru na kuongeza:

"Tunawaomba wadau wetu kama Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar na Shirika la Posta Tanzania (TPC) kuendelea kuwahudumia wanafunzi katika kipindi hicho."

Katika kipindi kilichoongezwa cha hadi Agosti 23, Badru alisema dawati la huduma kwa wateja la HESLB litakuwa wazi ili kutoa ufafanuzi kwa waombaji mkopo pale utakapohitajika.




Mkuu wa Mkoa wa Morogoro ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maafa Mkoa, Dk. Kebwe Steven Kebwe (kushoto), akipokea hundi yenye thamani ya Sh. milioni 10 kutoka kwa Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Milima Udzungwa, Donatus Bayona, mkoani humo jana, kwa ajili ya kusaidia majeruhi waliopata ajali ya moto baada ya mlipuko wa lori la mafuta, ajali iliyotokea katika eneo la Msamvu. Kulia ni Kaimu Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi Kanda ya Mashariki, Crispin Mwinuka. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

# Sababu walipakodi wakubwa kulimbikiza madeni makubwa

**Na Enock Charles**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imeeleza changamoto za ukusanyaji wa mapato kwa walipakodi wakubwa yakiwamo mashirika ya umma na taasisi za serikali kufanya manunuzi yasiyokuwa na stakabadhi za kielektroniki na kuwa na malimbikizo makubwa ya madeni.

Akizungumza kwa niaba ya Kamishna Mkuu wa mamlaka hiyo, wakati wa semina ya elimu kwa walipakodi wakubwa, kamishna wa walipa kodi wakubwa, Alfred Mregi, alizitaka taasisi za serikali kurekebisha upungufu huo ili zilipe kodi kwa wakati na kwa mujibu wa sheria za kodi nchini.

"Kupitia mkutano huu, ninazikumbusha taasisi mbalimbali za serikali kuepuka malimbikizo ya kodi, na pia taasisi na mashirika yaliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria za kodi yana wajibu wa kuwasilisha ritani za kodi na kulipa kodi iliyokadiriwa kwa muda unaotakiwa kwa mujibu wa sheria," Mregi alisema.

Alisema mamlaka hiyo inalenga kukusanya shilingi trilioni 19.1 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 likiwa ni ongezeko la Sh. trilioni 1.1 ya lengo la mwaka jana 2018/2019 ikiwa ni asilimia 57.6 ya Bajeti ya Serikali ya Sh. trilioni 33.11 ya mwaka 2019/2020.

Akitaja changamoto zingine, kamishna huyo alisema ni pamoja na mapungufu ya tafsiri ya ukokotoaji wa kodi kwenye mishahara, posho, stahiki mbalimbali za watumishi, vibarua na makandarasi katika miradi mbalimbali kutokana na kutokuzingatia matumizi sahihi ya mabadiliko mbalimbali yatokanayo na sheria za fedha za miaka husika, hivyo kupelekea taasisi na mashirika husika kukadiriwa ongezeko la kodi, adhabu na riba.

Changamoto nyingine ni kutowasilishwa kwa ritani za kodi kwa wakati na baadhi kutowasilishwa kabisa na upungufu katika tafsiri na utozaji wa kodi ya zuio husan katika kandarasi, miradi na zabuni mbalimbali.

Pia alikiri kuwapo kwa changamoto ya risiti za kielektroniki kufutika na zingine kutokusomeka na kuahidi kuwa mamlaka hiyo, itarekebisha upungufu huo ili kutokuwa kikwazo kwa walipakodi nchini.

# Ujenzi Coco Beach kugharimu bil. 14/-

**Na Philip Nyiti**

UENDELEZAJI wa ufukwe wa Coco jijini Dar es Salaam utaanza rasmi mwezi ujao ukigharimu Sh. bilioni 14, imeelezwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Meya wa Manispaa ya Kinondoni, Benjamin Sitta, alisema wanatarajia kumtangaza mkandarasi ambaye amechaguliwa kufanya kazi hiyo muda wowote.

Sitta alisema kwa sasa, halmashauri ina michoro sahihi yenye gharama ambayo ipo ndani ya bajeti iliyoombwa kutoka serikali kuu kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

"Tayari nyaraka za zabuni zimekwishatolewa kwa makandarasi walioidhinishwa ambao wanatarajiwa kurudisha nyaraka hizo na kufanya ufunguzi wa wazi Jumatatu ijayo," alisema.

Meya Sitta aliongeza kuwa michoro ya kuendeleza ufukwe huo inaonyesha namna utakavyokuwa baada ya ujenzi kukamilika, huku akieleza kuwa wananchi watautembelea bila gharama yoyote kama alivyoagiza Rais John Magufuli.

Alisema uendelezaji wa ufukwe huo utalifanya jiji hilo kuwa kivutio cha watalii na kuingizia kipato serikali.

Uendelezaji wa ufukwe huo ni sehemu ya mkakati wa serikali kuimarisha sekta ya utalii kwa kuhakikisha mwambao wa pwani ya Bahari ya Hindi unatumika ipasavyo kuvutia watalii na kuongeza mapato kupitia sekta ya utalii inayoshika nafasi ya kwanza kwa kuingiza fedha nyingi za kigeni nchini.

**"Tayari nyaraka za zabuni zimekwishatolewa kwa makandarasi walioidhinishwa ambao wanatarajiwa kurudisha nyaraka hizo na kufanya ufunguzi wa wazi Jumatatu ijayo," alisema.**

# Kiwango tozo maegesho ya magari Dar chatajwa

**Na Mary Geofrey**

HALMASHAURI ya Jiji la Dar es Salaam na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (Tarura) wamekubaliana tozo ya maegesho ya magari katikati ya jiji kuwa Sh. 500 na pembezoni mwa jiji kuwa Sh. 300 kwa saa moja.

Msimamo huo ulitangazwa jana na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Joseph Kakunda, baada ya kufanya kikao cha majadiliano ya pamoja ili kuwa na tozo maalum ya maegesho ya magari katika maeneo hayo.

Kakunda alisema wamefikia mwafaka huo baada ya kufanya kikao cha makubaliano kufuatia jiji kubadili sheria ya kupunguza gharama hizo katika maeneo ambayo Tarura wanatoza 500 kwa saa ilhali jiji lilishafanya marekebisho ya sheria kuwa watumiaji wa barabara za pembezoni mwa jiji watozwe Sh. 300.

"Maegesho yalikuwa hayana gharama maalum kutokana na Tarura kutoza Sh. 500 maeneo yote wakati jiji wao wamegawanyisha tozo ya Sh. 500 kwa maeneo ya katikati ya jiji na pembezoni mwa nje ya jiji wanatoza Sh. 300 kwa saa moja, hivyo serikali imeamua kutangaza gharama maalum," Kakunda alisema.

Aliongeza kuwa lengo la serikali ni kuweka gharama hizo kwa ajili ya kupunguza msongamano wa magari katikati ya jiji hilo, lakini pia kuiwezesha serikali kukusanya mapato.

Kakunda alisema jiji hilo linakusanya Sh. bilioni mbili kila mwezi kupitia tozo za maegesho ya magari na wanatarajia kuongeza mapato hayo pindi watakapoboresha maeneo ya maegesho.

Mkurugenzi wa jiji hilo, Spora Liana, alisema walikutana ili kujadiliana na kukubaliana gharama maalum za tozo ya maegesho ya magari na kuahidi kuwa watayafanyia kazi mapendekezo yote yaliyotolewa kuboresha eneo hilo.



Mawakili wa Tundu Lissu; Peter Kibatala (kulia), Jeremia Mtobisya (katikati) na Fred Peter Kalonga, wakiwa katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam jana, walipofika kutetea kesi ya mteja wao ya kupinga kuvuliwa ubunge na Spika Job Ndugai. **PICHA: MIRAJI MSALA**


**ULTIMATE SECURITY (T) LTD**

ULTIMATE

**INVITATION FOR BIDS**
**SALE OF ASSETS**
**TENDER No: US/FY19/01**

**Bids are invited from interested parties for the purchase of assets as listed below:**

| Snr: | Reg. No: | Make | Model | YOM | Location |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | T 939 ACX | NISSAN | PATROL | 1998 | INCAR yard, Pugu area DSM |
| 2 | T 627 CLB | FORCE | TRAX | 2009 | INCAR yard, Pugu area DSM |
| 3 | T 345 AXA | FORCE | TRAX | 2007 | INCAR yard, Pugu area DSM |
| 4 | T 588 ART | TOYOTA | HILUX D/CABIN | 2008 | INCAR yard, Pugu area DSM |
| 5 | T 633 CLB | FORCE | TRAX | 2009 | INCAR yard, Pugu area DSM |
| 6 | T 215 ADA | TOYOTA | HIACE VAN | 1996 | INCAR yard, Pugu area DSM |
| 7 | T 340 AXA | FORCE | TEMPO | 2007 | INCAR yard, Pugu area DSM |
| 8 | T 331 AXA | FORCE | TEMPO | 2007 | INCAR yard, Pugu area DSM |
| 9 | T 325 AQW | MERCEDES | BENZ AMBULANCE | 1996 | INCAR yard, Pugu area DSM |
| 10 | T 314 AEC | MERCEDES | BENZ FIRE ENGINE | 1990 | INCAR yard, Pugu area DSM |
| 11 | T 414 ACQ | DENNIS 2 | AXLE FIRE ENGINE | 1989 | INCAR yard, Pugu area DSM |

**Condition of Sale:**

1. Vehicle are sold on **"AS IS WHERE IS"** basis Ultimate Security shall note have further liability after sale
2. Viewing to verify details can be done during normal working hours (8.00am -4.00pm) at the location indicated.
3. Successfull bidder will be required to pay the full bid price within 2 working days from the date of the award
4. Successfull bidders will be required to remove purchased vehicle from site within 7 days from the date of award
4. Buyers will be required to un brand / repaint the vehicle within 7 days from the date the vehicles are handed over to them.
5. Ultimate Security reserves all rights and without assigning any reasons there of not to accept the highest bid.
6. Bids can be placed in a sealed envelope marked **" TENDER FOR MOTOR VEHICLE"** and deposited at Ultimate

Security Office Addressed to:

**GENERAL MANAGER**
**ULTIMATE SECURITY ( T ) LTD**
**WARIOBA STREET**
**P.O.BOX 21231 DAR ES SALAAM**
**Bids to reach us on or before Friday 30 August 2019.**

215377202


## JPM, Ramaphosa waahidi neema

**INATOKA UK. 2**

tumenunua Afrika Kusini," Rais Magufuli alisema.

Kwa upande wake, Rais Ramaphosa alimshukuru Rais Magufuli kwa kumwalika kufanya ziara hiyo na akamhakikishia kuwa wananchi Afrika Kusini wanaiona Tanzania ni nyumbani kwao na hivyo serikali yake iko tayari kuuendeleza na kuukuza uhusiano mzuri kati yake na Tanzania.

Rais Ramaphosa pia alieleza kufurahishwa kwake na kuwapo kwa kampuni 228 za Afrika Kusini zilizowekeza nchini na kuajiri wa zaidi ya watu 21,000 na ameahidi kwenda kuwahimiza zaidi wafanyabiashara na wawekezaji wa Afrika Kusini kuja kuwekeza nchini huku akiwakaribisha pia wawekezaji wa Tanzania kwenda kuwekeza Afrika Kusini.

Alipongeza Tanzania kwa kuzalisha mazao mengi ya chakula na akaahidi kuwa Afrika Kusini itaendelea kununua mazao kutoka Tanzania.

Rais Ramaphosa alisema Afrika Kusini iko tayari kushirikiana na Tanzania katika nyanja nyingine mbalimbali zikiwamo afya, ulinzi na usalama, utalii na amekubaliana na mapendekezo ya Tanzania juu ya mpango wa kufundisha lugha ya Kiswahili Afrika Kusini hasa wakati huu ambao SADC inatarajia kuifanya kuwa lugha rasmi ya nne ya mawasiliano kwenye shughuli zake. Rais Ramaphosa ameongozana na mkewe, Dk. Tshepo Motsepe, ambaye wakati wa mazungumzo yao rasmi jana, alikuwa na mazungumzo na Mke wa Rais Magufuli, Mama Janeth Magufuli.

## Mbivu mbichi ushahidi wa video kesi Mbowe, wenzake Jumatatu

**INATOKA UK.5**

Mapema mahakamani hapo, shahidi wa sita Koplo Charles wa Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, alidai kuwa alikimbilia kwenye gari la jeshi hilo kunusuru kamera yake ya video.

Aidha, alidai mihemko hiyo ilisababishwa na hamasa aliyoitoa Mwenyekiti wa Chadema, Mbowe, kutoa kauli ya kuwapandikiza chuki wafuasi hao dhidi ya serikali.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Paul Kadushi, shahidi alidai kuwa Februari 16, mwaka jana, alipangiwa kazi kama mwandishi wa habari katika mkutano wa kufunga kampeni wa Chadema katika viwanja vya Buibui, Kinondoni jijini Dar es Salaam.

Alidai kuwa alijiandaa na vitendea kazi vyake ikiwamo kamera ya kupiga picha za video na ilipofika saa 10:00 alasiri, alikuwa katika viwanja hivyo kwa ajili ya kuanza kazi.

"Nilipofika watu walianza kukusanyika na mshereheshaji alitangaza kwamba viongozi wakuu wa chama wameshafika. Baada ya muda wabunge na viongozi wakuu walipanda jukwaani, nilimsikia Mbowe akitoa kauli za kufanya hamasa ya kuichukia serikali," alidai na kuongeza kuwa:

"Wanachama walipata hamasa na mihemko iliyosababisha wapate jazba ya kuichukia serikali na vyombo vya ulinzi na usalama. Wananchi waliokuwa wamekaa walinyanyuka na kuhamasika, mimi na waandishi wenzangu tulitawanyika pale tuposimama karibu na jukwaa, nilikimbilia kwenye gari la polisi kunusuru kamera," alidai Koplo Charles.

Jopo la utetezi liliongozwa na Wakili Profesa Abdallah Safari, Peter Kibatala, John Mallya na Hekima Mwasipu.

Mbali na Mbowe, washtakiwa wengine ni Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche; Bunda Mjini, Ester Bulaya; Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko; Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Vincent Mashinji; Mbunge wa Iringa Mjini; Peter Msigwa; Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu; Mbunge wa Kibamba, John Mnyika na Mbunge wa Kawe, Halima Mdee.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanadaiwa kuwa kati ya Februari Mosi na Februari 16, mwaka jana, Mbowe na wenzake wakiwa Kinondoni, kwa pamoja walikula njama na wengine ambao hawakuwapo mahakamani, kutenda kosa la jinai ikiwamo kuendelea na mkusanyiko isivyo halali na kusababisha chuki na uchochezi wa uasi.

Ilidaiwa kuwa Februari 16, mwaka jana, Bulaya alishawishi kutenda kosa la jinai katika viwanja vya Buibui kutenda kosa la jinai kwa kufanya maandamano yenye vurugu.

Ilidaiwa Februari 16, katika barabara ya Kawawa eneo la Mkwajuni, Kinondoni, kwa pamoja washtakiwa na wenzao zaidi ya 12 walifanya mkusanyiko na kukaidi amri halali ya ofisa wa Jeshi la Polisi, Gerald Ngiichi, na kusababisha kifo cha Akwilina Akwiline na askari polisi wawili, Konstebo Fikiri na Koplo Rahim Msangi kujeruhiwa.

Ilidaiwa siku ya tukio la kwanza na la pili, katika viwanja vya Buibui kwenye mkutano wa hadhara, Heche alitoa lugha ya kuchochea chuki alitamka kwamba: "Kesho patachimbika, upumbavu ambao unafanywa kwenye nchi hii, wizi unaofanywa na serikali ya awamu ya tano, watu wanapotea, watu wanauawa wanaokotwa kwenye mitaro lazima ukome."

Washtakiwa wote walipsomewa mashtaka yao kwa nyakati tofauti walikana.

HABARI KITAIFA

# Mume, mke walivyonusurika kufa katika mlipuko wa petroli

**Na Said Hamdani,** LINDI

WATU wawili ambao ni mume na mke, wakazi wa Mkoa wa Lindi, wamenusurika kufa baada ya nyumba yao kuteketea kwa moto uliotokana na mafuta ya petroli.

Watu hao ni Shafii Selemani na Liuza Shafii, wakazi wa Kijiji cha Kilimanjaro, Kata ya Mtumbya katika Wilaya ya Lindi. Habari kutoka kijijini hapo zinaeleza kuwa tukio hilo lilitokea Jumanne saa 4:0 usiku.

Baadhi ya majirani waliojitokeza kusaidia kuzima moto huo bila mafanikio, walieleza kuwa moto huo ulichangiwa na petroli iliyokuwa imehifadhiwa kwenye madumu na kuwekwa ndani ya nyumba yao. Walieleza kuwa Shafii licha ya kujihusisha na uendeshaji wa bodaboda, pia alikuwa anajihusisha na uuzaji wa petroli kwa madereva wenzake.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hicho, Hamisi Mashaka, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa chanzo ni madumu ya petroli yaliyokuwa yamehifadhiwa ndani kulipuka.

"Moja ya dumu la uzito wa lita tano likiwa na petroli lilikuwa wazi bila kufungwa kizibo, hivyo harufu yake ilizagaa ndani ikizingatiwa kulikuwa na moto na kulipuka," alisema Mashaka.

Pia, Mashaka alisema moto huo uliteketeza mali zote zilizokuwamo ndani, vikiwamo vitanda, magodoro, chakula, pikipiki, nguo na vifaa vingine.

Shafii Selemani alisema amepata hasara hiyo, na kuwa alichofanikiwa kuokoa kutoka ndani ya nyumba yake zaidi ya bukta na kanga ya mkewe. Aliongeza kuwa pikipiki na kuku zaidi ya 50 waliokuwa kwenye zizi waliteketea.

Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, akizungumzia tukio hilo, aliendelea kuwasisitiza wananchi wanaojihusisha na uuzaji wa mafuta kuweka mbali na eneo la moto ili kuepuka matukio kama hayo.



Wananchi wakiangalia basi la abiria la Mvula Express lililokuwa likisafiri kutoka Dar es Salaam kwenda Kahama mkoani Shinyanga baada ya kupata ajali katika eneo la Malendi wilayani Iramba mkoani Singida juzi. Zaidi ya abiria 50 waliokuwamo kwenye basi hilo wamenusurika. **PICHA: MARC NKWAME**

# Pamba iliyonaswa ikisafirishwa kwa magendo sasa yataifishwa

**Na Happy Severine,** BARRIADI

SIKU chache baada ya kukamatwa kwa lori aina ya Scania namba za usajili T-917 BCN likiwa limebeba tani zaidi ya 20 za pamba inayodaiwa kuwa ni ya magendo, Serikali imeamua kuitaifisha pamba hiyo. Lori hilo ambalo lilikamatwa Agosti 12, mwaka huu majira ya usiku katika Kijiji cha Dutwa wilayani Bariadi, lilikutwa likisafirisha pamba hiyo bila kibali, huku ikiwa haijulikani wapi inapelekwa na wapi imenunuliwa.

Mkuu wa wilaya hiyo, Festo Kiswaga, alisema uchunguzi umeonyesha pamba hiyo ilinunuliwa kwa njia isiyo halali ya Sh.700 hadi 900 kwa kilo kutoka moja kwa moja kwa wakulima.

Alisema wakati serikali ikipambana na watu wanaonunua pamba kwa magendo, bado wapo wafanyabiashara wa zao hilo wanaendelea kupiga vita juhudi hizo kwa kuendeleza biashara hiyo na kuwanyonya wakulima.

" Baada ya wahusika kushindwa kujitokeza, sasa kama Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, nachukua uamuzi wa kuitaifisha pamba hii na tunaenda kuiuza kwenye viwanda vya kuchambua pamba. Leo hii (jana) na fedha zote zitapelekwa kununua vifaa vya kukamilisha ujenzi wa bweni katika shule ya sekondari Simiyu," alisema Kiswaga.

Aliongeza kuwa pamba hiyo ina thamani ya zaidi ya Sh. milioni 10, na baada ya kuuzwa uchunguzi utaendelea kujua nani mhusika mkuu, huku akieleza kuwa gari litaendelea kushikiliwa na Jeshi la Polisi mpaka mhusika atakapojitokeza.

# Mwalimu mkuu kortini madai kumpa ujauzito mwanafunzi

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MWALIMU Mkuu wa Shule ya Msingi Nyantole, Jason Rwekaza (42), mkazi wa Bigabilo wilayani Kigoma, amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Kigoma kwa makosa saba ya kubaka na kumpa ujauzito mwanafunzi mwenye umri wa miaka 17 wa darasa la saba.

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani jana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa mahakama hiyo, Flora Mtarania na alisomewa mashtaka yake alikana kuhusika na makosa hayo na yuko nje kwa dhamana ya wadhamini wawili wenye barua za utambulisho kutoka kwa Ofisa Mtendaji wa Kata na mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni moja.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na wakili wa serikali, Antia Julius, ulidai mahakamani kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa huyo maelezo ya awali.

Hakimu Mtarania alikubali ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Agosti 19, mwaka huu kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa huyo maelezo ya awali.

Vile vile, katika kesi hiyo mshtakiwa anatetewa na wakili wa kujitegemea, Thomas Msasa, ambaye alisema mteja wake anatuhuma za kubaka na kumpa ujauzito mwanafunzi, kazi yake ni kuhakikisha mteja wake anapata dhamana na ana imani kuwa mahakama hiyo itatenda haki.

Akisoma hati ya mashtaka Wakili wa Serikali, Antia Julius, alidai mahakamani kuwa mshtakiwa alimbaka mwanafunzi huyo kwa nyakati tofauti na tarehe tofauti kati ya mwezi Mei, mwaka 2017 (Mlole), Juni 7, 2017, (Mwandiga), Agosti 16, 2017, (Mwandiga), Machi 22, 2018 (Bigabilo), Julai 10, 2018 (Bigabilo), Febuari 5, 2019 (Kahabwa) Manispaa ya Kigoma/Ujiji, mshtakiwa anadaiwa kumbaka mwanafunzi huyo.

Julius aliendelea kueleza mahakamani kuwa Febuari 5, 2019 maeneo ya Kahabwa katika Manispaa ya Kigoma/Ujiji, mshtakiwa alimpa ujauzito mwanafunzi mwenye umri wa miaka 17 wa darasa la saba kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.

# Wanawake 7,648 wakeketwa Singida

**Na Dotto Mwaibale,** SINGIDA

JUMLA ya wanawake na watoto 7,648 katika Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi mkoani Singida, wamekeketwa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2016 na 2018.

Hayo yalielezwa hivi karibuni na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika lisilokuwa la kiserikali la Save the Mother and Children of Central Tanzania (SMCCT), Evalyene Lyimo, katika uzinduzi wa mradi wa utetezi dhidi ya mila potofu ya ukeketaji na udhalilishaji uliofanyika hivi karibuni wilayani Ikungi mkoani hapa.

"Kuanzia Januari hadi Oktoba 2018 jumla ya wanafunzi 37 wa Shule ya sekondari wilayani humo, walibainika kuwa na mimba, huku wanawake na watoto 7,648 wakiwa wamekeketwa katika kipindi cha mwaka 2016 hadi 2018," alisema Lyimo.

Akizungumzia mradi huo Lyimo alisema ulianza mwaka 2017 hadi mwaka jana na kuwa katika kipindi hicho umetoa elimu juu ya madhara kuhusiana na mila potofu na udhalilishaji wa kijinsia kwa wakazi wapatao 15,000.

Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Edward Mpogolo, aliwataka viongozi wa madhehebu ya dini na ngariba wastaafu kushiriki kikamilifu vita dhidi ya vitendo hivyo.

Alisema utekelezaji wa masuala ya mila kwa mambo ya maendeleo ni jambo jema, lakini inakuwa kinyume kama masuala hayo ya ukeketaji inakuwa ni changamoto kubwa kwa jamii na kinyume cha haki za binadamu.

"Tuna taarifa kuwa ukeketaji wa sasa wanafanyiwa watoto wadogo na wachanga ambao hawawezi kukataa au kujihami na vitendo hivyo... serikali haitaweza kuvumilia kuona vikiendelea, na mtu yeyote atakayebainika anavifanya atachukuliwa hatua kali," alisema Mpogolo.



Wachuuzi wa maparachichi wakiwa wamejipumzisha katika bustani iliyopo katika eneo la Palm Beach, jijini Dar es Salaam jana, kabla ya kuingia mitaani kusaka wateja. **PICHA: JOHN BADI**

# Askofu ataka JPM aungwe mkono

**Na Dotto Mwaibale,** SINGIDA

ASKOFU mstaafu wa Kanisa la Pentekoste (FPCT) la Singida Kati, Dk. Paul Samwel, amewahimiza Watanzania kuunga jitihada zinazofanywa na Rais Dk. John Magufuli za kuiletea nchi maendeleo.

Aliyasema hayo hivi karibuni katika hafla ya makabidhiano ya kituo cha kupima uoni na usikivu kwa wanafunzi wa shule za sekondari na msingi zilizopo mkoani hapa, kituo hicho kimewekwa Shule ya Msingi Mahembe, kikisimamiwa na kanisa hilo chini ya mradi wa elimu jumuishi.

Askofu Samuel alisema ana uhakika kuwa kila Mtanzania mwenye mapenzi mema na uzalendo ni lazima ataziunga mkono jitihada za Rais Magufuli za kutuletea maendeleo nchini.

"Rais Magufuli alipoingia madarakani alianza kwa kusema Tanzania sio nchi maskini, lakini baadhi yetu hatukumwelewa baada ya muda mfupi tuliona miradi mikubwa ya maendeleo ikianza kufanyika ikiwa ni pamoja na kununuliwa kwa ndege kubwa za kisasa tena kwa fedha taslimu," alisema Dk. Samwel.

Alisema pamoja na miradi hiyo kuendelea kujengwa hawajawahi kusikia malalamiko ya makandarasi kukosa pesa za malipo baada ya kukamilika kwa miradi hiyo na kuwa sasa hivi ile tabia ya nchi kuwa ombaomba imebaki kuwa historia.

Mgeni rasmi wa hafla hiyo, Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida, Omari Kissuda, alilishukuru kanisa hilo kwa msaada huo na kueleza utasaidia ufaulu kwa wanafunzi hao.

Ofisa Tawala wa mradi huo, Karistoni Mwenda, alisema ukarabati wa kituo hicho kuanzia chumba cha upimaji na vifaa vyake na ujenzi wa ngazi mterezo, umegharimu Sh. milioni 7.6 na aliiomba Manispaa ya Singida kusaidia kuweka kiyoyozi kwenye chumba cha upimaji.

Mwenda alisema mradi huo umefadhiliwa na Shirika la Misaada la Denmark (DANIDA), kupitia Shirika la Misaada la Danish Mission Council Development (DMCDD) likishirikiana na International Aid Service (IAS).

# Skimu 100 zanufaika mafunzo umwagiliaji

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAKULIMA zaidi ya skimu 100 za umwagiliaji nchini wamenufaika na mafunzo ya kukuza na kuboresha kilimo cha umwagiliaji katika kuongeza uzalishaji zaidi.

Akizungumza wakati wa mkutano wa tano wa kamati ya pamoja ya uratibu wa mradi wa kujenga uwezo kwa wakulima wadogo awamu ya pili (Tancaid II), Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, Marco Ndonde, alisema wakulima walionufaika na mafunzo hayo wanatoka kwenye kanda zote nane za umwagiliaji nchini na kuongeza kuwa mafunzo hayo yameleta matokeo makubwa katika sekta hiyo.

"Baada ya mafunzo hayo wakulima katika skimu mbalimbali nchini sasa wana uwezo wa kuibua miradi inayowaletea faida na kuitekeleza kwa ufanisi na hivyo kuongeza uzalishaji wa mazao yao," alisema Ndonde.

Kadhalika, alisema mradi wa Tancaid II, uliofadhiliwa na Shirika la Maendeleo ya Japan (JICA), tangu mwaka 2015 umejikita katika kujenga uwezo wa wakulima wadogo ambao ulitekelezwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (NIRC), ukiwa na lengo la kukuza na kuboresha sekta ya umwagiliaji nchini.

Mkurugenzi Msaidizi wa Tancaid II, Anthony Nyarubamba, alisema chini ya mradi huo NIRC imetumia wataalamu wake kuandaa miongozo ya umwagiliaji (CGL) ambayo imeanza kutumika na wakulima katika maeneo mbalimbali katika skimu za umwagiliaji.

Alisema wakulima sasa wanaweza kusimamia skimu zao za umwagiliaji katika ngazi mbalimbali kuanzia uibuaji wa miradi hadi usimamizi wa miundombinu inayojengwa na serikali badala ya kuiacha iharibike kama ilivyokuwa awali.

Alisema moja ya mafanikio makubwa ya mradi wa Tancaid II ni kuwajengea uwezo maofisa kilimo, wahandisi wa umwagiliaji wa wilaya, kanda na wakulima kwa ujumla katika maeneo ya uibuaji, utekelezaji, uendeshaji na matunzo ya miradi husika.

Akizungumza awali, Mhandisi Amy Mchelle alisema kutokana na kupata mafunzo ya wakulima sasa wanaweza kulipa asilimia tano ya mapato wanayopata baada ya uzalishaji.

"Miongozo imesaidia uboreshaji na utunzaji wa miundombinu ya umwagiliaji na kuwasaidia wakulima kupanga vizuri, kutekeleza, kufuatilia na kutathmini miradi wanayoianzisha," alisema.

Naye Mshauri wa JICA nchini. Namiko Yamada, alisema kwa zaidi ya miaka 40 Serikali ya Japan imetoa misaada kusaidia maendelea ya kilimo cha umwagiliaji.

Yamada alisema JICA chini ya mradi wa Tancaid II imesaidia ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji na kutoa mafunzo kwa vyama vya wamwagiliaji na wahandisi wa umwagiliaji.

Alisema JICA kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, pia imesaidia uendelezaji wa kilimo cha mpunga chini ya mradi wa TANRUCE2.



Mkurugenzi wa Shirika la WaterAid Tanzania, Abel Dugange, akizungumza kwenye uzinduzi wa mradi wa maji wa thamani ya Sh. milioni 229 wa Kijiji cha Sangara, Kata ya Riroda, wilayani Babati mkoani Manyara. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wananchi waambiwa wanywe chai kujitibu

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MTAALAMU wa masuala ya lishe amewashauri wakulima kuzalisha chai kwa wingi kwa vile ina faida lukuki ikiwamo kutibu magonjwa mbalimbali.

Aidha, chai inatajwa kuwa inasaidia kuimarisha viungo vya mwili na pia ni dawa inayomwepusha mtumiaji na maradhi, hivyo kuepuka gharama za matibabu.

Ushauri huo ulitolewa jana na mtaalamu wa lishe wa Shirika la Taha, Rozalia Aloyce, alipozungumza na Nipashe juu ya faida za chai.

"Chai inasaidia kuimarisha mifupa na kupambana na magonjwa ya sukari na magonjwa mengine mengi," alisema Aloyce. Alieleza kuwa zao hilo si geni nchini na kuongeza kuwa mbegu zake zimeanza kuingia kutoka Kenya na kwamba linafaa kwa biashara, hivyo wakulima waanze kulichangamkia. Alisema mtu akitumia chai kama alikuwa ameanza kuchoka na kuzeeka usoni, inamsaidia kubadilisha mwili wake na kuonekana kijana japo umri ni mkubwa.

Baadhi ya wakazi wa Babati, akiwamo Keneth Daud alisema ni mara ya kwanza kulisikia kama lina faida za kutibu maradhi, hivyo aliishauri serikali kulihamasisha lilimwe na matumizi yake yahamasishwe, ili watu waweze kupata tiba na kuepuka kemikali za dawa za kisasa.

Kwa upande wake Kemilembe Novath, mkazi wa Kagera anayeishi Babati kimatembezi alisema, zao hilo linalimwa sana Wilaya ya Karagwe, hivyo wenye uhitaji wanaweza kupata mbegu huko bila shida.

Alisema wakulima wengi mkoani Kagera wanalichangamkia kulilima, ila changamoto iliyopo ni ya wanunuzi ambao ni wachache. Chai inaelezwa kuwa inatibu ugonjwa wa sukari, hivyo ni vyema wataalamu wa kilimo wakalipa kipaumbele na wataalamu wa afya waendelee kulifanyia utafiti kama linatibu sukari na kung'arisha miili ya watu.

# Wadau wa lishe washiriki kukabiliana na udumavu

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

WADAU wa masuala ya kuboresha lishe wakiwamo wazalishaji na wasindikaji wanaoongeza thamani bidhaa za chakula, wametakiwa kutokomeza udumavu kwa kuwa unawaumiza zaidi watoto wengi huko vijijini.

Mratibu wa Asasi ya Infoy inayoshughulika na masuala ya chakula, Laurent Sabuni, alisema hayo jana katika maonyesho ya bidhaa za lishe, yaliyoandaliwa na shirika hilo kwa kushirikiana na shirika la kuhudumia viwanda vidogo (Sido) mkoa wa Arusha.

Alisema wazalishaji na wasindikaji wa bidhaa za lishe, wanapaswa kushiriki kutatua matatizo ya lishe duni katika jamii na kuhakikisha kuwa wanazifikisha bidhaa hizo vijijini. Sabuni alisema kuwa wamekuwa wakitoa mafunzo kwa wasindikaji wa bidhaa za lishe juu ya namna bora ya kusindika na kuzifungasha, ili ziweze kuwafikia wateja na kusaidia kupunguza tatizo la udumavu, linalowakabili watoto wengi nchini.

Meneja wa Sido Mkoa wa Arusha, Nina Nchimbi, alitaka wasindikaji na watengeneza unga wenye virutubisho na viini lishe, ili kukidhi afya ya mlaji na kuhakikisha suala la viwango vya ubora katika bidhaa za lishe wanazozalisha unazingatiwa.

Nina alisema kuwa Sido imefanya juhudi za kuwaunganisha wajasiriamali hao na taasisi za kudhibiti ubora ikiwamo TBS ili bidhaa zao zithibitishwe ubora na kupata masoko ya kitaifa na kimataifa.

Kwa upande wao wasindikaji na wajasiriamali wa bidhaa za lishe, Dorice Assenga na Walter David walisema wamekuwa wakitoa elimu kuhusu umuhimu wa matumizi ya unga wa lishe kwa watoto wadogo na kuzipeleka bidhaa hizo maeneo ya pembezeni, ambako kuna hitaji kubwa la lishe, ili kuwasaidia kinamama wajawazito na watoto chini ya miaka mitano.

Mtaalamu wa Lishe, Prisca Mwakalasi, alisema kuwa mchango wa wadau wa lishe ni mkubwa, kwani madhara ya udumavu huonekana hasa mtoto anapokuwa na kuwa mtu mzima na inakuwa vigumu kufanya maamuzi sahihi.

Alieleza kuwa ni kwa sababu anakua amedumaa hadi akili, hivyo masuala ya lishe kwa watoto na watu wazima yanapaswa yapewe kipaumbele kwani lishe ni kiini cha maendeleo.

# Wafanyakazi watinga kwa DC kuhoji hatima

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAFANYAKAZI zaidi ya 300 wa kampuni ya ulinzi tawi la Arusha, wametinga Ofisi za Mkuu wa Wilaya ya Arusha Gabriel Daqarro, kutoa malalamiko na kuhoji hatima ya mafao yao.

Watumishi hao kutoka kampuni ya Ultimate Security wanalalamikia kuuzwa kinyemela kwa kampuni hiyo, bila wao kushirikishwa na hawafahamu hatima ya stahiki zao.

Wakiongea na vyombo vya habari baada ya kupeleka malalamiko yao kwa mkuu huyo, kwa niaba ya wenzao, Abedy Ally, Baraka Makala na Alex Mollel, wamelalamikia kampuni hiyo kuuzwa bila kuelezwa mustakabali wa stahiki zao licha ya kufanyakazi kwa muda mrefu.

Walisema kuwa kampuni ya Ultimate imeuzwa kwa kampuni mpya Gardaworld, jambo ambalo wanahofu kupoteza stahiki zao baada ya mabadiliko hayo, huku wakimtaka mmiliki mpya wa kampuni ya Gardaworld kujitokeza ili kuwahakikishia stahiki zao.

"Sisi tutapataje haki zetu na tumefanya kazi miaka mingi, katika kampuni hii, tunaomba Mkuu wa Wilaya utusaidie katika hili, maana hata hatujashirikishwa katika maamuzi haya," alisema Alex Mollel.

Akiongelea suala hilo Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro, alisema mabadiliko ya umiliki wa kampuni ya Ultimate kwenda kwa kampuni ya Gardaworld yapo kisheria, isipokuwa aliutaka uongozi wa Ultimate kukaa na wafanyakazi hao na kuwaelimisha mabadiliko hayo.

"Msihofu ondoeni hofu wala hawajauza kinyemela kila kitu katika mauzo haya kati ya kampuni hizi yapo kisheria ila nawaomba nyie uongozi wa Ultimate kaeni na wafanyakazi wenu waelezeni mabadaliko haya ili kuondoa sintofahamu inayojitokeza kwao," alisema.

Kwa upande wake, Eliuta Mjawike, ambaye ni Meneja Mkuu wa Kampuni ya Ulinzi ya Ultimate Tanzania, aliwahakikishia wafanyakazi hao kuwa hawatapoteza haki zao baada ya kutokea mabadiliko ya umiliki wa kampuni hiyo.

Alisema hakuna haja ya kupata hofu sababu wafanyakazi hawajauzwa kama wanavyodai, ila mabadiliko hayo yametokana na kampuni ya Ultimate kuuzwa hisa zake asilimia 100 kwa kampuni hiyo ya Gardaworld ya nchini Canada na hivyo wafanyakazi hawataathirika popote na mabadiliko hayo.

"Mfanyakazi yeyote wa Ultimate hatapoteza stahiki zake kwa haya mabadiliko yaliyofanyika kutoka kampuni ya ultimate kwenda kuwa Gardaworld kwa sababu mikataba yao ipo kisheria na wasiwe na hofu," alisema Mjawike

Meneja wa Ultimate Kanda ya Arusha na Moshi, Abdallah Ally, alisema kuwa kampuni hiyo ina jumla ya wafanyakazi 325 katika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro na changamoto iliyojitokeza ya wafanyakazi kwenda ofisi za Mkuu wa Wilaya, ni kutokana na baadhi yao kutopata elimu juu ya mabadiliko yaliyojitokeza.

Kampuni ya Gardaworld yenye makao yake nchini Canada inaelezwa pia kuwa imenunua kampuni nyingine mbili za ulinzi na kwamba zitaunganishwa kabla ya kuanza majukumu.

# CCM yakemea udini, ukabila

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAKATI ikiwa imebaki miezi miwili kabla ya kufanyika kwa uchaguzi wa serikali za mitaa Oktoba, mwaka huu, Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kilimanjaro, kimewataka wakazi wa mkoa huo kutowaunga mkono wanasiasa wanaoshabikia ubaguzi wa kidini na ukabila kwa kuwa haviitakii mema Tanzania.

Katibu wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro, Jonathan Mabihya, akizungumza jana na Nipashe kuhusu maandalizi ya chama hicho kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa, alisema wako baadhi ya wanasiasa wameanza kutengeneza hoja za kibaguzi ili kutaka kuleta chuki baina ya wananchi na viongozi wa serikali.

"Hatutakubali na kama chama tawala, tumeanza kutoa elimu kila mahali tunapokutana na wananchi kuwapuuza wanasiasa wa aina hiyo. Tutalikemea hili zaidi wakati wa uchaguzi wa serikali za mitaa," alisema Mabihya.

Amewataka wananchi wa mkoa wa Kilimanjaro wanapomwona mtu anayeshabikia suala la ubaguzi, wanapaswa kumwangalia kwa umakini sana kwa vile atakuwa haitakii mema nchi yake.

Alisema serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Rais John Magufuli, itaendelea kuwatumikia wananchi wote bila kujali mwaka 2015 walikipigia kura Chama Cha Mapinduzi au la.

Kama ilivyo kwa uchaguzi mkuu, uchaguzi wa serikali za mitaa nao hufanyika kila baada ya miaka mitano kupita, mara ya mwisho ulifanyika Desemba, 2014.

"Mheshimiwa Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, aliwahi kusema: "Watanzania wakichagua viongozi wazuri watamaliza kero na changamoto walizo nazo wananchi kwa haraka lakini wakichagua wazito, watazama tu chini, kunyanyuka hawanyanyuki, kutembea hawatembei. Jiongezeni wananchi wa Kilimanjaro," alishauri Mabihya.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), uchaguzi wa serikali za mitaa kwa mwaka huu utatumia Sh. bilioni 82.9.

# Agizo la Jafo lapokewa kwa mitazamo tofauti

**Na Mwandishi Wetu,** SAME

WATU wa kada mbalimbali wilayani hapa wamelipokea kwa hisia tofauti agizo la Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, kutaka wakurugenzi wajieleze.

Juzi, Jafo aliwataka wakurugenzi wa halmashauri za wilaya ambazo zimefanya vibaya kwenye utoaji wa fedha za miradi ya maendeleo, kujitathmini na kuandika barua ya kujieleza ndani ya siku 14.

Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro ni miongoni mwa halmashauri zilizotajwa na Jafo kwamba ziko kikaangoni kutokana na kufanya vibaya katika utoaji wa fedha hizo.

Mwanasiasa na mkazi wa Hedaru, Wilaya ya Same, Christopher Mbajo, alisema kwa halmashauri hiyo kuingia katika kundi hilo, ni tatizo ambalo linatokana na ama mfumo wa siasa kutishiwa na itikadi za kisiasa au uongozi kushindwa kusimamia makusanyo ya fedha na mgawanyo wake.

"Kama kweli tunataka kuendeleza jitihada za kupambana na umaskini hasa katika maeneo ya vijijini na kuongeza fursa za ajira ili kuharakisha maendeleo, serikali inapaswa kuchunguza kwa makini ni kipi kisababishi chake hadi halmashauri yetu kushindwa kutoa fedha za miradi ya maendeleo. Isiishie kwa ma DED (Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya) tu kuandika barua za kujieleza," alisema Mbajo.

Halmashauri ya Wilaya ya Same iliyoanzishwa rasmi kwa Sheria ya Bunge, Sura ya 287 (Mamlaka za Wilaya) ya Sheria za Tanzania na kuanza kutekeleza majukumu yake Januari Mosi, 1984, imetajwa kuchangia asilimia nne.

Mchungaji wa Usharika wa Makasa wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Pare, Elisa Mrutu, alisema tatizo si wakurugenzi bali ni mfumo mpya wa ukusanyaji wa mapato yanayopatikana na upelekaji wa pesa hizo zinazokusanywa katika mfuko mkuu wa serikali.

"Nasema hivyo kwa sababu kuna kitu kinaitwa OC (fedha za matumizi mengineyo) ambazo haziji kwa wakati katika halmashauri na zikija zinakuja chini ya asilimia 50. Unategemea mkurugenzi labda alitaka kutekeleza kipaumbele cha kujenga madarasa au vituo vya afya, fedha atatoa wapi?

"Mfumo huo mpya unaleta changamoto hasa unapopeleka fedha kwenye mfuko mkuu wa hazina na zile pesa walizokuwa wanategemea wanakosa na halmashauri sasa hivi ziko hoi. Walete hela kwa wakati waone kama hazitachangia katika miradi ya maendeleo," alisema. Naye Furaha Mgonja, mkazi wa kata ya Stesheni, alitaka kujua sababu gani za msingi zinazoifanya serikali kutowabana mapema watendaji hao wa halmashauri na kuwaacha hadi kushindwa kufikia lengo lililowekwa.

Aidha, katika taarifa hiyo ya Waziri Jafo, alinukuliwa akisema wakurugenzi 102 wameshindwa kuchangia katika miradi ya maendeleo kwa asilimia 20.



Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Festo Kiswaga, akizungumza na waandishi wa habari wilayani humo mkoani Simiyu juzi, wakati akitoa maamuzi ya kuitaifisha pamba zaidi ya tani 20, ambayo ilikamatwa juzi ikisafirishwa kinyume na utaratibu na kuiuza katika gulio za pamba kisha fedha itakayopatikana itatumika kukamilisha vifaa na ujenzi wa sekondari ya vipaji maalumu. Kulia ni Katibu Tawala wa wilaya hiyo, Veronica Kinyemi. **PICHA: HAPPY SEVERINE**

# Kasi wanafunzi kuolewa kwa siri yaongezeka

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

KIWANGO cha wanafunzi wa shule za sekondari, hasa wasichana wanaotoka jamii ya wafugaji wa Kimasai katika Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro kuchumbiwa kwa usiri mkubwa na kisha kuolewa bado wakiwa shuleni imeongezeka.

Siri ya kuongezeka kwa wanafunzi wanaoendelea kuandaliwa kwa ajili ya ndoa za utotoni, ilifichuliwa jana na Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Magadini, iliyoko Kata ya Gararagua, Felister Kileo, mbele ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Onesmo Buswelu. Kileo aliyasema hayo muda mfupi kabla ya kukabidhiwa madarasa mawili yaliyojengwa kwa zaidi ya Sh. milioni 30 na Africado Limited kwa kushirikiana na serikali. "Idadi ya wanafunzi wa kike ambao wamekuwa wakishindwa kuendelea na masomo na kuolewa baada ya kuhitimu kidato cha nne inapaa kwa kasi. Jambo hili linatokana na usiri mkubwa unaofanywa na wazazi wa pande zote mbili, kukubaliana taratibu za uchumba ziendelee hata mtoto akiwa shuleni, ndiyo maana huwaoni wakiendelea na masomo ya kidato cha tano na sita na hata vyuo vikuu.

"Mwaka 2018 kati ya wanafunzi 79 waliohitimu kidato cha nne shuleni hapa, walioendelea na masomo ya kidato cha tano ni wanafunzi 15 tu," alisema.

Shule hiyo ndiyo kinara kwa shule za kidato cha tano na sita kwa kuwa na matokeo mazuri ya ufaulu katika Wilaya ya Siha katika mitihani ya taifa ya kidato cha sita.

Mmoja wa wazazi kutoka jamii ya wafugaji wa Kimasai, Jeremia Mollel, alikiri kwamba tatizo hilo limekithiri na linatokana na mila kandamizi kuachwa na kuendelea kumea, kwa kisingizio cha kulinda utamaduni wa Wamasai.

Licha ya mafanikio hayo, shule hiyo haina maabara ya sayansi, bwalo la kulia chakula na inakabiliwa na tatizo la wizi kutokana na kukosekana kwa uzio kuzunguka shule hiyo. Akipokea vifaa vya ujenzi na kuzindua vyumba hivyo vya madarasa ya kidato cha tano na sita, Buswelu alisema tayari serikali na wadau wengine wa maendeleo, wameanza kutoa elimu kwa jamii hiyo ya wafugaji kuacha watoto wa kike kuendelea na masomo.

Meneja Utawala wa Africado Limited inayozalisha maparachichi na kuuza katika masoko ya kimataifa, Paschal Shayo, aliishukuru serikali na wananchi wa Siha kwa namna wanavyoipa ushirikiano katika shughuli za maendeleo.

Alisema katika shule hiyo, Africado Limited imetoa vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni tano kusaidia kukamilisha ujenzi wa bwalo la wanafunzi na vyumba vya madarasa.



Ukurasa 16

Wa kukata tamaa walivyopewa uhai wachangamke kupitia nyenzo ya uchumi



Ukurasa 19

...Waziri Mkuu alipojitokeza kumaliza mtihani walima pamba vs wanunuzi


# BUFE

Ijumaa Agosti 16, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




## Mjadala wa mkulima mdogo 88 Moro

Ukurasa 15



# KIZUNGUMKUTI CHA PAMBA 'KUWADODEA' WAKULIMA

**Na Marco Maduhu,** Shinyanga

***IJUMAA iliyopita, katika jarida hili ilikuwa na simulizi ya mtihani wa kufanikisha kufikisha zao la pamba sokoni wilayani Malinyi, mkoani Morogoro, changamoto kuu ni viuatilifu shambani. Endelea na simulizi ilivyo kwa wazoefu wa kuzalisha pamba, Kanda ya Ziwa.***

KILIMO kinapotamkwa kuwa uti wa mgongo wa uchumi wa nchi ni tafsiri pana. Eneo mojawapo ni kwamba, kwa sehemu kubwa inawaajiri Watanzania wengi.

INAENDELEA UK.14

UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

## Mradi unaowanasua waliokwama baada ya shule hadi ujasiriamali

Ukurasa 20

BIASHARA

# KIZUNGUMKUTI CHA PAMBA 'KUW

• RC Shinyanga, RAS wafunguka namna ilivyowatesa • Wakulima, wanu
mtihani uliowakuta • Waziri Hasunga akawafuata waliko akiwa na maji



Wakulima wa pamba kutoka mikoa ya Shinyanga, Mwanza na Wilaya ya Igunga, Mkoa wa Tabora, walipopeleka pamba yao kuuza kwenye kiwanda cha Afrishani miini Shiny

INATOKA UK.13

Vivyo hivyo, katika orodha ya mazao muhimu ya biashara na kimkakati kilimo imo pamba, inashika nafasi kubwa na muhimu katika uchumi nchini, kwa maeneo kama malighafi na ajira ya kundi kubwa la Watanzania .

Idadi kubwa ya Watanzania wanashiriki kukuza uchumi kupitia kilimo moja kwa moja, wanaoishi vijijini na katika eneo la Kanda ya Ziwa wamejikuta zaidi kwenye zao la pamba, ambalo wanalo katika uzalishaji tangu kabla na baada ya uhuru.

Mara baada ya uhuru nchini, serikali ilianzisha viwanda vya kati, kutumia malighafi hayo ya pamba na mengine kiuzalishaji bidhaa kama nguo na uzi.

Hapo ndipo kunapokuja simulizi ya viwanda vya nguo nchini zilizotumia mazao ya pamba, mfano jiji Dar es Salaam, Gongolamboto kulikuwapo Kiltex na Sunguratex, Ubungo kilikuwapo Urafiki.

Vingine ni Mwatex (Mwanza), Mutex (Musoma), Tabotex (Tabo-

> **Marekani waliweka vikwazo kwenye bidhaa zinazotoka China na kusababisha bei kwenye soko la dunia la pamba kushuka kutoka seti 77 hadi 65 kwa paundi.**



# ADODEA' WAKULIMA

## unuzi wasimulia bu



vanga. **PICHA ZOTE MARCO MADUHU**



ra), Mbeyatex (Mbeya) na Morogoro.

Kwa bahati mbaya, sehemu kubwa havifanyi kazi baadhi kama Kiltex na Sunguratex, vimeshatoweka kabisa. Kikwazo kikubwa ni soko la kigeni kuvamia nchini.

Ni mabadiliko yaliyochukua sura ya kutegemewa soko la kigeni kama ilivyokuwa kabla ya uhuru, pamba inauzwa kwenye masoko ya nje na kuchangia kushindwa kufufuliwa viwanda vya ndani ya nchi.

Mkulima anakwazika, anakwama katika bei yake ya kununua kutokuwa rafiki wao wanaendelea kuwa masikini.

Katika msimu uliopo wa kuuza zao la pamba chini, kumetokea tatizo la wakulima kushindwa kuuza pamba yao na wengine kuishia kukopwa kupitia kwenye vyama vya msingi vya ushirika, maarufu kama 'Amcos' kwa sababu ya ukosefu wa fedha.

**MGOGORO SOKONI**

Ni tatizo lililosababisha ukosefu wa fedha hizo ni baada ya mununuzi mkuu wa pamba hivi sasa China, kuingia msuguano na Marekani, hali inayotasfsiriwa kuchangia kushusha thamani ya dola sokoni. Inatajwa asilimia 70 ya pamba ya Tanzania, inanunuliwa nchini China

Baada ya kushuka dola, kukasababisha taasisi za kifedha na hasa benki nazo kushindwa kuwakopesha fedha wafanyabiashara wa chini, wanaonunua pamba hiyo kwa wakulima, hofu yake ni kupata hasara ya kutorudishiwa fedha zao, kwa sababu thamani yake inashuka kwenye soko la pamba duniani.

Wafanyabiashara walipokosa mikopo, nao wakashindwa kununua pamba kupitia fedha zao mbadala wakihofu hasara, kwa sababu baada ya dola kushuka bei elekezi ya serikali ilisimama Sh. 1,200 hofu kuu sasa ni hasara sokoni.

Baada ya kuwapo mknaganyiko, baadhi ya wakulima walianza kuuza pamba kwa wafanyabiashara wajanja waliolangua kwa bei ya Sh. 500 kwa kilo kutokana na wakulima kuelemewa mahitaji ya pesa za kukidhi mahitaji ya kifamilia wakiendelea kuelemewa na lindi la umaskini.

**WAZIRI HASUNGA**

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, anaanika changamoto inayosababisha kusuasua ununuzi wa pamba nchini ni mgogoro wa uchumi kati ya China na Marekani.

"Marekani waliweka vikwazo kwenye bidhaa zinazotoka China na kusababisha bei kwenye soko la dunia la pamba kushuka kutoka seti 77 hadi 65 kwa paundi," anasema Hasunga.

"Kushuka kwa bei hiyo ya pamba kwenye soko la dunia kumekaathiri wafanyabiashara wetu, walipokokotoa wakienda kununua pamba kwa bei ya 1,200 watapata hasara na wafanyabiashara wengi wanatengemea fedha kutoka kwenye mabenki.

"Nayo yaligoma kuwapatia fedha kwa kuhofia kupata hasara na kusababisha kusuasua kwa ununuzi wa pamba kwenye maeneo mengi,"anafafanua Hasunga.

Waziri ana mtazamo wa haja ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT), itoe dhamana kwa taasisi hizo za kifedha, ili ziweze kuwapatia mikopo wafanyabiashara na kwenda kununua pamba ya mkulima, Serikali ikiwajibika na hasara, endapo bei ya dola sokoni ikiendelea kuwa chini.

Hasunga anarejea kikao chao na |Waziri Mkuu Kassim Majaliwa mkoani Tabora, Julai 14, maamuzi ya kwanza yalikuwa kuishusha bei pamba, ili iendane na soko hilo la dunia, lakini wakaweka mtazamo watamuumiza mkulima na kuazimia bei ya pamba ibaki Sh. 1,200.

"Tanzania huwa tunapanga bei ya kununua pamba kutoka kwa mkulima, kulingana na bei ya soko la dunia ikoje. Mara baada ya dola kushuka, ingetulazimu kununua pamba kwa mkulima kwa bei ya Sh. 900 kwa kilo moja, lakini kutokana na Serikali yetu ya wanyonge ikaona italipa hiyo Sh. 300 kwa wafanyabiashara," anasema Hasunga.

Anatoa wito kwa wakulima wa pamba kujikita kwenye kilimo chenye tija kitakachowapatia uzalishaji wa kilo nyingi kwenye heka moja na kuacha kulima kimazoea ambapo watapata kilo chache na kuanza kulalamikia bei iongezwe lakini wakilima kitaalamu watapata mavuno mengi na kukua kiuchumi.

Waziri Hasunga anadokeza utaratibu unaoendelea kukamilishwa na BoT, pamba yote ya mkulima waliokopwa na Ancos watalipwa pesa zao zote.

**MKOA SHINYANGA**

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu Telack, anapongeza juhudi za Serikali za kutatua tatizo hilo la ununuzi wa pamba, kwani hali ilikuwa mbaya kufikia wakulima wanapelekewa fedha Sh. milioni tano na wanalipwa wachache, zinaisha mara moja wengine wakibaki wamekopwa.

"Naomba wakulima wa pamba mkoani Shinyanga, changamoto hii ambayo imejitokeza isiwakatishe tamaa ya kuendelea kulima zao la pamba, pamoja na kuliweka katika hali ya usafi ili liendelee kuwa bora kwenye masoko ya nje,"anasema Talack.

Katibu Tawala wa Mkoa Shinyanga, Albert Msovela, anasema kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi Mwaka 2012, Shinyanga ina jumla ya wakazi milioni 1.9, kati yao asilimia 80 ni wakulima na mazao yao makuu ya biashara

**INAENDELEA UK.18**

# Mjadala wa mkulima mdogo 88 Moro



Mfanyakazi wa kampuni ya Farmbase, Shaha Simbaliana, akionyesha mashine ya kupukuchua mahindi, anayoamini inamfaa mkulima mdogo, katika Maonyesho ya Wakulima Nanenane, yaliyomalizika mjini Morogoro. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

UCHUMI wa Tanzania, moja ya mbeleko zake kuu ni kilimo. Hiyo inajulikana! Lakini kinapoangaliwa kikosi kazi cha wakulima hao, basi wakulima wadogo ndio wanachukua nafasi kubwa zaidi. Nayo haina ubishi!

Sasa wakulima nao wana ombi kwamba Serikali iwawezeshe katika mikopo, ili wanunue mashine ndogo za kisasa za kilimo zitakazowawezesha kuzalisha mazao mengi, kwani pasipo mtaji, mkulima hatonyanyuka.

Ni rai iliyojitokeza katika Maonyesho ya Nanenane, yaliyomalizika mjini hapa, baadhi wakilalamika bado wana changamoto ya mtaji.

Akizungumza katika banda la kampuni ya Farmbase kwenye Maonyesho ya Wakulima kanda ya Mashariki, kwenye viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, mkulima Anna Komba, anasema wakulima wengi wapo katika hali ya chini kiuchumi na hawawezi kununua zana nyingi.

Anna anasema, zana zilizopo kwenye banda hilo ni nzuri na zina bei ya chini na mkulima akizifuatilia anaweza akafanikiwa ambapo aliwataka wakulima wenzie kutembelea banda na maduka Farmbase ili kuzipata kwani matumizi ya jembe la mkono kwa sasa yameshapitwa na wakati.

Pia, anaiomba Serikali kuwasaidia katika upatikanaji wa pembejeo kwa wepesi, kwani wakulima mara nyingi wanapata shida ya pembejeo ya mazao yao huwa yanaharibika sana.

Meneja Kiongozi wa Mashine wa Farmbase, Suleiman Ben, anasema, wao lengo lao kumsaidia mkulima kupanda hatua ya juu kukuza uchumi wao kupitia kilimo.

Anataja maeneo walioijiandaa kuwa ni katika dawa, mbegu na mashine zikiwemo trekta, majembe na kifaa kinachoitwa 'mini tillerr' ambacho kinachotumiwa na wakulima wadogo, kuipa trekta uwezo maradufu.

"Lengo ni 'kuwabust' wakulima wadogo waweze kupanda kwenye 'production (uzalishaji). Mashine ni imara na mashine hizo hutumia dizeli, kama power tila hutumia dizel nusu lita na kulima zaidi ya saa moja," anasema.

Mbwana Bernard, ofisa wa kampuni hiyo anasema, wakulima wengi waliopo vijijini hawajui kuwapo tofauti kati ya vifaa bora na duni, jambo ambalo ni tatizo katika jamii, hasa kada ya wakulima.

Mkurugenzi wa Farmbase, Ahmed Msellem, anasema mkulima mdogo mara nyingi anapaswa kuinuliwa, kwani hana uwezo wa kununua mashine zinazouzwa kwa gharama kubwa, anabaki akiendelea kutumia kilimo cha jembe la mkono ambacho hakina tija katika maisha ya sasa.

Anasema, katika kumsaidia mkulima mdogo anaona haja ya kuletwa mashine ndogo na rahisi ambazo mkulima anaweza kutumia na kuona faida ya kilimo mahali aliko katika safari ya kitaifa iliyoko kusaka kipato cha kati ifikapo mwaka 2025.

BIASHARA

PALE INAPOWEZEKANA...

# Wa kukata tamaa Rorya walivyopewa uhai wachangamke kupitia nyenzo ya uchumi

• Walionyanyapaliwa, kutengwa wamiliki chao • CGF yawaandalia njia kupitia vikundi 43 Mara



Kikundi cha Upendo Agape.



kikundi cha wanawake Mkono kwa Mkono.

**Na Anthony Gervas,** aliyekuwa Rorya

SEHEMU iliyopita ya makaka ya toleo la jarida hili jana ilikuwa na simulizi namna shirika lisilokuwa la kiserikali la Grain to Grow Foundation (GGF), ambalo limeingia wilayani Rorya Mkoa wa Mara katika staili ya ubia na Serikali ya wilaya, kuhamasisha miradi ya maendeleo katika eneo la kukabili ukosefu wa maji, ikionyesha mageuzi makubwa .

Ikiwa mwendelezo wa uchunguzi wa Nipashe wilayani humo, ilipata tafsiri pana ya malengo yake, inayojikita zaidi katika kusimamia utoaji huduma sawa za kijamii zilizolenga ushirikishwaji na kuzingatia haki katika kunufaika na matumizi ya rasilimali zilizopo.

Hiyo ni katika ushiriki wa kila mmoja kuanzia familia na jamii kwa ujumla, ikiwa inalenga kuletea maendeleo endelevu, kushirikiana na wadau wengine wa nje na ndani wenye mtazamo wa kupunguza umasikini uliokithiri katika jamii.

Ni kwa vipi? Ikiwa katika wilaya za Rorya na Butiama mkoani Mara, Nipashe ilishuhudia miradi ya kuisaidia vikundi mbalimbali vya wajasiriamali wadogo vijijini katika wilaya hizo, ambavyo CGF inajishughulisha navyo.

Sehemu kubwa ya walioubuliwa na kujumuishwa ni wanaoangukia katika tafsiri ya 'hali ngumu kimaisha' wakigawanywa kulingana na aina ya makundi yao.

Hapo inajumuisha miradi midogo ikiwamo kilimo cha mahindi, maharage, mihogo, ufugaji kuku wa kienyeji, kondoo, ufumaji wa soksi, kofia, utengenezaji mazulia, cheni, rozari na uuzaji sabuni za unga na miche.

> **Sehemu kubwa ya walioibuliwa na kujumuishwa ni wanaoangukia katika tafsiri ya 'hali ngumu kimaisha' wakigawanywa kulingana na aina ya makundi yao.**



Kikundi cha Tuaminiane. **PICHA ZOTE: ANTHONY GERVAS**

### MKURUGENZI GGF.

Mkurugenzi Mtendaji wa shirika hilo, Amillen Saria, anasema wamekuwa wakivisaidia vikundi 43 vya wajasiriamali kutoka wilaya hizo mbili. Kati yake, anasema 25 viko wilayani Rorya na vikundi 18 kutoka wilayani Butiama.

"Jumla ya vikundi vya wajasiliamali tunavyovisaidia ni 43 kati ya hivyo 25 kutoka Wilaya ya Rorya na 18 wilaya ya Butiama, lakini kwa sasa tunaendelea kuvisaidia vikundi vinne kutoka wilaya hizo, ambavyo ni Imani, Upendo Agape na Tuaminiane vilivyopo katika kata ya Baraki Rorya na kikundi kimoja cha Mkono kwa Mkono kilichopo Buturi Butiama," anasema Saria.

### KIKUNDI IMANI

Anafafanua kuwa kikundi Imani kilianzishwa mwaka 2017 kwa malengo ya kuwaunganisha watu wa rika zote wanaoishi na virusi vya ugonjwa wa Ukimwi.

Pia, anataja mtazamo mwingine ni kuwakusanya watu wanaoishi kwenye mazingira magumu na hatarishi, kutokomeza dhana potofu ya kunyanyapaliwa, kudharauliwa katika jamii wanazoishi nazo na kuwazunguka.

Anasema, kikundi hicho kilianza na wanachama 25 hai, na shughuli yake ya kwanza ilikuwa kufanya vibarua vya kilimo mashambani wakipalilia na baadaye walikubaliana kuchanga fedha na kukopeshana kwa riba nafuu.

Saria anasimulia namna ilivyotanua shuguli zake kwamba, walifikia hatua zaidi ya kuanzisha mradi wa kufuga kuku wa kienyeji na faida walioipata walinunua mbuzi.

Mwenyekiti wa kikundi hicho cha Imani, Tatu Mussa anatafsiri ujio wa shirika hilo kuwa ni 'mapenzi ya Mwenyezi Mungu' huku anafafanua mchakato wake katika mtazamo wa kiuchumi kwamba:

"Katika kikundi chetu baada ya kuliona limekuja kijijini hapa 2017, tuliomba litusaidie tuweze kufanya kazi za kilimo, ili kumfukuza adui njaa. Pili, kujikwamua kwenye umaskini; tatu, tulime mazao yatakayotupatia fedha tuweze kuendesha shughuli za kikundi na baadaye kugawana faida baada ya kuuza mazao hayo."

Anasema, hivi sasa wameiomba CGF kuwasaidia zana za kilimo za kisasa zikiwamo jembe la kukokotwa na ng'ombe, mbolea, mbegu bora, mashine ya umwagiliaji kilimo cha nyanya, mboga mboga, matikiti na kabichi, ili kuondokana na changamoto zinazokikabili kikundi chao.

### KIKUNDI TUAMINIANE.

Mwenyekiti wake, Faustine Kitoka, anasema kwamba kikundi chao kilianzishwa kwa lengo la kuwasaidia wanakikundi kuondokana na wimbi la umasikini kwa kuanzisha miradi ya kuboresha kilimo na ufugaji ng'ombe wa kienyeji.

Kuhusu mafanikio kuptia msaada wa CGF, Kitoka anasema:"Mafanikio ya kikundi chetu cha Tuamimiane wanachama sasa hivi tumeanza kukopeshana (pesa) kwa riba ya asilimia tano kwa mwezi na kila mwanachama anaweza kukopa wastani wa Sh. 40,000 na chanzo cha mapato yetu ni ada za wanachama."

Kiongozi huyo pia anadokeza changamoto kubwa inayowakabili ndani ya kikundi kukosa vitendea kazi vya kuendesha kilimo na kutokuwa na mashamba, kwani wanayolima kwa sasa ni mashamba ya kukodi.

Anataja gharama ya kukodi ni kubwa kwamba Sh. 180,000, hivyo rai yake kwa shirika mama ni kuwasaidia msaada wa kupata mashine ya kutumia umeme ya kusaga nafaka, pia mkokoteni kwa ajili ya kusomba mazao yao shambani wakati wa mavuno.

### UPENDO AGAPE.

Kikundi cha Upendo Agape kilianzishwa mwaka 2016, kwa lengo la kuboresha maisha ya wanakikundi wenyewe kiuchumi na kijamii katika kufanya kazi za ujasiriamali, ili kuondokana na wimbi la umaskini kutoka kwa wanachama wake, akitaja kati yao 28, wako ni walemavu.

Katibu wa Kikundi hicho, Mtatiro Chacha, anafafanua zaidi akisema: "Kikundi hiki kinajishughulisha na miradi ya kijasiriamali ya ufugaji wa kuku wa kienyeji, kondoo, kilimo cha mahindi, ufuta na maharage."

"Lakini baada ya kupata msaada kutoka GGF kilianzisha pia utengenezaji wa mazulia na rozali baada ya kusaidiwa na shirika hilo," anaongeza Chacha.

Anataja changamoto mbele yao ni pamoja na wanakikundi wenye ulemavu kukosa baiskeli za kutembea, hivyo inakwamisha nyendo zao, pia hawana zana za kilimo zinazotosheleza mahitaji yao, pamoja na mashine za umwagiliaji wakati mvua zinapokosekana katika msimu wa masika.

Mbali na changamoto, Chacha anajivunia mafanikio ya kupata ujuzi wa kutengeneza vitu mbalimbali kupitia msaada wa shirika la CGF ambao wanawafadhili, akitaja baadhi ni kuhudhuria semina mbalimbali, kupatiwa pembejeo za kilimo, mahitaji ya ufumaji wa soksi, kofia, pia ya kutengeneza mazulia, rozali na cheni mbalimbali.

### MKONO KWA MKONO.

Hicho ni kikundi mahsusi cha kinamama wajasiliamali wadogo kilichoanzishwa mwaka 2015, ambacho sasa kina wanachama 30, lengo lake kuu ni kusaidiana kati yao wenyewe katika nyendo za kijasiriamali na kilimo,

Mwenyekiti wao, Pili Frank, anafafanua kuwa GGF imewawezesha kupata fursa mbalimbali zikiwamo pembejeo za kilimo, vifaa vya kilimo kama vile maksai wa ng'ombe wa kukokota kwa mkokoteni, kulima na jembe la plau na kuwe na maghala ya kuhifadhi chakula.

"Wanachama wa kikundi tunakopeshana fedha tunalo pia shamba darasa la mihogo na tuna mfuko wa jamii, kila wiki mwanachama anachangia Sh. 500," anasema Pili.

***Mwandishi wa makala hii anapatikana kupitia simu: (+255) 0682 86 92 44 au barua pepe: anthonygervas@yahoo.com***

# Biashara katika picha



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akisisitiza jambo kwa wafanyakazi wa Benki ya NMB, alipotembelea banda la benki hiyo, kwenye maonesho ya Wiki ya Uwekezaji mkoani Kagera yanayoendelea katika viwanja vya Gymkana mjini Bukoba juzi. Kulia kwake ni Mkuu wa Mkoa huo, Brigedia Jenerali, Marco Gaguti. Benki ya NMB ni mdhamini wa Wiki ya Uwekezaji ya mkoani Kagera. **NA MPIGAPICHA WETU**



Wachuuzi wa bidhaa mbalimbali wakizinadi kwa abiria waliokuwa wakisafiri na basi la Hajees, katika Kituo cha Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**



Wachuuzi wakiwa wamepanga bidhaa zao pembezoni mwa reli maeneo ya vingunguti jijini Dar es Salaam jana, jambo ambalo ni hatari kwa usalama wao. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

BIASHARA

# KIZUNGUMKUTI CHA PAMBA ‘KUWADODEA’ WAKULIMA



Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga (watatu kutoka kushoto) akiwa na uongozi wa Mkoa wa Shinyanga, kukagua ununuzi wa pamba kwenye kiwanda cha Afrishani, mjini Shinyanga, ambako wakulima walipeleka kuuza pamba yao hapo baada ya vyama vya msingi vya ushirika kushindwa kuinunua. **PICHA: MARCO MADUHU.**

**INATOKA UK.13**

ni dengu, mkonge, tumbaku na pamba ambao.

Msovela, anasema katika msimu wa kilimo (2018-19), walihamasisha wakulima wengi kulima pamba na kufanikisha hekta 97,270 na hadi sasa zimeshavunwa tani 48,435. ikiwa msimu wa mavuno bado unaendelea.

“Changamoto iliyopo kwenye ununuzi wa zao hili la pamba ni ukosefu wa fedha wa kununua pamba kwa mkulima kupitia kwenye vyama vyetu vya msingi vya ushirika na ninawaomba wakulima wawe wavumilivu wakati Serikali ikilishughulikia tatizo hili,” anasema Msovela.

**KIWANDA PAMBA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha Kununua Pamba mkoani Shinyanga (Afrishani), Ally Habshy, anasema awali walishindwa kununua pamba kutoka kwa mkulima kutokana na kushuka bei ya dola kwenye soko la pamba duniani.

> **“Mimi nimeshavuna pamba yangu tani moja, nimeshaiweka ndani tu nikisubiri pesa zije kwenye chama chetu cha msingi cha ushirika hapa kijiji, ndipo niiuze.**

Habshy anasema, walinunua pamba kwa bei ya Sh. 1,200 wakihisi kupata hasara na ilipaswa bei ishuke chini zaidi na Serikali ilijitokeza na ahadi ya kulipa fidia hasara, hivyo kiwanda chake kimeshaanza kununua pamba kwa kufanya anachokiita ‘kuweka Amco nje ya kiwanda chake’ na mkulima atalazimika kupeleka pamba kiwandani hapo kwa gharama yake mwenyewe.

Anasema amelazimika kufanya hivyo, kuweka Amcos nje ya kiwanda chake, ili kujieupusha na gharama zingine za usafirishaji na matengenezo ya magari, ikiwa bei ya pamba kwenye soko la dunia itabaki Sh. 1,200.

**WAKULIMA**

Mwenyekiti wa Chama cha Msingi cha Ushirika ya Uzogole Shinyanga Mjini, Kulwa Chagu, anasema wameshanunua pamba ya mkulima Tani Tisa, lakini hawana pesa ya kumlipa mkulima na wamewakopa na pesa zikifika watawalipa stakabadhi zao za madai.

Peter Samsoni, ni mkulima wa pamba kutoka kijiji cha Mwaweja wilayani Kishapu, Shinyanga, anayesema ameshavuna pamba tani moja, lakini alipopeleka kuiuza kwenye Amcos, akaambiwa pesa hakuna labda akopwe. Aliahirisha kuuza.

Anasema walakini huo umesababisha baadhi ya wakulima wenzake wenye shida kulazimika kuwauzia walanguzi bidhaa yao kwa bei ya Sh. 500 kwa kilo moja, jambo litakaolowafanya wapate pesa kidogo na kukwama kiuchumi.

“Mimi nimeshavuna pamba yangu tani moja, nimeshaiweka ndani tu nikisubiri pesa zije kwenye chama chetu cha msingi cha ushirika hapa kijiji, ndipo niiuze. Tofauti na hapo, nitaendelea kuwa nayo ndani, japo ni hatari. Inaweza hata kuungua,” anasema Samson.

“Tunasikitika sana Serikali yetu imetuhamasisha sana wakulima tulime zao la pamba kwa wingi na tukaitikia, lakini sasa hivi tunataka kuuza pamba yetu, tunaambiwa pesa hakuna, yani mara mia ningelima hata mpunga, sasa hivi ningekuwa na hela zangu tu,” analalamika.

Mkulima Kazwenge Marco, kutoka kijiji cha Ilobashi Kata ya Masengwa, Shinyanga Vijijini, anasema naye ameshavuna tani nne za pamba, lakini ameshindwa kuiuza kwa sababu ya kuambiwa hakuna pesa,. hivyo akaamua kukaa nayo nyumbani.

Anasema, licha ya kutoiuza pamba kwa bei elekezi ya serikali, shilingi 1,200 kwa kilo moja, bado siyo rafiki kwa mkulima, ikilinganishwa na gharama wanazotumia hadi kuvuna.

“Mimi nimelima ekari nne za zao la pamba sawa na kilo 4,000. Nimetumia jumla ya gharama zote hadi kuvuna Sh. 600,000. Ukijumlisha kwa bei ya Sh. 1,200 kwa kilo 40,000 nitapata Sh. 4,800,000 nkitoa laki sita nitapata Sh. 4,200,000 kwa mwaka mzima, nikianza kutoa pesa ya msimu ujao pesa ambayo itabakia ni kidogo sana,”anasema Marco.

Paulo Ntani ni mkulima wa zao la pamba kutoka kijiji cha Ilobashi katika kata ya Masengwa, Shinyanga Vijijini, anasema ni mara yake ya kwanza kulima zao hilo.

Anasema, awali alilima mpunga, lakini kutokana na hali ya hewa kwenye shamba lake la ekari moja amepata kilo 200 na pamba yake bado hajaiuza.

Ntani anasema, anasubiri fedha za Amcos bei ya pamba kupanda katika matarajio yake ya walau Sh. 1,500 kwa kilo, ili kumsaidia kumaliza kukidhi matatizo yake kifamilia.

“Nilijaribu kulima zao la pamba mara baada ya kutolewa hamasa na viongozi nikaona ngoja nijaribu, lakini kwa bahati mbaya nimepata mavuno kidogo kilo 200.

“Nikiuza kwa bei ya Sh. 1,200 nitapata Sh. 240,000, nikitoa na gharama ambayo nimetumia Sh. 200,000 nitabakiwa na 40,000 kwa mwaka mzima,” anasema Ntani.

“Kama serikali inania kweli ya kutuinua sisi wakulima kiuchumi, tunaomba pesa ziwe zinapatikana kwenye ‘Amcos’ pamoja na kuongeza bei ya kununua pamba angalau ikaribie hata kwenye Sh. 2,000 kwa kilo.

“Sasa hivi tumetangaziwa kuwa pembejeo tutakuwa tunanunua wenyewe , siyo za mkopo tena hali ndio inazidi kuwa mbaya” anasema.

***Makala hii imeandaliwa kwa mujibu wa yaliyojiri ziara ya Waziri wa Kilimo, mwezi uliopita. Katika ukurusa wa 19, pata picha kamili ya mtazamo wa kiserikali ulikofikia sasa kutoka yaliyojiri ziara ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, siku chache zilzopita.***

BIASHARA

# ...Majaliwa alipojitokeza rasmi kumaliza mtihani soko la pamba



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alipokuwa katika ziara yake kukagua ununuzi wa pamba mjini Shinyanga, siku chache zilizopita. **PICHA ZOTE: MARCO MADUHU.**

**Na Marco Maduhu,** Shinyanga

NI tatizo zito lililomnyanyua Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, kufika katika eneo la tukio kuwa shuhuda na kuwashirikisha maamuzi makuu.

Hili ni zao ambalo hata kabla ya matatizo ya sasa amekuwa akilipigia 'debe' kwamba liko kimkakati na lina nafasi ya kuleta mageuzi ya uchumi wa nchi na watu wake.

Mara baada ya kufanya ziara mkoani Shinyanga, Agosti 9 mwaka huu, kuangalia hali ya ununuzi wa zao la pamba, akakumbana na changamoto ya kuwapo kasi ndogo ya ununuzi wa zao hilo kutoka kwenye viwanda vinavyowajibika na kufanya uchambuzi, sababu kuu ikiwasilishwa ni upungufu wa fedha.

Anasema, kutokana na Serikali kumjali mkulima, ilibidi waingie makubaliano na taasisi za kifedha nchini ziwakopeshe fedha wanunuzi wa pamba, ili zipate nguvu za kununua kwa mkulima na waweze kupata fedha zao kwa wakati, ili wajiandae na msimu ujao wa kilimo.

Majaliwa anasema, pamba ikibaki kwa mkulima maana yake ni kumbebesha hasara, pamoja na kukosa pesa za kuendesha kilimo katika msimu ujao.

Waziri Mkuu anataja kuwa moja ya kigezo kilichoisukuma Serikali kuchukua dhamana ya kuzitaka taasisi za fedha kuwakopesha wafanyabiashara, ili pamba itoke kwa mkulima na wao kama Serikali watakaa na wafanyabiashara kutafuta masoko ya pamba, nje ya nchi.

> **Pamba ikibaki kwa mkulima maana yake ni kumbebesha hasara, pamoja na kukosa pesa za kuendesha kilimo katika msimu ujao.**

"Lengo la Serikali ni kumlinda mkulima wa pamba asiweze kupata hasara, bali aweze kunufaika na kilimo chake, pia, kumlinda mfanyabiashara naye asiweze kupata hasara na ndio maana tukaweka dhamana benki pale tutakapo kosa masoko nje ya nchi, basi ile hasara Serikali tutaifidia," anasema Waziri Mkuu.

"Kutokana na changamoto niliyokutana nayo hapa ya kasi ndogo ya ununuzi wa pamba kwenye kiwanda hiki cha Fresho cha kuchambua Pamba Shinyanga Mjini na sababu nilizopewa ni kuwapo upungufu wa fedha, hivyo nahimiza sasa mabenki yote muongeze kasi ya utoaji fedha ili pamba ipate kununuliwa," anaongeza.

## FUNGUENI VIWANDA

Pia, anawataka wamiliki wote wa viwanda vya kuchambua pamba nchini, hasa wazawa. kuongeza wigo wa viwanda vyao kwa kufungua viwanda vingine vinavyotumia malighafi ya pamba, vikiwamo vya nyuzi na nguo, kuondokana na changamoto ya utegemezi wa kuuza pamba nje ya nchi.

"Natoa wito kwa wafanyabiashara wazawa wa viwanda vya kuchambua pamba ikiwamo Shinyanga, fungueni sasa na viwanda vya kusokota nyuzi na kutengeneza nguo na kama mnaona gharama ni kubwa, mnaweza kuunganisha nguvu ya pamoja na kufungua viwanda hivi ambavyo vitawasaidia pia kupata pesa nyingi," anahimiza Majaliwa

"Niwape tu hesabu ndogo ambayo mtaweza kupata faida endapo mkifungua viwanda hivi vya kusokota nyuzi na kutengeneza nguo. Unaona sare zote za wanafunzi wanatumia pamba, tenda hizo zitakuwa za kwenu na bado nguo za wananchi na hata makoti yangu nitakuwa nakuja kushonea hapa Shinyanga," anawahimiza.

Mazumguzo ya Majaliwa, msisitizo wake mkubwa ulikuwa namna ya kuondokana na changamoto inazoikabili soko la zao la pamba, kupitia ufunguzi wa viwanda vingi na kuacha kutegemea masoko ya nje ya nchi, akiwahakikishia watakaodhubutu, Serikali itawashika mkono.

Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda cha kuchambua kilichopo mjini Shinyanga (Fresho), Fred Shoo, anasema licha ya Serikali kuhamasisha benki kuwapatia mikopo, bado ni ndogo na isiyoridhisha, hali inayochangia kasi ndogo katika ununuzi wa pamba kutoka kwa mkulima.

"Changamoto ambayo ipo kwa sasa ni taasisi hizi za kifedha kushindwa kutii maagizo ya serikali kwa ufasaha, na kushindwa kutupatia fedha za kutosha, ambazo zitatusaidia kununua pamba yote ya mkulima na ndiyo maana kumekuwapo kasi ndogo ya ununuaji pamba," analalamika Shoo, mbele ya Waziri Mkuu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha Kuchambua Pamba cha mkoani Shinyanga (Afrishani), Ally Habshy, anarejea kauli ya mwezi uliopita kwa mkuu wa mkoa, kwamba walishindwa kununua pamba kutokana na kushuka thamani ya Dola ya Marekani inayotumika katika mabadilishano kimataifa, wakihofu hasa kuwaangukia.

Baada ya tamko la Waziri Mkuu la Serikali kuahidi kulipa fidia ya hasara, Habshy anasema ameshaanza kununua pamba hiyo kutoka kwa mkulima kwa kuweka vituo vya vyama vya ushirika, ambao ni wakala wa ununuzi nje ya kiwanda chake anakofanya malipo, pia ikiwa ni kigezo cha kujipunguzia gharama.

Ni hatua inayopongezwa na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu Telack, katika namna ya kuitafsiri kwamba ni sehemu ya kupumua kutoka mtihani uliopita, mkulima kukosa soko la jasho lake la msimu mzima

Wito wake kwa walima pamba mkoani kwake nji kwamba, changamoto hiyo iliyojitokeza ya kusuasua ununuzi wa zao hilo, isiwakatishe tamaa bali waendelee kulima, pamoja na kuweka katika hali ya usafi, iendelee kufikia ubora unaotakiwa sokoni.

UCHUMI

# Mradi unaowanasua waliokwama baada ya shule hadi ujasiriamali



Mkurugenzi wa Kituo cha Maarifa, Selemani Bishagazi (kushoto), akimuonyesha Naibu Meya wa Manispaa ya Ilala, Omary Kumbiramoto, mboga zinazolimwa na wanakikundi chake na kuwaingizia kipato.

**Na Yasmine Protace**

YANAPOZUNGUMZIWA makundi, zaidi inamaanisha mkusanyiko wa watu kwa ajili ya kutekeleza nia fulani ya kijamii. Ni kawaida, makundi yanakuwa kwa maana maalum na matunda ya kazi zake kusifiwa kuwa chanya zaidi.

Hata itakumbukwa kaulimbiu iliyotumika zaidi nchini na hasa baada ya uhuru "Umoja ni Nguvu, Utengano ni Udhaifu" ilibeba ujumbe mkubwa kuonyesha inatoa matunda chanya katika kila kinachotekelezwa katika mfumo wa kujumuika.

Kuna makundi yanaanzishwa kwa ajili ya kufanya mradi au kufanya jambo fulani, ikinuia kwa ajili ya maendeleo mbayo yanashuka hadi ngazi ya maisha ya mtu mmoja mmoja.

Serikali kupitia njia hiyo imekuwa ikihamasisha vijana wajiunge katika makundi ili waweze kunufaika na mikopo ambayo imekuwa ikitolewa na Serikali kwa ajili ya ujasiriamali.

Hata benki nyingi na asasi nyinginezo za kifedha, zimekuwa na kanuni, miongozo na sheria, zinazowezesha watu kupata mikopo katika njia ya vikundi.

Jumuiya za ushirika wa aina mbalimbali, ikiwamo ya kuweka na kukopa maarufu kama 'saccos' nazo ni mazingira ambayo yanawawezesha watu kukopeshana ndani ya mjumuiko wa kijamii. Katika hilo, mikopo inayotolewa na Serikali kwa vijana imekuwa mkombozi kwao kuwainua kimaendeleo na hasa kiuchumi.

**NAIBU MEYA**

Naibu Meya Manispaa ya Ilala, jijini Dar es Salaam, Omary Kumbiramoto, anawataka vijana wachangamkie mikopo kwa nia ya kunufaika nayo

Ni kauli aliyoitoa alipofungua mafunzo ya mwezi mmoja kwa watoto waliotoka katika mazingira magumu, katika Kata ya Ukonga.

Naibu Meya anafafanua kwamba Serikali inayasaidia makundi maalumu, kwa kutatua changamoto zao, ikiwamo kuwawezeshea mikopo wanawake na vijana. Anawaasa vijana kwamba ni jukumu lao kujiunga katika makundi, ili wanufaike kiuchumi kupitia daraja la mikopo na akiwakumbusha kwamba elimu inayotolewa na kituo itawasaidia vijana hao kujiongezea kipato.

> “ wanaokuwa na changamoto za kimaisha, inapotokea wakiwezeshwa wanaweza kuleta mabadiliko ya kiuchumi katika maeneo yao wanayoishi.



Wanakikundi wakijifunza ujasiriamali katika Kata ya Ukonga. **PICHA ZOTE: YASMINE PROTACE.**

**MKURUGENZI**

Mkurugenzi wa Kituo cha Maarifa ya Jamii, Selemani Bishagazi, anasema jumla ya vijana 100 watanufaika na mafunzo hayo, kutoka kwa walimu wataalamu waliobobea katika stadi ya ujasiriamali.

"Mafunzo haya ni ya mwezi mmoja, yanatolewa na hakuna gharama zozote ambazo watalipa. Watajifunza kutengeneza mifuko, mishumaa, batiki, kuweka dawa, kichwani, kutengeneza keki, kupamba ukumbi na kilimo cha mbogamboga," anaeleza.

Bishagazi anasema kuwa mafunzo hayo yanatolewa katika Kata ya Ukonga, ambako vijana wanaoishi katika mazingira magumu kutoka maeneo mbalimbali ya kata watanufaika na mafunzo hayo.

Mwenyekiti wa Sauti ya Jamii, Fatma Abdulrahman, anasema wamekuwa wakiiangalia jamii inayowazunguka na kubaini watoto wengi hawajaendelea au kupiga hatua ndogo, baada ya kumaliza elimu za msingi na sekondari.

Anasema baada ya kubaini hilo, waliamua kuwachukuwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu na kuwafundisha elimu ya ujasiriamali, ili iweze kuwa mkombozi katika maisha yao. Anasema mafunzo hayo pia yalishatolewa kwa wasichana 30 manusura wa kukeketwa. Fatma anafafanua: "Wasichana walionusulika kukeketwa walifundishwa kupambana, kilimo na ufundi wa kushona nguo."

Wito wa Fatma ni kwamba, wazazi na watoto wanaoishi katika mazingira magumu wajitokeze kupatiwe elimu itakayokuwa mkombozi kwao.

Mkurugenzi wa kampuni ya CSI, Upendo Invocaviti, ambao ndio walifadhili mafunzo hayo, anaeleza historia yao kwamba kampuni ilianzishwa mwaka 2011, lengo ni kuleta usawa kwa jamii inayowazunguka..

Anasema, changamoto ya mabinti wanaioshi katika mazingira magumu, kwa kukosa elimu na waliamua kuandaa mafunzo ya kuwasaidia watoto walio katika mazingira magumu wajiendeleze katika ujasiriamali, utakaowainua kiuchumi.

**DIWANI KIPUNGUNI**

Diwani Kata ya Kipunguni, Mohamed Msofe, anasema kwamba kituo hicho ni mkombozi kwa watoto waishio katika mazingira magumu na kimekuwa chachu katika maendeleo ya kundi hilo.

Anasema, jamii inapaswa kuchangamkia fursa pale wanaposikia kuna nafasi bure kwa ajili ya kuwasaidia watoto walio na mazingira mabaya.

Msofe anaeleza kwamba, wanaokuwa na changamoto za kimaisha, inapotokea wakiwezeshwa wanaweza kuleta mabadiliko ya kiuchumi katika maeneo yao wanayoishi.

Kwa mujibu wa diwani huyo, Kipunguni mpaka sasa ina wakazi zaidi ya 50,000 wanaojishughulisha na biashara kubwa na biashara ndogo, ikiwamo shughuli za mboga ambazo ni maarufu katika eneo hilo.

**MNUFAIKA**

Tatu Gasana, ni mmoja wa wanufaika wa mafunzo hayo anasema kuwa, yeye alimaliza Elimu ya Msingi mwaka Jana, lakini wazazi wake hawakuwa na uwezo wa kumwendeleza kielimu.

Anasema aliposikia tangazo la ujasiriamali hasa mafunzo kutolewa bure, alijisajili ili yamsaidie katika maisha yake. Amina Ramadhan, mmoja wa mnufaika wa mafunzo hayo, anasema kuwa, mafunzo hayo yatamsaidia katika maisha yake pale atakapopata ujuzi.





Spika wa Bunge, Job Ndugai (katikati), akimsikiliza bwana nyuki, Ramia Konyo, wakati alipotembelea kiwanda cha asali kilichopo wilayani Manyoni, mkoani Singida jana, akiwa katika ziara ya kikazi ya siku moja. **PICHA: BUNGE**

# Vijana 200 wanufaika na fursa za uchumi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ZAIDI ya vijana 200 mkoani Mbeya wamenufaika na fursa mbalimbali za kiuchumi ambazo zinatolewa na Shirika Lisilokuwa la Kiserikali la Elimisha linalosaidia juhudi za serikali katika nyanja za utafiti, ushawishi na utetezi, kujenga uwezo na kuelimisha jamii kwa mwaka 2018/2019.

Hayo yalisemwa jana na Mratibu wa Elimisha, Debora Mwanyanje, alipokuwa akizungumza na Nipashe wanavyowawezesha vijana kutumia fursa zilizopo ikiwa ni Maadhimisho ya Siku ya Vijana Duniani. Mwanyanje alisema shirika hilo limekuwa likifanya kazi karibu na vijana kwa kuwawezesha na kuwafundisha kutumia fursa za kiuchumi zinazowazunguka.

Alisema miongoni mwa mambo waliyowasaidia vijana ni kuwapa mafunzo ya upangaji bajeti zenye mlengo wa kijinsia, ujasiriamali, uwekaji akiba na ushauri wa kibiashara. "Kwetu sisi siku hii ya vijana ina muhimu kwa sababu tumekuwa tukifanya kazi kwa karibu na kundi hilo ili kuwatoa kwenye utegemezi na kujiajiri kwa kufanya shughuli za kuwaingizia kipato," alisema Mwanyanje. Alisema kwa kutambua umuhimu wa kundi la vijana, wamehakikisha wote waliopata mafunzo ya ujasiriamali na upangaji bajeti, waanzisha biashara lakini pia kuwa na matumizi mazuri ya fedha wanazozipata ili watimize malengo yao.

Baadhi ya vijana walionufaika na fursa za kiuchumi kupitia shirika hilo, Joyce Nsolo, kutoka Iyawala, alisema mafunzo ya upangaji bajeti yamemsaidia kuwa na nidhamu ya fedha kwa kupunguza baadhi ya mahitaji yasiyo ya lazima na kumsaidia kufanya maendeleo.

Nsolo alisema elimu ya upangaji bajeti kwa vijana ni muhimu ili kutimiza malengo yao badala ya kutumia fedha vibaya ikiwamo unywaji wa pombe kupita kiasi na kushindwa kutimiza ndoto zao.

# Viziwi wapewa elimu ya ujasiriamali

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limeendesha mafunzo ya ujasiriamali kwa watu wenye matatizo ya kusikia (viziwi) zaidi ya 40 Mkoa wa Mbeya lengo likiwa ni kuliwezesha kundi hilo kuzalisha bidhaa zenye ubora na viwango vinavyotakiwa ili kumudu soko la ushindani.

Msimamizi wa TBS, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Abel Mwakasonda, aliyasema hayo jana wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo ya ujasiriamali.

Alisema waliamua kutoa elimu ya ujasiriamali kwa viziwi kwa sababu ni kundi ambalo lilisahaulika na kwamba mafunzo hayo yatawasaidia kuzalisha bidhaa nzuri ambazo zitauzika ndani na nje ya nchi.

Mwakasonda alisema katika kuelekea kwenye uchumi wa kati na ujenzi wa viwanda, ni muhimu makundi yote kushirikishwa, hivyo watu wenye matatizo ya kusikia kama sehemu ya jamii wanapaswa kupewa mbinu mbalimbali za uzalishaji ikiwa ni pamoja na kuzingatia ubora wa bidhaa.

"Mafunzo haya ni muhimu kwenu kwa sababu baadhi yenu tayari mnajihusisha na shughuli za ujasiriamali, elimu hii itawasaidia kuongeza matumizi ya viwango na uthibiti ubora kupitia biashara, viwanda na huduma kwa lengo la kuchangia juhudi za kitaifa za kuzalisha bidhaa na huduma bora na zenye uwezo wa kushindana katika soko la dunia," alisema Mwakasonda. Akimwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Mwakasonda alisema shirika linathamini mchango wa uzalishaji bidhaa zenye viwango kupitia kundi la viziwi na kwamba elimu ya ujasiriamali watakayoipata itasaidia kuongeza ujuzi na maarifa wa kutengeneza bidhaa zitakazouzika kimataifa.

Mgeni rasmi katika ufunguzi wa mafunzo hayo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Mbeya, Hassan Mkwawa, akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alipongeza TBS kwa kutambua umuhimu wa viziwi kupata fursa ya kujifunza ujasiriamali.

Alisema kwa kutambua umuhimu wa makundi maalum, serikali ilipitisha sheria inayozitaka halmashauri zote nchini kutenga asilimia mbili ya mikopo kuwapatia walemavu ili wafanye shughuli zao za ujasiriamali.

Mkwawa alisema katika kuboresha utoaji wa mikopo hiyo wameleta utaratibu mpya ambao unakitaka kikundi kilichokuwa na sifa ya kupata mkopo kununua mashine ambazo watazitumia kwenye uzalishaji badala ya kupewa fedha ambazo wakati mwingine wanazitumia kinyume na malengo yaliyokusudiwa.

Miongoni mwa viziwi walioshiriki mafunzo hayo, Suzan Magoyo, kutoka Ubaruku wilayani Mbarali, alisema mafunzo hayo yamemsaidia kujua namna ya kufanya biashara ndogo ndogo, kilimo cha mboga, uuzaji wa bidhaa na uwekezaji mdogo wa kununua mpunga.

# Barabara kujengwa kwenda Ziwa Ngozi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Kanda ya Mbeya, umeahidi kuboresha miundombinu ya barabara kwenda kwenye kivutio cha utalii cha Ziwa Ngozi ili kufungua fursa mbalimbali za kiuchumi.

Meneja wa TFS Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Ebrantino Mgiye, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea kivutio hicho.

Mgiye alisema wako kwenye mchakato wa kukusanya fedha kwa kushirikiana na wadau wengine wa utalii ili kutengeneza miundombinu ya barabara kuelekea kwenye kivutio cha Ziwa Ngozi.

"Hivi karibuni Ziwa Ngozi limekuwa kivutio kutokana na mwonekano wake mithili ya ramani ya Afrika, njia zinazotumika kufikia ziwa hilo ni za kuvutia na kusisimua kwani zimejaa milima na miteremko, hali ya hewa lakini pia maji yaliyopo ndani ya ziwa hilo kitu ambacho kimesababisha kuvutia watalii wengi," alisema Mgiye.

Mgiye alisema Ziwa Ngozi kuwa na miundombinu ya kuridhisha hasa barabara litawezesha watalii wanatembelea kivutio hicho kwa lengo la kujionea uzuri na maajabu yake.

Ziwa Ngozi ambalo liko katika safu za Milima ya Uporoto inayopakana na Wilaya za Mbeya na Rungwe lina urefu wake wa kilometa 2.5, upana kilometa 1.6 kina chake kwenda chini ni mita 74. Ziwa hilo ni pili kwa ukubwa katika maziwa yatokanayo na kreta barani Afrika.

Mdau wa utalii mkoani Mbeya, Amos Mwamugobole, alisema Ziwa Ngozi ni miongoni mwa vivutio vinavyopendwa na watalii kutokana na upekee wake ambao huwavutia.

Alisema kutokana na fursa zilizopo ndani ya ziwa hilo, wadau wa utalii akiwamo yeye, huandaa matembezi ya mara kwa mara kutembelea kivutio hicho.





# Pinda ampamba JPM utendaji safi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, ameipongeza serikali kwa kazi kubwa na ya kipekee kwenye miradi ya maendeleo, hususani sekta ya afya, maji, miundombinu na umeme.

Akizungumza wakati wa kupokea Mwenge wa Uhuru jijini Dodoma, uliopokelewa Nzinje katika kata ya Zuzu, Pinda alisema kuna kila sababu ya kumpongeza Rais John Magufuli kwa sababu utendaji wake ni wa kipekee.

Alisema amekuwa jasiri wa kuamua kufanya maendeleo bila kuhofia kitu chochote kitendo kinachomtofautisha na utendaji wa awamu nyingine.

Alisema mradi wa uzalishaji umeme (stiegler's Gorge) awali ilidaiwa utasababisha uharibifu wa mazingira kitu ambacho Rais Magufuli amethubutu kukipuuza na kuanza kutekeleza mradi.

"Kwa kweli Rais Magufuli anastahili pongezi katika ujenzi wa miundombinu kwa ujumla hata wale wanaopinga baadhi ya mambo wanapaswa kumpongeza," alisema Pinda.

Kuhusu ununuzi wa ndege, alisema awali katika mitandao ya kijamii baadhi ya watu walionekana wakimlaumu ya kuwa zinalitia hasara taifa ili hali kipindi kile ilikuwa ni majaribio.

Alisema hivi sasa ndege hizo zinafanya safari mara mbili kwa siku na abiria wanapanda kwa wingi jambo ambalo linaingiza faida kubwa ikiwamo kuchangia kuongeza uchumi wa nchi kupitia mapato yanayopatikana.

"Tujifunze kuweka akiba ya maneno natamani hivi sasa niwaulize, waliokuwa wakitoa lawama hizo, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni," alisema Pinda.

Aliongeza kuwa kwenye miundombinu ya barabara serikali imeipa kipaumbele kutokana na kwamba barabara nyingi zimeboreshwa jijini Dodoma na maeneo mengine jambo ambalo limesaidia kurahisisha utendaji kazi wa wananchi kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

Awali, akisoma taarifa ya mradi wa ufugaji samaki wa Pinda Farm, mke wa Waziri Mkuu mstaafu, Tunu Pinda alisema ufugaji samaki shambani kwao Pinda Products Farm, alisema ni miongoni mwa miradi michache ya ufugaji samaki iliopo jijini hapa.

Alisema mradi huo umegharimu Sh. milioni 29 kujenga mabwawa saba, yakiwamo madogo sita na kubwa moja ambayo yanazalisha sato na kambale.

Alisema changamoto zinazowakabili katika mradi huo ni pamoja na upatikanaji wa chakula cha samaki cha uhakika kwa bei nafuu hapa nchini, ambapo chakula hicho kinatengenezwa nje ya nchi ikiwamo kuuzwa kwa gharama kubwa ikichangiwa na usafirishaji.

Alisema kutokana na hilo wananchi wa kata ya Zuzu wameiomba serikali isaidie wafugaji wa samaki kupata elimu ya kutosha kuhusu uwekezaji huo.

Kwa upande wake, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, vijana Ajira, Anthony Mavunde, alimpongeza Pinda kwa kazi nzuri ya ufugaji anayofanya na kwamba amesaidia kuongeza ajira kwa vijana wa eneo hilo.

"Nakupongeza sana mstaafu kwa kusaidia kuongeza ajira kwa vijana nami kama mbunge na waziri nitaendelea kuhimiza upatikanaji wa Umeme Vijijini -Rea," alisema Mavunde.

Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Mzee Mkongea Ally, alisema mradi huo ni darasa kwa wakazi wa eneo hilo na jamii kwa ujumla kwa sababu wengi wanapita kujifunza kupitia shamba hilo.



Mtendaji wa Shirika la Maendeleo la Vijana Kibaha (YPC), Israel Irunde, akitoa mada kwenye mkutano wa wadau wa demokrasia, uongozi na ushiriki wa vijana katika mchakato wa siasa nchini, uliofanyika jijini Dodoma juzi. **PICHA: PAULO MABEJA**

# Wakumbushwa fursa za zabibu SADC

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKULIMA wa zabibu na wasindika mvinyo wametakiwa kutumia fursa ya Tanzania kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), kujipatia soko la uhakika la bidhaa hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Jumuiya ya Wafanyabiashara, wenye viwanda na kilimo Tanzania (TCCIA) Mkoa wa Dodoma, Idd Senge, alisema wakati alipokuwa akizungumza na wanahabari.

Alikuwa akizindua jukwaa la wadau wa zabibu jijini Dodoma.

Tanzania inazalisha zabibu kwa wingi katika jumuiya ya SADC hivyo, ni fursa kwa wakulima pamoja na wasindikaji wa mvinyo kujipatia soko la uhakika la zao hilo.

Senge, alisema zipo nchi nyingi katika jumuiya hiyo ambazo hazilimi kabisa zabibu hivyo wakulima wakichangamkia fursa hiyo kwa kutafuta masoko katika nchi hizo watakuwa wametibu shida ya ukosefu wa soko. "Katika jumuiya hii nchi ambayo inalima kwa wingi ikiondoa Tanzania ni Afrika Kusini, lakini zipo nyingine ambazo hazilimi kabisa hivyo sisi tutatumia fursa hii kupata soko kuuza mvinyo au kusafirisha juisi ya zabibu," alisema Senge.

"Hivi sasa zabibu nyingi zinaozea mashambani kutokana na kukosa soko kwa vile wazalishaji ni wachache, hivyo kuelemewa na kile wanachozalisha wakulima," alisema Senge.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, Patrobas Katambi, akizungumza wakati wa uzinduzi wa jukwaa hilo la wadau wa zabibu alisema kuwa vijana wanatakiwa kubadili mitazamo yao na kuingia katika kilimo cha zabibu ambacho kitaweza kuwakwamua kiuchumi.

"Katika mataifa makubwa kama Marekani wakulima ndiyo watu wenye fedha kuliko makundi mengine, lakini huku kwetu vijana wanaona kilimo kama kazi ya wazee, hali ambayo siyo kweli kwani kilimo kinaweza kuwatoa vijana kuliko kitu kingine," alisema.

"Kama kijana ataingia katika kilimo cha zabibu basi kinaweza kumkomboa kwa sababu zabibu ukilima leo unavuna mfululizo ndani ya miaka zaidi ya 60, hivyo hata watoto wako hadi wajukuu wanaweza kufaidika nayo harafu sasa kwa neema za mungu hapa kwetu tunavuna mara mbili kwa mwaka tofauti na maeneo mengine duniani," alisema Katambi.

Mkurugenzi wa Baraza la Kilimo, Timoth Mbaga, alisema lengo la kuanzisha jukwaa hilo ni kusaidia kuinua zao hilo la zabibu ambalo kama litasimamiwa linaweza kuitangaza Tanzania kimataifa.

## Mwenge waagiza kufanywe ukarabati

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KIONGOZI wa mbio za Mwenge Mzee Mkongea Ally, ameagiza Halmashauri ya Jiji la Dodoma, kukarabati chumba cha kuhifadhi miili cha kituo cha afya Makole pamoja na kuziba nyufa katika baadhi ya majengo ya kituo hicho.

Pia, aliwataka kusimamia maboresho ya ukarabati wa majengo ya zamani katika vituo vya afya ili wananchi waweze kuhudumiwa kikamilifu.

Agizo hilo lilitolewa juzi na kiongozi huyo wa mbio za Mwenge kitaifa wakati akitembelea miradi ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma, zinazoendelea.

Ally aliitaka halmashauri hiyo kufuatilia maboresho hayo lengo ni kutekeleza agizo la serikali la kuboresha sekta ya afya kulingana na fedha zilizotolewa katika ujenzi wa vituo mbalimbali vya afya nchini.

"Naomba halmashauri kwa ujumla simamieni suala hili tunahitaji kuona vituo vya afya vya jiji la Dodoma vina ubora unaostahili," alisema Ally.

Katika kituo cha Mkonze, kiongozi huyo alisema halmashauri inapaswa kuhakikisha mkandarasi anafanya kazi na kutumia nondo zinazotakiwa.

Awali, akisoma taarifa ya kituo hicho, Kaimu Mganga Mkuu, Dk. Joseph Mdachi, alisema kituo hicho ni moja ya vituo vinne vya afya jijini Dodoma ambavyo vipo katika idadi ya uongezaji wa majengo ikiwamo ukarabati wa zamani.

Alisema lengo la mradi huo ni kuongeza majengo katika kituo hicho pamoja na ukarabati wa majengo ya zamani ikiwamo kuweka mazingira bora ya utendaji wa watumishi jambo linaendelea kufanyika.

Alisema mradi huo umegharimu Sh. milioni 500 kwa ujenzi wa majengo matano na pia kiasi cha Shilingi milioni 72.6 ni kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya zamani.





# PBZ yawezesha hospitali vifaa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BENKI ya Watu wa Zanzibar (PBZ), imekabidhi msaada wa vifaa mbalimbali zikiwamo mashine za kuangalia vichochezi vya mwili (hormones) kwa watoto, kwa uongozi wa Wizara ya Afya Zanzibar.

Akikabidhi msaada huo katika Hospitali Kuu ya Mnazimmoja, Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Khadija Shamte, alisema PBZ ni benki ya watu, hivyo ina haki ya kusaidia masuala mbalimbali yanayowagusa wananchi.

Alisema sekta ya afya ni sekta muhimu katika maendeleo ya nchi na bila afya hakuna nguvu kazi iliyo bora.

Shamte alisema afya ni sekta muhimu katika maendeleo ya nchi na inahitaji mambo mengi, hivyo aliwaomba wadau wengine kuendelea kutoa misaada na vifaa mbalimbali kuisaidia sekta hiyo ambayo inasaidia watu hasa wanyonge.

"Sekta hii ni muhimu sana katika kuboresha afya za wananchi na kurudisha nguvu kazi kwani bila ya afya hakuna kitu kinachoweza kufanyika," alisema.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Zanzibar, Halima Maulid Salum, alipongeza PBZ kwa kuendelea kuwajali na kila mara kuendelea kuikumbuka jamii hasa Wizara ya Afya ambayo ni sekta muhimu ya maisha ya watu.

Alisema PBZ inaonyesha uzalendo ambao aliouweka Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohammed Shein, ambaye ameipa kipaumbele sekta hiyo na kujitahidi kutoa huduma zote kuhakikisha kwamba huduma zote za afya ikiwamo vifaa tiba na dawa, zinapatikana pale wananchi wanapokwenda hospitali.

Alisema vifaa hivyo vitapelekwa katika hospitali zote za wilaya na mikoa za Unguja kwa kuwa ndiyo mahitaji makubwa ambayo yako katika hospitali hizo hasa za vijijini.

Kutokana na hali hiyo, aliwaomba madaktari kuvitunza vifaa hivyo, ili viweze kudumu kwa muda mrefu na kuhudumia wagonjwa ambao watafika kupata matibabu katika hospitali za serikali.

"Tuvitunze vitu hivi ili wengi wapate kuvitumia na vitunufaishe sote na sio kuviharibu kwa makusudi hili si lengo la watu wanaotusaidia," alisema.

PBZ ilikabidhi mashine mbili magodoro 50, vitanda 50 na mashuka 50 ambavyo vitu vyote hivyo vimegharimu zaidi ya Sh. milioni 85.

# Waziri apigia debe utalii wa majahazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Mahmoud Thabit Kombo, amesema utalii wa majahazi ni kivutio kikubwa cha watalii licha ya kwamba Zanzibar inapokea watalii wengi wanaosafiri kwa kutumia ndege.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza katika hafla ya kumuaga Nassir Salum Mabrouk ambaye atashiriki tamasha la safari ndefu duniani kwa kutumia usafiri wa boti katika kutembea dunia nzima kupitia baharini.

Alimtaka mshiriki huyo ambaye ni pekee kwa nchi za Afrika Mashariki kuitangaza Zanzibar kiutalii kupitia mashindano hayo.

Kombo alisema iko haja sasa ya kukuza utalii wa bahari ili watalii wanaofika Zanzibar watumie usafiri wa baharini.

"Nikupongeze sana kwa ujasiri wako maana huko unakwenda katika safari ndefu ambayo utatumia boti ambayo haina mashine," alisema waziri huyo.

Akizungumza katika hafla hiyo, Nassir alisema anatumaini atarudi na ushindi mzuri na ataitangaza Zanzibar kimataifa kupitia mashindano hayo.

Alisema mashindano hayo ya tamasha la safari ndefu duniani, anatumia boti ambayo haitumii mashine na badala yake itakua inategemea upepo na watazunguka mabara sita.

"Tunategemea kuanza safari Septemba, mwaka huu na kumalizia Agosti, mwakani na tutaanzia London (Uingereza), Ureno, Uruguay, Cape Town (Afrika Kusini), Australia, China, New York (Marekani), Bermuda, Ireland na kurejea London," alisema.

Aidha, alisema nchi 11 zitashiriki katika tamasha hilo na kwa Afrika Mashariki yeye ni mshiriki pekee.

Nassir alisema ana uzoefu wa kutembea na majahazi masafa marefu na amekuwa akitoka Unguja hadi Pemba kwa kutumia usafiri wa jahazi akiwa baharini na kwamba jahazi hilo linategemea upepo pekee.

"Sijawahi kusafiri kwenda Pemba kwa kutumia boti au ndege. Naondoka kwa kutumia jahazi ambalo linatumia upepo pia nimeshasafiri kwa kutumia jahazi kutoka Zanzibar hadi Madagascar tena nakwenda na kurudi salama," alisema.

Alisema usafiri wa baharini ni mzuri licha ya kwamba una changomoto nyingi lakini unamjengea ujasiri na ustahamilivu.

Hata hivyo, alisema changamoto kubwa iliyopo katika usafiri wa majahazi ni pale linapokatika tanga na kupoteza mwelekeo wa safari na upepo hukupeleka popote hivyo inabidi uvumilivu.




Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Mahmoud Thabit Kombo (kulia), akimkabidhi bendera ya Tanzania mshiriki wa tamasha la safari ndefu duniani kwa kutumia boti litakalofanyika London, Uingereza mwezi ujao, katika hafla iliyofanyika mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Taasisi yaahidi kulea watoto yatima

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TAASISI ya Pondeza Foundation Zanzibar (TPFZ) imesema utaratibu wa kusaidia yatima katika Jimbo la Chumbuni katika sekta ya elimu na kula chakula cha pamoja utakuwa wa kudumu na kufanyika kila mwaka.

Msimamo huo ulitolewa juzi na Mwenyekiti wa Taasisi hiyo, Ussi Salum Pondeza, alipokuwa akizungumza katika hafla ya chakula cha pamoja ilioshirikisha watoto yatima 503 huko Maruhubi, mjini Zanzibar.

"Utaribu wa kusaidia yatima utakuwa wakudumu lengo kubwa kuwainua kielimu pamoja na kuwakutanisha pamoja kula chakula kila mwaka hasa wakati wa sikukuu," alisema Pondeza ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Chumbuni.

Alisema watoto yatima wana haki sawa na watoto wengine kwa mujibu wa katiba ikiwamo ya kupata elimu na kuhifadhiwa kutokana na mazingira magumu yanayowakabili baada ya kuondokewa na wazazi au walezi wao.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili kupongezwa kwa kuhakikisha watoto wote waliofikisha umri wa kusoma wanapata haki hiyo wakiwamo watoto yatima visiwani Zanzibar. Awali, mgeni rasmi katika hafla hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Ayoub Mahmoud Mohamed, alisema ni jambo la faraja kuona taasisi za kiraia zinaendelea kusaidia watoto yatima mahitaji yao.

Mkuu wa Mkoa alisema kutokana na kuguswa na shughuli ya chakula ya yatima 503, taasisi yake ya Mimi na Wewe iko tayari kushirikiana kuandaa shughuli kama hiyo mwakani kwa watoto yatima.

"Serikali toka katika awamu ya kwanza imekuwa na utaratibu wa kuwatunza watoto yatima ikiwamo kujenga nyumba za kulelea watoto yatima Zanzibar," alisema.

Alisema watoto yatima wanapaswa kupatiwa mahitaji muhimu kama kuthaminiwa, upendo, elimu, afya, chakula bora, mavazi na kushirikiana nao katika mikusanyiko ya shughuli za kijamii kama sikukuu.

# Wananchi wapaza sauti kwa serikali kilio cha maji

**Na Elizabeth Faustine,**
MWANZA

WANANCHI wa Kata ya Kisesa na Bujora Wilaya ya Magu mkoani Mwanza, wameonyesha kusikitishwa na ahadi ya kupatiwa maji wanazopewa kila wakati bila kutimizwa.

Wakizungumza katika mkutano wa hadhara uliofanyika uwanja wa Mkapa Kisesa, wananchi hao walitoa kilio chao mbele ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Prof. Kitila Mkumbo, wakieleza adha ya kukosekana kwa maji kunakosababisha majanga kwa wanawake kubakwa, watoto kuungua kwa moto na hatimaye kukutwa na umauti.

Wananchi hao wakiwa katika mkutano huo uliohudhuriwa na viongozi mbalimbali, wengi wao waliitikia salamu ya viongozi hao kwa kuitikia 'majiiiii', huku baadhi yao waliopewa nafasi ya kusema wakieleza changamoto wanazokutana nazo kwa kukosa maji.

Tereza Andrew, alisema Kisesa maji yanatoka mara moja kwa mwezi na ndoo wanauziwa Sh. 500, na kwamba mara ya mwisho kuona maji yakitoka katika bomba lake ni Mei, hivyo mpaka sasa limepata kutu.

"Malalamiko yetu makubwa ni maji, tunaamka usiku wa manane, kinamama tunasomesha watoto kwa ajili ya mboga, sasa hivi watoto hawaendi kwa sababu biashara haiendi... watoto wanakosa mahitaji, kama shida ni hawa watendaji ambao wanamkwamisha Rais basi watolewe," alisema Tereza Andrea.

Sara Masalu alisema suala la maji kwao imekuwa kero wanaamka saa nane usiku, huku ndoo wakiuziwa Sh. 200, na wakati mwingine wanayakosa, ikizingatiwa wao ni wafanyabiashara hali inayopelekea biashara kutofanyika vizuri kwani muda mwingi wanatumia kutafuta maji, hivyo watoto kuumia kwa kukosa mahitaji.

Evaristina Mahela alisema watoto wadogo wanakumbwa na umauti kutokana na wamama kuamka usiku kwenda kutafuta maji, huku wakiacha kibatari kikiwaka matokeo yake kinashika neti na moto unawaka.

"Mama anaamka asubuhi kwenda kutafuta maji anaacha watoto ndani wamelala, hukuA kibatari kikiwaka, matokeo yake moto wa kibatari unashika neti watoto wanaungua hatimaye maafa, mama naye huko njiani anabakwa kwa kweli hili naomba mliangalie, mabomba yameota kutu," alisema Mahela.

Mbunge wa Magu, Boniventura Kiswaga, alisema, changamoto ya wananchi wa Kisesa na Bujora ni maji hivyo mwarobaini wa kuitatua ni mradi wa euro milioni 30, huku akitumia fursa hiyo, kumwomba Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji kujengwa tangi kubwa la maji katika eneo hilo ili kumaliza shida ya maji.

Akijibu kilio hico, Prof. Mkumbo, alisema, alisema watendaji hawatoi ahadi bali majibu, hivyo hatua wanazochukua kutatua changamoto ya maji Kisesa ni kupanua mtandao wa maji utakaoendana na mahitaji ya sasa na miaka ijayo.

"Nyamohongolo nimepita nimeona wameanza kutandaza mabomba, hivyo nawaagiza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Mwanza (Mwauwasa) kuhakikisha mradi huu unakamilika kwa siku 90 kuanzia Agosti 15 hadi Novemba 15, mwaka huu, ili wananchi wa Kisesa na Bujora waweze kupata maji, lakini wanawake waondokane na adha walizokuwa wanazipata, alisema Prof. Mkumbo.

"Ni kweli mnahitaji matangi kwa ajili ya kutunzia na kuteremsha maji, hivyo pia nimeagiza mradi wa ujenzi wa tangi kubwa uanze na ukamilike ndani ya miezi sita(6), hivyo miradi yote ikikamilika wananchi wanatakiwa kuuziwa maji kwa Sh. 50 kwa ndoo, tukirudi hapa mwezi Novemba na Desemba wapige ngoma za kutushukuru," alisema Prof. Mkumbo.



Mafundi wa Shirika la Ugavi Umeme Tanzania (Tanesco), wakitengeneza transfoma iliyopata hitilafu katika eneo la Tandale kwa Mtogole, Manispaa ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Tanapa yasaidia majeruhi ajali Moro

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) limetoa msaada wa Sh. milioni 10 kusaidia majeruhi waliopata ajali ya moto eneo la Itigi Msamvu mkoani Morogoro wiki iliyopita.

Alizungumza kwenye Hospitali ya Rufani mkoani Morogoro, Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa, Donatus Bayona, huku akikabidhi hundi ya fedha hizo, alisema, Tanapa wameguswa na janga hilo lililowakumba Watanzania wenzao kwani wamekuwa wakishirikiana na jamii katika matukio mbalimbali yakiwamo sherehe na maafa.

Akipokea msaada huo Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Kebwe Stephen Kebwe, alishukuru Tanapa kwa msaada mkubwa waliotoa utakaoweza kusaidia majeruhi wa ajali hiyo waliopo kwenye hospitali hiyo.

Aidha, Dk. Kebwe, alisema wanakabiliwa na changamoto ya kukosekana kwa vifaa mbalimbali kama monita za kuangalia hali ya mapigo ya moyo inakwendaje, msukumo wa damu na hewa ya oxygeni ikoje kwenye mwili na vifaa vingine vya kusaidia mgonjwa kupumua.

Dk. Kebwe alisema wanatarajia fedha hizo zinazotolewa na wadau kuzielekeza kwenye ununuzi wa vifaa hivyo vya kusaidia wagonjwa.

Alisema, hapo baadaye kupitia bajeti za serikali na mapato mengine ya hospitali, wataangalia namna ya kuimarisha chumba cha kuangalia wagonjwa mahututi na watokanao na ajali.

# Ataka mafanikio ya JPM yapongezwe kwa ushindi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MJUMBE wa Halmashauri Kuu Taifa ya CCM (NEC) mkoani Shinyanga, Gaspal Kileo, ametoa maagizo kwa Umoja wa Wazazi CCM mkoani humo, kuhakikisha wagombea wote wa chama hicho kwenye uchuguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu mwakani, wanashinda viti vyote.

Alisema kutoa tamko la kumpongeza Rais John Magufuli kuhusu utendaji kazi wake haitoshi, bali zawadi pekee ambayo anapaswa kupatiwa ni kumpa ushindi wa kishindo kwa kushinda viti vyote kwenye uchaguzi na wapinzani waweze kupata ziro.

Kileo alizungumza hayo juzi alipokuwa mgeni rasmi kwenye kongamano la Umoja wa Wazazi CCM mkoani Shinyanga, wakati wa kutoa tamko la kumpongeza Rais Magufuli kwa kutekeleza ipasavyo ilani ya uchaguzi ya CCM kwa asilimia 100 ndani ya utawala wake kwa miaka minne.

Alisema pongezi hizo si chochote kama hawatampatia Rais Magufuli ushindi wa kishindo kwenye chaguzi zote na hiyo ndiyo zawadi pekee anayopaswa kupewa ili aweze kupata wasaidizi wazuri wa kuendelea kuchapa nao kazi na kuwaletea maendeleo Watanzania.

"Tusiwe tunaishia kumpongeza tu Rais John Magufuli, bali tuwe tunaiga na yale ambayo anayafanya ya kupinga vitendo vya rushwa, ufisadi, utovu wa nidhamu kazini, ukwepaji wa kodi, pamoja na kufuata mambo yote mazuri ambayo amekuwa akiyatenda hapa nchini hapo ndipo tutakuwa tuna mpongeza sasa," alisema Kileo.

"Pia pale mtakapokuwa mnapitisha wagombea wa CCM kwenye kura za maoni hakikisheni mnachagua watu wazuri, wenye maadili, waaminifu na wachapakazi, ambao wataendana na kasi ya serikali ya awamu ya tano hapo ndipo tutamtendea haki Rais wetu Magufuli," aliongeza.

Awali Katibu wa Umoja wa Wazazi CCM Mkoa wa Shinyanga, Masanja Salu, akisoma tamko kwa niaba ya umoja huo, alisema wanampongeza Rais Magufuli kwa kutekeleza ilani ya CCM, kwa kutetea haki za wanyonge pamoja na kuiletea nchi mafanikio ya kimaendeleo.

Alisema ndani ya utawala wake wa miaka minne amefanya maajabu nchini kwa kudhibiti mafisadi, rushwa, mishahara hewa, utoroshwaji wa madini, makinikia, upotevu wa mapato, katoa pia elimu bure, ujenzi wa madaraja, miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege, reli, huduma za kiafya, na ununuaji wa ndege.

# Marekani yaomba meli kuzuiliwa

**WASHINGTON, Marekani**

IDARA ya haki nchini Marekani imewasilisha ombi la dakika za mwisho kwa mamlaka nchini Gibraltar kuzuiwa kuachiliwa kwa meli kubwa ya mafuta ya Iran.

Meli hiyo yenye jina Grace 1 iliyokuwa ikibeba mafuta ilikamatwa na wanamaji wa Uingereza Julai 4 , mwaka huu hatua iliyosababisha mgogoro na Iran.

Meli hiyo ilikuwa inakaribia kuachiliwa, baada ya mkuu wa sheria nchini Gibraltar kusema kuwa hakutakuwa na agizo jingine la zaidi kuizuia.

Lakini Marekani iliomba taifa hilo kufikiria tena huku kesi yake ikitarajiwa kusikilizwa saa tisa kwa mujibu wa saa za Uingereza.Gibraltar ilisema kuwa ombi hilo la Marekani linatokana na baadhi ya madai ambayo yanaangaliwa kwa sasa.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Uingereza ilisema kuwa haiwezi kuzungumza kuhusu ombi hilo la Marekani.

Mwandishi wa masuala ya dunia wa BBC, Marcus Jonathan, alisema kwamba Uingereza, imekuwa ikitumai kwamba kuachiliwa kwa Grace 1 kutasababisha kuachiliwa kwa meli inayopeperusha bendera ya Uingereza ya Stena Impero iliyokamatwa na Iran huko Ghuba.

Msemaji wa serikali ya Gibraltar pia alithibitisha kwamba uchunguzi wa polisi dhidi ya wafanyakazi wote wa nne wa meli hiyo akiwamo nahodha raia wa India umekamilika.

Mawakili wa wafanyakazi hao waliambia BBC kwamba maofisa wa polisi walisema kwamba hilo linatokana na vitendo vya serikali ya Iran na kwamba haikuwa hamu ya umma kuendelea nayo.

Meli hiyo ya mafuta ilikamatwa baada ya serikali ya Gibraltar kusema kwamba ilikuwa inaelekea Syria ikiwa ni ukiukaji wa vikwazo vya Muungano wa Ulaya.

Takriban wanamaji 30 walisafirishwa kutoka Uingereza kuelekea Gibraltar ili kuwasaidia maofisa wa polisi kuizuia meli hiyo ya mafuta na mizigo yake kufuatia ombi la serikali ya Gibraltar.

Kukamatwa kwa meli hiyo kulizua mgogoro wa kidiplomasia kati ya Uingereza na Iran ambao umeongezeka katika wiki za hivi karibuni.

**BBC**

# Ndege yagonga kundi la ndege

**MOSCOW, Urusi**

NDEGE ya abiria ya Urusi imelazimika kutua kwa dharura kwenye shamba la mahindi karibu na jiji la Moscow baada ya kugonga kundi la ndege.

Watu 23 wamejeruhiwa katika tukio hilo, ambalo lilisababisha ndege kutua huku injini yake ikiwa imezima na gia yake ya kutua ikirudi nyuma, walisema maofisa wa afya.

Ndege hiyo Ural Airlines, Airbus 321 ilikuwa ikisafiri kuelekea katika eneo la Simferopol Crimea ilipogonga kundi la ndege muda mfupi baada ya kuondoka uwanjani , hali iliyovuruga utendaji wa injini yake.

Vyombo vya habari vya Urusi vimetaja kutua kwa ndege hiyo kama "muujiza wa eneo la Ramensk".

Maofisa wa ndege hiyo walisema ndege imeharibika sana na haiwezi kupaa tena. Uchunguzi rasmi juu ya ajali hiyo unaendelea.

Ndege hiyo ilikuwa na abiria 233 wahudumu waliporipotiwa kuwa ndege iliingia ndani ya injini na rubani wake akaamua kutua mara moja.

Abiria mmoja ambaye hakutajwa jina lake aliiambia televisheni ya taifa kuwa ndege ilianza kuyumba kwa hali ilisiyo ya kawaida baada ya kuondoka uwanjani.

"Sekunde tano baadaye, taa za upande wa kulia za ndege zikaanza kuwaka na kuzima na kulikuwa na harufu ya kuungua, halafu tukatua na kila mtu akatimua mbio kwenda mbali," alisema.

Shirika la usafiri wa ndege la Rosaviatsia limesema kuwa ndege hiyo ilitua katika shamba la mahindi kilomita moja kutoka kwenye njia yake kwenye uwanja wa kimataifa Zhukovsky, huku injini yake ikiwa imezima na breki zake za kutua zikiwa zimerudi nyuma.

Wasafiri walitolewa kutoka kwenye ndege, huku baadhi wakipelekwa hospitalini kwa matibabu na wengine wakiongozwa kuelekea kwenye uwanja wa ndege.

Wizara ya Afya ilisema: "Watoto watano walikuwa miongoni mwa wasafiri waliolazwa kufuatia ajali hiyo. Wale waliojeruhiwa katika mkasa huo walichukuliwa kama watu wenye "hali mbaya na hali ya kawaida."

Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya ndege ya Ural Airlines, Kirill Skuratov, aliwaambia waandishi wa habari kuwa wasafiri walitaka kuendelea na safari yao watawekwa kwenye ndege mbadala baada ya kufanyiwa uchunguzi wa kimatibabu.

Vyombo vya habari vya Urusi vimelinganisha tukio hilo na tukio la safari ya ndege ya Marekani-US Airways iliyolazimika kutua kwa dharura katika mto Hudson muda mfupi baada ya kupaa mnamo mwaka 2009.

Migongano baina ya ndege na ndege ni jambo la kawaida katika safari za anga , huku maelfu ya ajali hizo zikitokea nchini Marekani pekee. Hata hivyo, ni nadra kusababisha ajali au kusababisha uharibifu kwenye ndege

***BBC***



Ndege yenye abiria 233 ikiwa ndani ya shamba baada ya kutua kwa dharura. **PICHA: EPA.**

# Museveni awaambia vijana waache anasa

**KAMPALA , Uganda**

RAIS Yoweri Museveni wa Uganda, amewataka vijana kufuata na kulinda utamaduni wa Kiafrika na sio kudanganywa na ulimwengu wa kimagharibi ambao ameuelezea kama "unaoumwa", limeripoti gazeti la Daily Monitor nchini humo.

"Nchi za magharibi hazina miwani ya kuona utofauti kati ya mwanamke na mwanamume. Ni wagonjwa.Urithi wa utamaduni wetu lazima udumishwe, lakini wengine utamaduni wetu unaofuatwa na asilimia kubwa ya watu , ubadilishwe kwa lazima ," alisema Museveni.

Rais huyo wa Uganda alitoa kauli hizi alipokuwa akikutana na wawakilishi wa vijana kutoka maeneo mbali mbali ya nchi hiyo wanaounda baraza la kitaifa la vijana- National Youth Council katika Wilaya ya Jinja Jumatano wiki hii.

Museveni aliwashauri vijana juu ya kile alichokiita "nidhamu ya jamii" kwa kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na sherehe kubwa na anasa. Alisema pia anashangazwa ni pesa gani vijana wanazimwaga kwenye baa huku wakidai hawana pesa.

"Unakwenda baa unawakuta wamejaa, ukienda wanakochoma nguruwe unakuta vijana wamejaa. Huu ni utovu wa nidhamu ya jamii na ni sehemu ya tatizo tunalokabiliana nalo " alisema Museveni.

Katika taarifa iliyotolewa na maofisa wake wa habari , Museveni alisisitizia umuhimu wa haja ya kuwa na nidhamu ya kiuchumi na akaahidi usaidizi wa serikali yake kwa vijana ambao watafungua vyama vya ushirika na kujihusisha na shughuli za uzalishaji, limeripoti gazeti la Daily Monitor.

"Vijana wanapaswa kufahamu kuwa wanapozungumza na mimi, wanapozungumza na mtu ambae zamani alikuwa kijana, wakati mmoja . Nilikuwa kijana lakini kijana asiye wa kawaida, aliyekuwa bora kuliko hata watu wazima wakati huo. Nilifundisha mabadiliko ya njia za kisasa za ukulima wakati watu wa Ankole walipokuwa wanaamini kwamba kilimo cha biashara kilikuwa ni kwa ajili ya wasomi pekee ," alisema.

Aliwashauri viongozi wa vijana kuanza wenyewe kubadilika kimawazo jambo ambalo litawasaidia kuwabadili wale walio chini ya uongozi wao .

"Hata kama itamaanisha kuwahamasisha watu kubadilika juu ya matumizi ya pesa kupitia Twitter. Ninaweza pia kutweet na ninyi ," alisema Rais Museveni.

Mkutano baina ya Museveni na vijana ni moja ya misururu ya maadhimisho ya siku ya kimataifa ya vijana.

***BBC***

# Kardinali Pengo ang'atuka, Ruwa'ichi awa mrithi rasmi

INATOKA UK.4

"Naamini katika karama ya utii, nikiwa Shemasi na umri wa miaka 26, Askofu Msakila (Sumbawanga) aliniambia nikipata upandre nitakuwa Katibu wa Jimbo, nilishtuka sana, baada ya miaka miwili nikaambiwa naenda Roma kufanya masomo ya juu, niliporudi nikafundisha Seminari Kuu ya Kipalapala mwaka 1977." Kardinali Polycarp Pengo alisema siku hiyo.

Pia alisema baadhi ya wanafunzi wake ni Askofu Mkuu, Ruwa'ichi na Askofu Rweyongeza.

"Baadaye mwaka 1978 niliitwa TEC nikaambiwa natakiwa kuwa Gombera mwanzilishi wa Seminari Kuu ya Segerea, nilipokaa hadi mwaka 1984," alieleza.

Aliongeza: "Sikuwahi kuwa kiongozi wa seminarini, ni mara moja kidogo pale seminari ndogo ya Kaengesa nilikuwa kiranja msaidizi. Lakini muda mwingi sikuwa kiongozi shuleni. Sasa sijui kwa nini Mungu alinipa kuongoza kanisa.

"Siyo mpenzi wa michezo hata kidogo, kiasi kwamba kule seminari ndogo nililazimika kucheza mpira kwa lazima ambao nilikuwa siuwezi pia, kwa sababu michezo ilikuwa lazima."

Kardinali Polycarp Pengo alinukuliwa akisema: "Siamini kama nimewahi kufanya lolote, ni Mwenyezi Mungu amefanya kupitia kwangu na wenzangu wote."

Kardinali Pengo alizaliwa Agosti 5, 1944 katika Parokia ya Mwazye, Jimbo Katoliki la Sumbawanga, aliingia seminari ya mwanzo ya Karema mwaka 1959 hadi 1964 na baadaye Seminari ya Kaengesa 1959 hadi 1964.

Alijifunza falsafa katika Seminari Kuu ya Kipalapala, Tabora mwaka 1965/67, Teolojia 1968/71 na elimu ya dini kutoka Chuo Kikuu cha Makerere, Uganda.

Juni 20, mwaka 1971 alipewa daraja takatifu ya upadri na hayati Askofu Karolo Msakila katika Parokia ya Mwazye na kuteuliwa kuwa Katibu wa Jimbo hadi Julai mwaka 1973 alipotumwa Roma kwa masomo ya juu ya Teolojia ya Maadili.

Desemba mwaka 1977 hadi 1983 alitumwa na maaskofu kuwa Gombera mwanzilishi wa Seminari Kuu ya Mtakatifu Karoli Lwanga, Segerea Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam.






# Mabula atangazia kiama maofisa ardhi

**Na Munir Shemweta,** URAMBO

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewaonya maofisa ardhi watakaoshindwa kuingiza taarifa za miliki za ardhi kwenye mifumo ya utunzaji na ukadiriaji kodi za ardhi ifikapo Oktoba, mwaka huu, watachukuliwa hatua.

Dk. Mabula alitoa onyo hilo wakati akizungumza na watendaji wa sekta ya ardhi katika Wilaya ya Urambo, ikiwa siku ya pili ya ziara yake katika mkoa wa Tabora. Alitembelea pia Wilaya ya Kaliua kuhamasisha ukusanyaji maduhuli ya serikali kupitia kodi ya ardhi na kukagua masijala ya ardhi na mfumo wa ukusanyaji kodi ya pango la ardhi.

Alisema mfumo wa utunzaji na ukadiriaji kodi za ardhi, unasaidia kujua wamiliki wa ardhi na madeni yao kwa urahisi kwa kuwa taarifa kuhusiana na miliki za ardhi sambamba na kiasi wanachodaiwa zinajulikana kwa urahisi, hivyo kuiwezesha wizara kuwa na kumbukumbu zenye uhakika.

"Wasiotimiza asilimia mia moja inapofika Oktoba, mwaka huu, nitaanza kushughulika na maofisa ardhi wasioingiza taarifa za miliki za ardhi katika mfumo. Kama ni mteule au mkuu wa idara utaondolewa," alisema.

Mabula alisema hivyo kutokana na kutoridhishwa na kasi ya uingizaji taarifa za miliki za ardhi katika mifumo ya utunzaji na ukadiriaji kodi ya ardhi kwa baadhi ya halmashauri alioueleza kuwa unachangiwa na maofisa ardhi wasiofanya kazi ipasavyo.

Naibu Waziri alitolea mfano wa Halmashauri za Kaliua na Urambo ambapo kwa upande wake, Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi Halmashauri ya Urambo, Joel Mayunga, alieleza halmashauri hiyo kuingiza viwanja 3,501 katika mfumo kati ya 4,831 huku Mkuu wa Wilaya ya Kaliua, Abel Busalama, akieleza halmashauri ya wilaya yake kuingiza viwanja 553 kati ya 1,597.

Aliwataka makamishna wasaidizi wa ardhi wa kanda zote kuhakikisha wanafuatilia maofisa ardhi katika kanda zao wanaingiza taarifa hizo za miliki za ardhi kwenye mfumo huo na Mkuu wa Idara ya Ardhi atakayeshindwa kutekeleza, hafai kuongoza idara hiyo.

Akiwa wilayani Kaliua, Dk. Mabula alikasirishwa na utaratibu mbovu wa utunzaji majalada ya ardhi unaofanywa na maofisa ardhi katika halmashauri hiyo na kufafanua kuwa utaratibu huo unachangia migogoro ya ardhi kushindwa kuisha.

Alisema utaratibu wa utunzaji majalada ya ardhi katika halmashauri ya Kaliua hauzingatii taratibu ikiwamo baadhi ya majalada kukosa maelekezo kutoka kwa ofisa mmoja kwenda kwa mwingine na badala yake jalada moja kuwa na majalada zaidi ya mawili, huku kukiwa na nyaraka za wamiliki tofauti.



Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa uongozi wa kampuni ya Lake Group, inayomiliki viwanda vitatu vya kuzalisha nondo, mabomba ya kusambaza maji na kutengeneza mitungi, kabla ya kuweka mawe ya msingi kwenye viwanda hivyo, wilayani Kibaha, mkoani humo jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Tigo yakiwezesha chuo kikuu kompyuta

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Tigo imekabidhi kompyuta za mezani 20 kwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (Must) ambazo zitawanufaisha wanafunzi 4,630 wa chuo hicho.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo yaliofanyika jana, Mkurugenzi wa Tigo Nyanda za Juu Kusini, Henry Kinabo, alisema wana imani kompyuta hizo zitachangia sehemu kubwa kubadilisha wanafunzi na kuleta nafasi za kubuni teknolojia mpya na kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi.

"Tunaamini ya kwamba kompyuta tunazozitoa hapa leo, zitachangia sehemu kubwa katika kubadilisha jinsi wanafunzi wanavyosoma na pia zitaleta nafasi kwao kubuni teknolojia mpya," alisema.

Aliongeza kuwa Tigo iko mstari wa mbele kuboresha viwango vya elimu katika vyuo vikuu kwa kuleta nyenzo za kusomea na kuwasaidia wanafunzi na walimu kukuza vipengele muhimu vinavyohitajika katika karne hii ya 21 hasa katika teknolojia.

Kinabo alisema kupitia mchango huo, Tigo imeunga mkono juhudi za serikali katika mtazamo wake wa kubadilisha nchi kuwa ya viwanda na uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025, ambapo teknolojia ya habari na mawasiliano (Tehama) ndiyo chachu ya maendeleo hayo.

"Mwaka 2017 Tigo ilichangia kompyuta 47 katika Chuo Kikuu cha Dodoma, zilizowanufaisha wanafunzi takriban 36,150. Mpaka sasa wanafunzi 40,780 katika vyuo vikuu nchini wamenufaika na msaada wa kompyuta kutoka Tigo kwa kipindi cha miaka miwili sasa," alisema.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA NYUMBA INAUZWA**
Shamba ekari 13 lililopo Vikuruti barabara iendayo Bagamoyo lina matunda, maji ya dawasco na Kisima Kirefu. Piga simu: 0767 237404, 0715 237 404 na 0767 856900.

### NAFASI ZA KAZI

**Nafasi za Kazi**
Anahitajika - Mhasiibu
Sifa – Awe Mwanamke
Elimu – Diploma
Ofisi yetu ipo Posta – Dar es Salaam
Kwa Mawasiliano :- 0715 – 885 533


**NIPASHE NI JIBU LAKO**
NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0767 223311


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**(S.M.M 1994 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika Mahakama ya mwanzo **TEMEKE**
**USIMAMIZI WA MIRATHI 314/ 2019,**
Ombi la Robert Maria Pius Madidi kuteuliwa kuwa Msimamizi wa mirathi ya marehemu Pius Madidi.

Watu wote mnaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhuthuria kesi wakitaka, mnao tarehe 27-08-2019 kabla huyu mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa .
Tarehe ............

115375901

### KUPOTEA KWA CHETI



**Sonia Santu** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0283-0034** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2013 katika shule ya Sekondari John The Baptist.

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa Kituo cha Polisi.**

**Polisi Taarifa:**
**DAR/MBA/RB/210640/2016**

### TANGAZO LA KUPOTEZA KADI YA PIKIPIKI

**JOHN GWAGA** WA SLP 70 GEITA KIJIJI CHA NYARUGUSU WILAYA NA MKOANI GEITA ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA KING LION YENYE NAMBA ZA USAJILI MC 174 AWC RANGI NYEKUNDU CHASSIS NAMBA LTBPK8BG4F2K11648 NA ENGINE NAMBA KL157 FMI NA KUFUNGULIWA TAARIFA KUMBU NAMBA **NYR/RB/402** YA TAREHE 22/10/2018 KATIKA KITUO CHA POLISI NYARUGUSU – GEITA.

### PLOTI HEKARI MBILI INAUZWA MTONI KIJICHI-WILAYA YA TEMEKE

**Ploti hekari mbili inauzwa Mtoni**
Kijichi-wilaya ya temeke inafaa kwa biashara yeyote kubwa inafaa kwa kanisa na msikiti.

**Mawasiliano namba :**
**0778 742 848**

115375702

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Rajabu Rasuli Msangi** anatangaza kupotea kwa kadi yenye usajili wa namba T 233 CQS gari aina ya TOYOTA CAROLLA.
Yenye chasis namba NZE1213007319, Engine namba INZA068855.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**DAR/KIJ/RB/210433/2019**

215375802

**Katika Mahakama ya mwanzo Moshi Mjini**
**USIMAMIZI WA MIRATHI 71 2019,**

Ombi la Robert Greyson Mchome

Usimamizi wa mirath marehemu Rest Peter Rugiga.
Kwa yeyote anaehusika

Watu wote mnaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhuthuria kesi wakitaka, mnao tarehe 26-08-2019 kabla huyu mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa .

215376402

### KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**VENANCE PATRICE NJAU** amepotelewa na paspot ya kusafiria yenye namba **AB618968.**
Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa katika kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi;
**MOR/MOR/RB/204633/2019.**

215376802


*Kwa Habari Motomoto*
*usikose Gazeti lako la*
*Nipashe kila siku*
*Tupigie 0767 223 311*

**Nipashe**
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

**NEWSPAPER**
**CLASSFIED ADVERTISEMENT**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# STURRIDGE KUSAJILIWA UTURUKI

**ISTANBUL, Uturuki**

MCHEZAJI wa zamani wa Liverpool, Daniel Sturridge, anakaribia kujiunga na klabu ya nchini Uturuki ya Trabzonspor, kwa mujibu wa ESPN FC.

Klabu hiyo imetoa ofa kwa Sturridge ambayo gharama yake ni euro milioni 2 hadi tatu pamoja na bonansi.

Mama wa Sturridge na mjomba wake ambao kwa sasa wanafanya kazi kama mawakala wake, walisafiri kwenda jijini Istanbul Alhamisi na leo Ijumaa watafanya mazungumzo na Trabzon kwa ajili ya kukamilisha uhamisho huo.

Klabu hiyo ina matumaini kwamba itamsajili Sturridge ambaye kwa sasa hana timu yoyote tangu alipoachwa na Liverpool.

Sturridge mwenye umri wa miaka 29, pia alifanya mazungumzo na klabu ya nchini Marekani ya D.C. United, ingawa ripoti zaidi zinasema klabu hiyo imeamua kuachana na mpango huo.

Sturridge kwa kipindi chache cha uchezaji amatumia muda wake mwingi zaidi nchini England katika Ligi Kuu, akizichezea klabu za Manchester City, Chelsea na Liverpool.

Pia amewahi kuichezea kwa mkopo Bolton Wanders na West Bromwich Albion.

Alikuwa sehemu ya vikosi viwili tofauti vilivyoshinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambapo msimu wa 2010-11 alishinda akiwa na Chelsea na msimu uliopita alibeba taji hilo akiwa na Liverpool.

Pia alikuwa sehemu ya kikosi cha Chelsea kilichotwaa kombe la Ligi Kuu England msimu wa 2009-10.

Amecheza jumla ya mechi 306 na kufunga mabao 105, huku pia ameichezea timu ya taifa ya England mechi 26 akifunga mabao nane.

## BEN YEDDER ATUA MONACO

**MONACO, Ufaransa**

KLABU ya Monaco ya hapa Ufaransa imekamilisha usajili wa mshambuliaji wa kimataifa wa Ufaransa, Wissam Ben Yedder aliyejiunga akitokea Sevilla ya Hispania kwa mkataba wa miaka mitano.

Yedder alikuwa akihusishwa na kutakiwa na Manchester United kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili Agosti 8, lakini ameweza kuhama kutoka Hispania kwenda Ufaransa ambao bado hawajafunga usajili wao.

Monaco ilimaliza vibaya msimu uliopita wa Ligue 1, ikishika nafasi ya 17, ikiwa juu kwa pointi mbili kutoka katika janga la kushuka daraja, baada ya msimu 2017-18 kumaliza nafasi ya pili nyuma ya mabingwa PSG.

Katika dirisha hili Monaco wamekuwa katika jitihada kubwa za kujenga kikosi chake kwa kumsajili Henry Onyekuru kutoka kwa Everton na kuwakopesha Djibril Sidibe, huku wakimuuza Youi Tielemans kwa Leicester.

Ben Yedder ni mchezaji mpya aliyewasili baada ya kucheza kwa miaka mitatu Sevilla, akiwa amefunga mabao 70 katika mechi 138, za mashindano yote.

Mshambuliaji huyo mwenye miaka 29, amewahi kucheza Ufaransa kwa miaka sita katika klabu ya Toulouse akiwa amefunga mabao 63, katika mechi 156 za Ligue 1.

“Nimefurahi kuhusishwa na AS Monaco,” Ben Yedder aliiambia tovuti ya klabu hiyo. “Najiona mwenye bahati kwa kufuatwa na klabu hii.

“Nimeichagua Monaco kwa sababu naamini ina mipango mikubwa na naamini nitafanya kila niwezalo kutimiza malengo yetu.

“Nimekuja kwa lengo la kuthibitisha ubora wangu, wakati wote matamanio yangu ni kufikia malengo ya juu zaidi.

“Napenda kushukuru kwa klabu kwa kuniamini. Ni siku nzuri inayoanza na hadithi mpya ndicho kitu nisichotaka kupoteza muda kuanza.”

## SANCHEZ KUONDOKA KABLA YA DIRISHA KUFUNGWA

**MANCHESTER, England**



MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Alexis Sanchez inaaminiwa anataka kuondoka hapo Old Trafford kabla ya kufungwa kwa pazia la dirisha la usajili wa kipindi cha majira ya joto.

Kwa mujibu wa Daily Mail, klabu za ligi kuu ya nchini Italia, Serie A, ndiko anakoweza kwenda kucheza kwa mkopo kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili.

Sanchez hadi sasa ameshindwa kuthibitisha ubora wake hapo United tangu alipotua akitokea Arsenal Januari mwaka 2018 akiwa amefunga mabao matano tu kwa kipindi cha miezi 18.

Kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer alisisitiza wiki iliyopita kwamba, Sanchez yupo katika mipango yake msimu huu, na anachosubiria kwa sasa ni kupona kwanza majeruhi yake.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Chile anauguza majeruhi aliyoyapata wakati wa michuano ya mataifa ya Amerika Kusini, Copa America.

Zaidi ni kwamba, gazeti la The Times limeripoti kuwa Sanchez mwenyewe kwa sasa anataka kuondoka hapo United kabla ya kufungwa kwa dirisha hili la kipindi cha majira ya joto.

Klabu za Juventus, Napoli, Milan na Inter Milan ndio zinazotajwa kwamba zinawania kumsajili kwa mkopo.




# LINDELOF

## KUONGEZEWA MSHAHARA MAN UNITED

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United ipo tayari kumwongezea mshahara mara mbili zaidi beki Victor Lindelof ili alipwe pauni 150,000 kwa wiki, kwa mujibu wa gazeti la Daily Mirror.

Kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer anataka kumfanya Lindelof kuwa beki wa kati wa muda mrefu na patina na Harry Maguire aliyesajiliwa hivi karibuni kwa pauni milioni 80.

Lindelof na Maguire walitengeneza upatina mzuri zaidi wakati wa mchezo wao wa kwanza wa ufunguzi wa Ligi Kuu wakicheza pamoja Jumapili na kuweza kuibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Chelsea.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 raia wa Sweden, alisajiliwa kwa pauni milioni 30 akitokea Benfica mwaka 2017, ameonekana kurudi kwenye kiwango chake hapo Old Trafford baada ya kuwa na mwanzo mbaya.

Lindelof amebakiwa na miaka miwili kwenye mkataba wake wa sasa ambao unamfanya alipwe pauni 75,000 kwa wiki huku kukiwa na kipengele cha kumwongezea miezi 12.

United kwa sasa wapo tayari kumpa ofa ya mkataba wa miaka mitatu Lindelof ambao utamfanya alipwe pauni 150,000 na kuendelea kukaa hapo Old Trafford hadi mwaka 2025.

# Iwobi: Nitatengeneza jina langu Everton

**LIVERPOOL, England**

ALEX Iwobi amejipanga kutengeneza jina lake baada ya kukamilisha uhamisho wa pauni milioni 30 kutoka Arsenal na kujiunga na Everton wakati wa siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la usajili wa kipindi cha majira ya joto nchini England.

Winga huyo alikuwa mchezaji wa saba wa kocha Marco Silva kusajiliwa kipindi hiki cha majira ya joto, akijiunga na Jean-Philippe Gbamin, Moise Kean, Andre Gomes, Fabian Delph, Jonas Lossl na Djibril Sidibe pale kwenye dimba la Goodison Park.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Nigeria alipewa mkataba na timu ya wakubwa ya Arsenal mwaka 2015 baada ya kuanzia hapo akiwa kinda, huku akifunga mabao 15 katika mechi 149 alizoichezea Arsenal, na sasa ameelezea nia yake ya kujitengenezea historia yake kwa Toffees hao.

"Nimezungumza na kocha kuhusu mipango yangu na amenielewa," amesema Iwobi akiambia Everton TV.

"Ofa yao ilinivutia mno na nisingeweza kuipiga chini. Kocha alikuwa ananiambia mimi, "Kuna nafasi kwa ajili yako, na utakupa nafasi."

"Mara zote nilikuwa nachukuliwa kama mchezaji kijana pale Arsenal, matumaini yangu uhamisho huu utanifanya nitengeneze jina langu kwenye Ligi Kuu ya England na kutengeneza historia yangu na Everton."

"Huu ni muda wangu wa kuwa na hamasa hapa Everton. Nilikuwa na nafasi ya kuangalia wachezaji ambao wamenunulia hapa, wengine ni wachezaji wenye vipaji vikubwa," alisema.

"Sio mimi peke yangu. Kuna wachezaji wangine ambao wana vijaji vikubwa walikuwa hapa kabla ya hata kusajiliwa wengine. Kocha anawajua wachezaji wengi na hivyo tutakuwa na wakati mzuri wa kufanya makubwa na klabu hii.

"Nina matumaini pia Moise Kean atafanya makubwa hapa tukiwa wote."




# Bayern kumchukua Sane Januari

**MUNICH, Ujerumani**

USAJILI wa Leroy Sane kutoka Manchester City kwenda Bayern Munich unaweza kukamilishwa Januari mwakani, licha ya mchezaji huyo kuumia goti, kwa mujibu wa vyombo vya habari vya Ujerumani.

Winga huyo wa kimataifa wa Ujerumani aliumia goti la mguu wa kulia wakati wa mchezo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Liverpool mwanzoni mwa mwezi huu na sasa amelazimika kufanyiwa upasuaji.

Licha ya kuwa hofu kwamba anaweza kuwa nje ya dimba kwa kipindi cha miezi sita au saba kwa msimu huu, mabingwa hao wa Bundesliga bado wanaweza kumsajili mchezaji huyo wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari.

Miamba hao wa soka la Ujerumani wana machaguo matatu ya uwezekano wa kumsajili mchezaji huyo kwa mujibu wa gazeti la Bild.

Wanaweza kumsajili kipindi hiki cha majira ya joto kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili Septemba 2 au wakati wa dirisha dogo la Januari ama kipindi cha majira ya joto mwakani, ambapo atakuwa anamaliza mkataba wake na City.

Bayern imeripotiwa kwamba ipo tayari kumlipa Sane mshahara wa pauni 400,000 kwa wiki ili kuweza kumshawishi aondoke hapo kwenye dimba la Etihad.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR ACHELEWESHWA NA MADOGO REAL, BARCA

Ni Semedo na Vinicius ambao PSG inataka wajumuishwe, hata hivyo Real inanukia kumpata, lakini...

**PARIS, Ufaransa**

Barcelona na Real Madrid zimetuma ofa ambazo zimeonekana hazina mashiko kwa Paris St-Germain, wakati miamba hiyo ya Hispania yote ikigonga mwamba wa kuipata saini ya mshambuliaji wa kimataifa wa Brazil, Neymar, imeeleza BBC Radio 5.

Klabu ya zamani ya Neymar, Barcelona inaaminika kutoa ofa ya euro milioni 100 sawa na pauni milioni 92.4 pamoja na Philippe Coutinho.

Ivan Rakitic pia alijadiliwa kama sehemu ya kuhusishwa katika mpango huo na klabu hiyo ya Ufaransa ili kumtoa nyota wao wa Brazil mwenye umri wa miaka 27.

Lakini kwa mujibu wa Mail Online, PSG imependekeza kwa Barca kwamba itakuwa tayari kuiachia Neymar endapo tu miamba hiyo ya Camp Nou itakubali kutoa pauni milioni 93 sambamba na Coutinho, Rakitic, huku iking'ang'ania pia kujumuishwa kwa beki dogo wa kulia Mreno Nelson Semedo, 25.

Kwa upande mwingine Real Madrid nayo ilitoa ofa yake ya fedha taslimu ikimjumuisha Gareth Bale na James Rodriguez.

Lakini PSG nayo ikataka ajumuishwe dogo Vinicius Junior, 19, katika mpango huo lakini, hata hivyo Real haikuliweka jina hilo katika dili hilo.

Hata hivyo, Gazeti la AS, limeripoti kuwa Real Madrid imekataa ombi hilo la Paris St-Germain la kutaka Vinicius Junior, kujumuishwa katika dili hilo la Neymar.

Mbali na Vinicius, PSG pia ipo tayari kwa Real Madrid kumjumuisha kiungo Mcroatia Luka Modric, 33, na kiungo Mbrazil Casemiro, 27, katika ofa hiyo, kwa mujibu wa Gazeti la Marca.

Hakuna ofa yoyote iliyokubaliwa, lakini inadhaniwa PSG itapendelea kumuuza kwa Real Madrid.

Neymar alikuwa mchezaji ghali zaidi duniani mwaka 2017 wakati PSG ilipolipa euro milioni 222 sawa na pauni milioni 205 aliponunuliwa kutoka Barcelona.

## KWA UFUPI

**SANCHEZ AMTESA SOLSKJAER**
Alexis Sanchez amekataa kuondoka Manchester United majira haya ya joto, licha ya kocha Ole Gunnar Solskjaer kumtishia kumshusha kujifua na wachezaji wa akiba kama atabaki, na Roma kwa sasa inatazama mbadala mwingine. ***(Sun)***

**COUTINHO ANA NAFASI PSG**
KIUNGO mshambuliaji wa Brazil, Philippe Coutinho, 27, bado anaweza kujiunga na PSG katika mpango mwingine wa uhamisho usiomjumuisha na dili la Neymar. ***(Goal)***

**ROSE KUONDOKA SPURS JANUARI**
BEKI wa kushoto wa England, Danny Rose, 29, hataki kuondoka Tottenham hadi Januari, wakati huu beki huyo bado akiwa sehemu ya mipango ya kocha Mauricio Pochettino. ***(Football. London)***

**ARSENAL YASUBIRI ASILIMIA 10**
Arsenal inajianda kupokea asilimia 10 ya mauzo ya kiungo wake wa zamani Jeff Reine-Adelaide, aliyeuzwa kwa pauni milioni 23.1 kwa Lyon akitokea Angers. (Ouest France, via Sun)

**SPURS YAMPOTEZEA DYBALA**
Spurs haivutiwi tena na kiungo mshambuliaji wa Juventus, Paulo Dybala, 25, licha ya Muargentina huyo kuendelea kuonyesha nia ya kuondoka Serie A. ***(Di Marzio - in Italian)***

**LINDELOF KUJIFUNGA UPYA UTD**
BEKI wa kati wa Manchester United na Sweden, Victor Lindelof, 25, anajiandaa kuanguka wino mkataba mpya ambao utamfanya kulipwa zaidi ya pauni 75,000 kwa wiki anazopokea kwa sasa. ***(Aftonbladet - in Swedish)***

**BAYERN KUMRUDIA TENA SANE**
Bayern Munich inaweza kurejea mpango wake wa kumsajili winga wa Manchester City na Ujerumani, Leroy Sane licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, kusumbuliwa na majeraha ya goti ambayo yatamweka nje ya uwanja kwa kipindi hadi cha miezi saba. ***(Bild - in German)***

**BALOTELLI AIGEUKIA BRESCIA**
MSHAMBULIAJI wa Marseille na Italia, Mario Balotelli, 29, anajiandaa kutia saini mkataba wa miaka mitatu na miamba ya Serie A, Brescia baada ya kukataa ofa kutoka klabu ya Flamengo ya Brazil. ***(Guardian)***

**MILAN, JUVE, NAPOLI ZATUA UTD**
MIAMBA ya Serie A, AC Milan, Juventus na Napoli zinavutiwa kuipata saini ya mshambuliaji wa kimataifa wa Chile, Alexis Sanchez, 30. ***(Mail)***

**STURRIDGE KUTIMKIA UTURUKI**
STRAIKA wa zamani wa Liverpool, Daniel Sturridge, 29, anaonekana kujiandaa kuanguka wino wa kuichezea Trabzonspor ya Uturuki katika dili linaloelezwa litagharimu euro milioni tatu sawa na pauni milioni 2.8 kwa msimu. ***(Goal)***

**IWOBI: SABABU KUSEPA ARSENAL**
WINGA wa Everton na Nigeria, Alex Iwobi, 23, amesema aliondoka Arsenal siku ya mwisho kabla ya dirisha la usajili wa majira haya ya joto kufungwa England kudhibitishwa kuwa yeye si kipaji kinachoibukia tu. ***(Mirror)***

**DORTMUND YAMFUNGUKIA SANCHO**
Borussia Dortmund imekataa ofa kibao majira haya ya joto kutoka kwa klabu nyingi za Ulaya zilizokuwa zikihitaji huduma ya winga wa kimataifa wa England, Jadon Sancho, ambaye aliripotiwa kuwindwa na Manchester United. ***(Ruhr Nachrichten - in German)***

## HABARI MICHEZO

# AZAM FC YAIFURAHIA SIMBA JUMAMOSI

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha Azam FC kitashuka Uwanja wa Taifa kesho kuivaa Simba kikiwa na malengo mawili, kwanza kutafuta taji la kwanza msimu huu na pili kuitafutia kasi Fasil Kenema ya Ethiopia zitakaporudiana kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Azam na Simba zitakutana kesho Uwanja wa Taifa kwenye mechi ya kuwania Ngao ya Jamii kabla ya Agosti 24, mwaka huu kuwa na kibarua kigumu cha kupindua matokeo ya bao 1-0 dhidi ya Fasil Kenema ambayo ilibuka na ushindi kwenye mechi ya kwanza kwao, lakini pia Wekundu wa Msimbazi hao wakiutumia mchezo huo kujianda na mechi ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya UD Songo ya Msumbiji baada ya kulazimisha sare tasa ugenini.

Jana usiku Azam ilianza kuitafutia kasi Simba baada ya kushuka katika Uwanja wao wa Chamazi kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Namungo FC.

Na juzi Msemaji wa Azam FC, Jafari Maganga alisema mipango yao ni kuhakikisha wanafika mbali na kuwania taji hilo, pia wanapata mazoezi kutoka kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu, Simba kuelekea mechi yao muhimu ya Kombe la Shirikisho dhidi ya Fasil Kenema

"Mechi dhidi ya Simba ni muhimu sana kwetu na si tu kwa ajili ya kuwania taji hilo ambalo linaweza kuwa la kwanza kwetu msimu huu, bali pia itampa nafasi Kocha Etienne Ndayiragije kurekebisha makosa yake kabla ya mchezo wetu wa Kombe la Shirikisho.

"Tunatambua utakuwa mchezo mgumu, kwa kuwa Simba ni mabingwa wa Ligi Kuu, lakini pia walifika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliopita, hivyo itakuwa mechi nzuri kwa wachezaji wetu kuelekea mchezo wetu wa marudiano dhidi ya Fasil Kenema," alisema.

Alisema lengo lao ni kushinda mechi ya marudiano dhidi ya Waethiopia hao, huku akiwataka mashabiki kujitokeza kwa wingi siku hiyo kuipa sapoti Azam FC ili iweze kupeperusha vema bendera ya Tanzania.

Azam inahitaji ushindi wa zaidi ya bao moja huku ikihakikisha haitoi nafasi kwa Fasil Kenema kupata bao ili kuweza kusonga mbele.

Endapo itafanikiwa kusonga mbele itakutana na mshindi wa jumla kati ya Triangle UnitedFC ya Zimbabwe na Rukinzo FC ya Burundi.



Kipa namba mbili wa Liverpool, Adrian akimdhibiti Mateo Kovacic kufunga katika mechi UEFA Super Cup iliyopigwa Istanbul, Uturuki juzi na Liverpool kushinda kwa mikwaju ya penalti 5-4 kufuatia matokeo ya mabao 2-2 ndani ya dakika 120. **PICHA: DAILY MAIL**

## Usajili Ligi Z'bar kwa vitambulisho uraia

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limezitaka timu kuhakikisha majina ya wachezaji wao kupitia vitambulisho vya uraia au vyeti vya kuzaliwa ili kuepusha changamoto za mabadiliko ya majina katika fomu za usajili na yale yaliyopo katika vitambulisho hivyo.

Hayo yameelezwa na Mkurugenzi wa Kamati ya Mashindano ya Shirikisho hilo, Ali Mohammed wakati akizungumza na gazeti hili katika mchakato wa kupitia fomu za uhamisho na usajili kwa wachezaji.

Alisema katika mchakato huo, changamoto iliyopo ni kutofautiana majina katika fomu mama na fomu ya uhamisho jambo linalowachanganya kutokana na mchezaji mmoja kuwa na majina hadi matatu tofauti.

Alisema karibu timu zote zilizofanya zoezi hilo, kumejitokeza tatizo la majina jambo ambalo linaweza kuleta mkanganyiko pindi timu hizo zitakapotaka kusafiri kwenda nje ya nchi kwa michuano ya kimataifa.

"Mfano mchezaji katika fomu mama anaitwa Mohammed (yenye herufi 'M' mbili), lakini fomu ya uhamisho kuna Mohamed (yenye herufu 'M' moja), haya ni majina mawili tofauti, au utakuta fomu ya uhamisho Saidi (yenye 'I' mwisho) lakini fomu mama Said (inakuwa haina 'I') Sasa hii inaweza hata kuleta tabu timu zitakapotaka kusajili na hili lishawahi kujitokeza, wapo wachezaji ambao fomu zao jina la pili limeandikwa kifupi mfano "S" hii haikubaliki," alisema.

# Eritrea, Burundi kukata utepe Cecafa U-15 leo

**Na Somoe Ng'itu, ERITREA**

TIMU ya soka ya vijana ya umri chini ya miaka 15 ya Eritrea inatarajia kuwakaribisha yosso wenzao kutoka Burundi katika mechi ya ufunguzi ya mashindano ya Afrika Mashariki na Kati itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Asmara nchini hapa.

Mashindano haya ya U-15 yanafanyika kwa mara ya kwanza kwenye ukanda huu chini ya usimamizi wa Baraza la Soka la Afrika Mashariki na Kati (Cecafa).

Mechi nyingine itakayochezwa leo mapema kuanzia saa 8: 00 mchana kwa saa za hapa (sawa na Tanzania), itakuwa ni kati ya vijana wa Kenya dhidi ya Somalia.

Akizungumza na gazeti hili jijini Asmara jana, Katibu Mkuu wa Cecafa, Nicholas Musonye, alisema jana kuwa maandalizi ya mashindano hayo yamekamilika na jumla ya timu 10 zinatarajiwa kuchuana kuwania kombe hilo zikiwa zimepangwa kwenye makundi mawili.

Musonye alisema kuwa sasa Kundi A litakuwa na Eritrea, Kenya, Somalia, Sudan na Burundi wakati Uganda, Rwanda, Sudan Kusini, Ethiopia na Tanzania zinaunda Kundi B.

"Sasa kila timu itapata nafasi ya kucheza mechi nne katika hatua ya kwanza ya makundi, na baada ya hapo, timu mbili zitakazofanya vizuri kutoka kila kundi zitatinga hatua ya nusu fainali ya mashindano hayo, mabadiliko ya ratiba yametokana na Djibouti kutangaza kujitoa katika dakika za mwisho, " alisema Musonye.

Aliongeza kuwa fainali za michuano hiyo sasa zitachezwa Agosti 30, mwaka huu na kuzipongeza Eritrea na Ethiopia kwa kushirikiana kuandaa mashindano haya ambayo yanalenga kuziandaa timu za Cecafa katika mashindano yajayo ya vijana ya Afrika na dunia.

## Manungu, Mabatini vyafungiwa Ligi Kuu

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI msimu mpya wa Ligi Kuu Bara 2019/20, ukitarajiwa kuanza rasmi Agosti 23, mwaka huu, Bodi ya Ligi imevifungia viwanja vitatu kutumika, imeelezwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Ligi Kuu, Boniface Wambura jana alitaja viwanja walivyovifungia kutokana na kuhitaji kwanza kufanyiwa marekebisho kuwa ni Uwanja wa Mwadui (Shinyanga), Manungu (Morogoro) na Mabatini (Pwani).

Alisema viwanja vivyo havitatumika hadi vitakapofanyiwa matengenezo na bodi hiyo kujiridhisha kabla ya kuruhusu tena kuanza kutumika.

Kutokana na kufungiwa kwa viwanja hivyo, itabidi Mtibwa Sugar inayotumia Uwanja wa Manungu kwa mechi zake za nyumbani, Ruvu Shooting (Mabatini) na Mwadui FC (Mwadui Complex) kusaka viwanja vingine hadi hapo vitakapofanyiwa marekebisho.

# Michezo

Ijumaa Agosti 16, 2019
Nipashe



**Neymar acheleweshwa na madogo Real, Barca** HABARI UK 30

**NDOO YA KWANZA...**



Nahodha wa Liverpool, Jordan Henderson, akisherehekea na wachezaji wenzake kwa kunyanyua juu taji la UEFA Super Cup baada ya kulitwaa juzi kwa kuifunga Chelsea kwa mikwaju ya penalti 5-4 kufuatia sare ya mabao 2-2 ndani ya dakika 120 katika mechi iliyopigwa Istanbul, Uturuki juzi. Hilo ni kombe la kwanza kwa klabu hiyo msimu huu wa 2019/20 kufuatia mapema mwezi huu kuikosa Ngao ya Jamii England kwa kufungwa kwa penalti na Manchester City. **PICHA: MTANDAO**

# GONJWA LA SIMBA, YANGA CAF HILI HAPA

## Zahera atafuta tiba Kilimanjaro akitumia mikanda ya video, Aussems apanga kumalizana na Azam FC kwanza kisha...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI timu kongwe nchini, Simba na Yanga zikiwa katika maandalizi makali kuelekea mechi zao za Ligi ya Mabingwa Afrika zinazotarajiwa kupigwa mwishoni mwa wiki ijayo hapa nyumbani na ugenini, gonjwa lililozitafuna na kupata matokeo ya sare mechi zao za awali, limebainika.

Katika mechi hizo za raundi ya awali, Simba ambayo ilianzia ugenini nchini Msumbiji, itakuwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam kuikaribisha UD Songo wakati Yanga iliyoanzia nyumbani itaifuata Township Rollers katika mchezo utakaopigwa Gaborone, Botswana.

Kocha wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems anajivunia kupata sare ugenini na kutoruhusu bao, jambo ambalo ameahidi kukiandaa kikosi chake kuendelea kutoruhusu mabao ugenini na kuhakikisha nyumbani anashinda.

"Kwa sasa akili yangu na mipango yote ipo katika mechi ya Ngao ya Jamii dhidi ya Azam, na baada ya hapo tutaanza kujiandaa na mchezo wa marudiano dhidi ya UD Songo, msimu huu nina kikosi imara na tunaweza kucheza mfumo tofauti na kutoruhusu mabao ugenini," alisema Aussems.

Kwa upande wa Kocha wa Yanga, Mwinyi Zahera, leo ataiongoza timu yake katika mechi ya kirafiki dhidi ya Polisi Tanzania itakayopigwa Uwanja wa Ushirika mjini Moshi, lengo likiwa ni kujiandaa na mechi ya marudiano dhidi ya Township Rollers.

"Bado kuna makosa ambayo nayafanyia kazi ikiwa ni pamoja na kuangalia mikanda ya video ili kuweza kubaini zaidi namna wapinzani wetu wanavyocheza.

"Tayari tulishaangalia mara moja jana (juzi), lakini tutaangalia tena kwa mara ya pili ikiwa ni pamoja na kuendelea kufanyia kazi kile tunachokiona uwanjani," alisema Zahera.

Hata hivyo, wawakilishi hao wa Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa timu zao zinaundwa na wachezaji wazuri na wenye vipaji, na kwa mujibu ya wachambuzi wetu, kushindwa kupata matokeo kwa timu hizo katika mechi hizo za awali kumechangiwa na mambo mengi yakiwamo...

**WACHEZAJI WENGI WAPYA**

Simba na Yanga zimesajili wachezaji wengi wapya, ambao bado hawajawa na muunganiko mzuri jambo ambalo zilitakiwa kucheza mechi nyingi za kirafiki ili kupata muunganiko huo, lakini pia katika mechi zao za awali zilitakiwa kutumia nyota wengi wa msimu uliopita ambao tayari wanaelewana.

Yanga ndiyo iliyoongoza kwa kuchezesha wachezaji wengi wageni, tofauti na wale waliokuwa kwenye kikosi hicho msimu uliopita. Ni wachezaji wawili wa zamani tu ambao walianza mechi hiyo ambao ni Paul Godfrey na Papy Tshishimbi pekee, huku Mrisho Ngassa akiingia kipindi cha pili.

Zahera alikiri kuwa kilichowamaliza ni kutokana na kukosekana kwa muunganiko jambo ambalo limemlazimu kutafuta mechi mbili za kirafiki, ya leo dhidi ya Polisi Tanzania kabla ya Jumapili kuivaa FC Leopards ya Kenya Uwanja wa Sheikh Amri Abedi jijini Arusha.

Kama ilivyo kwa Yanga, Simba nayo iliathiriwa na hali hiyo, ingawa si sana kwa sababu Aussems alijitahidi sana kutopanga wachezaji wengi wageni na badala yake akaziba mapengo ya wachezaji ambao wameondoka.

Kukosekana kwa Aishi Manula ambaye ni majeruhi, kulitoa nafasi kwa Beno Kakolanya, huku Gadiel Michael akipewa nafasi kutokana na mipango ya kocha, lakini Sharaf Eldin Shiboub, Francis Kahata na baadaye Deo Kanda walitumika.

**KUKOSA VIKOSI VYA KWANZA**

Michuano ya Ligi ya Mabingwa pamoja na Shirikisho barani Afrika ilianza mapema kabla ya Ligi Kuu Tanzania Bara haijaanza, nalo limekuwa ni tatizo kwa wawakilishi wa Tanzania kwenye kinyang'anyiro hicho cha kimataifa kutokana na wachezaji kukosa muunganiko na kasi kwani vikosi bado vilikuwa havijaelewana.

Kama ligi ingekuwa imewahi kuanza na timu hizo kucheza mechi kama tano za Ligi Kuu Bara, ni wazi wachezaji wangekuwa na kasi na muunganiko wa kutosha huku makocha wakipata vikosi vyao vya kwanza.

Mazoezi na mechi za kirafiki walizocheza timu hizo ikiwa ni pamoja na Azam FC na KMC FC zinazoiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho bado zilikuwa hazitoshi kwa makocha kupata vikosi vya kwanza kutokana na kutocheza mechi za kimashindano.

**ZAHERA KUCHELEWA KURUDI**

Yanga pamoja na kuonekana ina baadhi ya wachezaji wapya wenye uwezo mkubwa, lakini bado inaathiriwa na vitu vingi vya kiufundi na hii inasababishwa na Kocha Mkuu, Zahera kuchelewa kurejea kutoka kwenye mapumziko, kutokana na kurejea wiki moja tu kabla ya timu yake kuanza michuano hiyo.

Pamoja na matokeo ziliyoyapata kwa Simba na Yanga, huku Azam FC nayo ikichapwa bao 1-0 ugenini Ethiopia dhidi ya Fasil Kenema na KMC ikitoka sare tasa ugenini Rwanda dhidi ya AS Kigali, bado zinaweza kusonga mbele kwa kupata matokeo kwenye mechi za marudiano mwishoni mwa wiki ijayo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002